

YESU PEKEE

Desmond Ford

Ph.D., M.S.U.

Ph.D., Manchester

Kufupishwa na kilichorahisishwa na Ritchie Way

Haki zote zimehifadhiwa. Desmond Ford 2014

Hakuna sehemu ya kazi hii iliyo ruhusiwa kunakiliwa, kuhifadhiwa kwa namna yoyote au kuonyeshwa kwa jia yoyote kwa namna ya kielektroniki, kuandikwa, kuchapishwa, kunakiliwa au kunaswa kwa njia yoyote pasipo idhini kwa maandishi kutoka kwa mmliki wa kazi hii.

Jadala na utunzi wa ndani: Umefanywa na Darren Baker Bare Graphics.

Kitengo: kitabu cha kikristo/maisha ya kikristo/ na ni cha uvuvio.

Kimetafsiriwa na: Mch Boaz Nyariki, Mch Peter Morwabe, Mch Patrick Masita, pamoja na Ndugu Joash Nyasende

Picha kwenye Jalada: Raphael wa the Miraculous Draught of Fishes(1515) (PD-Art) faithful Reproduction.

Mpiga picta: M. Choham

Hati kuundwa kwa: Linda Ruth Brooks Publishing
ISBN: 978-1495925887

Kitabu hiki kinalenga Kristo, msalaba, na injili. Kinazingatia utimilikaji wa ahadi ya mungu iliyofanywa sawa kwa zaidi ya miaka elfu tatu iliyopita. Mungu aliahidi ya kwamba ataishi na kutembea pamoja nasi, na kuwa angekuwa mungu wetu nasi kuwa watu wake. Ahadi hiyo ilitimilika ndani ya Yesu ambaye alikuwa Mungu pamoja nasi. Yesu alikuja kutuonyesha vile mungu alivyo. Alitwaa dhambi zetu na kujivika, na pale msalabani alilaaniwa na kuhukumiwa kwazo ili sisi tuwe huru kutokana na hiyo hukumu. Na hivyo ndivo mungu alivyo.

Katika kitabu hiki “Yesu pekee”, kuna vito vya injili ambavyo havipatikani kwagineko- vito ambavyo vinakutia shime kumtukuza mungu kwa upendo na hekima yake kuu.

Daktari Desmond Ford ameandika vitabu vingi kuhusu injili ya Kristo. Taasisi yake ‘Good News Unlimited’, inachapisha jarida, inatoa mahubiri ya video kwenye mtandao, na inadhamini huduma za ibada.

www.goodnewsunlimited.com

“Wakainua macho yao wasimuone mtu ila Yesu peke yake”
Matt. 17:8

YALIYOMO

| | |
|---|-----|
| 1: Yesu Mungu Mtu | 5 |
| 2: Ulimwengu Wa Yesu: Mahali, Watu Na Wakati | 10 |
| 3: Ubatizo Wa Yesu Mpaka Juma Lake La Mwisho..... | 15 |
| 4: Yesu Aingia Kwa Kishindo..... | 28 |
| 5: Yesu Afundisha Injili Kwa Mataifa (Wayunani) | 32 |
| 6: Hukumu Ya Yesu Kuhusu Dini Mbaya..... | 36 |
| 7: Unabii Wa Yesu Kuhusu Siku Za Mwisho | 40 |
| 8: Yesu Awatawadha Wanafunzi | 46 |
| 9:Yesu Aeleza Kuhusu Pasaka | 47 |
| 10: Yesu Asema Msifadhaike | 49 |
| 11: Yesu Mzabibu Wa Kweli..... | 52 |
| 12: Ujumbe Wa Maagano Wa Yesu | 55 |
| 13: Ombi La Mwisho La Yesu..... | 57 |
| 14: Yesu Akiwa Gethsemane | 59 |
| 15: Yesu Ajaribiwa..... | 69 |
| 16: Yesu Mbele Ya Kayafa | 72 |
| 17: Yesu Mbele Ya Pilato | 75 |
| 18: Yesu Au Baranaba | 78 |
| 19: Yesu Msalabani | 82 |
| 20: Maneno Saba Yesu Msalabani..... | 86 |
| 21: Nyuso Zilizozunguka Msalaba..... | 93 |
| 22: Mafundisho Yatokayo Msalabani..... | 96 |
| 23: Yesu Apumzika Kaburini..... | 102 |
| 24: Kaburi La Yesu Li Wazi | 104 |
| 25: Yesu Akiwa Galilaya..... | 107 |

1: Yesu Mungu Mtu

Mtu wa mvuto zaidi kwenye historia ni yesu Kristo. Leo hii thuruthi moja (1/3) ya watu wote duniani wanamtambua mmoja aliyeigawa historia kuwili kwa mfano kabla na baada ya Kristo (BC na AD)

Tusidhubutu kumsawazisha kristo na mulka za viongozi wengine wa dini. Hao ni tofauti kadiri ya mchana na usiku. Pekua kuran na hautapata jina Mohammed, pekua waandishi wa zamani ya Buddha na jina Buddha halionekani. Lakini soma agano jipya na utalipata neon Kristo katika karibu kila ukurusa napengine zaidi ya mara moja.

Msomi maarufu W Griffith Thomas aliandika kwamba Ukristo ndiyo dini pekee duniani ambayo nguzo zake zimekitwa kwa mwanzilishi wake.

Hebu tafakari; Kristo ndiye mtu pekee aliywahi kuishi akidai kuwa Yesu ni Mungu huku akihesabiwa mtu timamu wa walitukuka katika kizazi chake. Mvuto wake ulikuwa mkuu kuliko wengine wote.

Mwanafulsafa sucrates alifundisha kwa miongo mine, pilato kwa nusu karne na alistotohe kwa miaka arobaini la kwa kuwajumuisha, mvuto wao wote haukufikia mvuto wa yesu alioweka kwa miaka mitatu na nusu ya huduma yake.hakuna mwalimu mwengine aliyeacha nje vitu visivyo vyaa maana katika mafundisho yake wala hakuna aliyechagua maswala yanayohusu umilele.

Ni mwalimu mwengine yupi aliyethubutu kutazamia kwamba mafundisho yake yangedumu milele? Yesu alisema ‘mbingu na nchi zitapita, ila maneno yangu hayatapita kamwe’ (Matt 24:35), na kila siku inadhihirisha upya ukweli wa dai hili.

Kila kizazi kipyaa kinapata kwenye mafunzo ya yesu kila kilicho kipyaa na cha kutia shime. Kama tunavyotazama katika

karne zote tunaona vile ambavyo maneno yake yamehitimu kuwa sheria, mafundisho ya kanisa, yamekuwa mithali, na maneno ya faraja lakini hayawahi pita. Je, ni mwalimu yupi mwanadamu aliyewahi kudai kwamba maneno yake yangedumu milele yote?

Mungu alitamka semi nyingine nyingi zionyeshazo ufahamu wake kuhusu mvuto wake. Hakuna mwalimu mwininge aliyewahi kutenda hilo. Tafakari haya, "Mimi ndimi nuru ya ulimwengu ye yote isipokuwa Kristo, ingelichukuliwa kama utani. Isingeweze kana tamko hili liendelee kuwa kweli hata baada ya karne ishirini kama Kristo angekuwa mtu wa kawaida kutoka kwa mgalilaya huyu kumetokea chemic hemi za uzuri zizizokoma kwa ubora wa mwanadamu. Hakuna mwininge amewahi kuwa wa manufaa ya namna hii kwa wanadamu wote.

Tungelitafuta kutoka katika hifadhi za usanii, fasihi, historia, vitendo vya Usamaria Wema, msaada kwa wasiojiweza, vilivyoanzishwa au kuhuishwa na yesu kuna pengo kubwa! Yesu alisema "nikiinuliwa juu nitawavuta wengi kwangu (John 12:32) Usemi huu waonyesha kwamba maisha ya Ukristo ni kuhusu mtu na wala si falsafa mtu mwenyewe ni seremala wa Nazareti mara nyingine katika taasisi na dini, tunagundua nguzo zake zi kwenye dhana na si mtu. Sembuse ukristo kiini cha ukristo hasa ni mtu, yesu kristo.

Kumbukumbu ya wahusika wakuu duniani inaleta taswira ya heshima na kicho ila si upendo wa kibinagsi. Fikiria mvuto wa Musa, Daudi, Socrates, Pilato na mamia ya majina makuu wa karne mbili zilizopita, hakuna wa kufanana na mvuto wa yesu.

Fikiria hakikisho la yesu ya kwamba atakuwa na kanisa la milele licha ya uwepo wa samaki walioooza na magugu (Mat 16:18; 13:37-40; 47:47-50). Na huku, ukijumulisha ujasiri wake kwenye utume mkuu wa kuhubiri injili kwa ulimwengu wote

ambao utawatia shime wake kwa waume hadi mwisho wa dahari (Matt 28:19-20) matendo 1:8. Tunasissitiza kwamba katika fasihi na historia yote hakuna mafanano na usahihi wa matazamiao hayo ya mda mrefu.

Sasa fikiria madai ya mhazareti huyu aliyekuwa masikini na kwa mtazamo wa mwanadamu asiye na nguvu. Huyu mtu alidai yafuatayo:

1. Ya kwamba mamlaka yote mbinguni na duniani ni yake (Matth 28:18-20)
2. Ati alikuwa na mamlaka yote juu ya uumbaji (Mark 4:39,41)
3. Malaika wote wa mbinguni ni wake (matayo 16:27)
4. Kwamba watu wanapaswa kumpenda zaidi ya jamii zao na hata maisha yao (matayo 10:37-38, Luka 14:26)
5. Kwamba ye ye ni Mwokozi wa ulimwengu (Luka 9:10)
6. Ya kwamba anasamehe dhambi (matayo 9:2)
7. Ya kuwa angekuwa hakimu wa mwisho wa kila mmoja (matayo 25:31-46)

Kwamba alikuwepo kabla ya Abraham na alifurahia utukufu pamoja na Mungu hata kabla ya ulimwengu kutiwa misingi (yohana 8:58;17:5)

Kristo anadai yakuwa alistahimili jaribio la kushindwa msalabani bado alijionyesha kuwa mfalme wa milele, akihaidi paradise kwa aliyetubu na kuombea maadui wake. Kwa uhalisi Kristo hakua wa kawaida, kwa kuwa kama alikuwa mwema basi Mungu alivyodai kwa maana mtu mwema hadanganyi kujiusu (Yohana 14:8)

Akielezea huduma duniani, yesu alisema, “Bwana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema;kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao; na vipofu kupata kuona tena na kuwaacha huru waliosetwa” (Luka 4:18) hiyo ndiyo iliyokuwa

kazi yake. Alienda kote akifanya mema na kuwaponya watu, hapakusalia hata mmoja aliyelia kwa uchungu wa maradhi. Upendo na huruma, vilidhiihikira katika kila tendo la maisha yake. Hata wachochole hawakusita kumkaribia hata watoto wadogo walivutwa naye walipenda kupakatwa na kucheza naye huku wakimtazama usoni. Yesu hakuwa mkaidi, hakunena lolote lisilo la maana wala hakumtia yeyote uchungu katika maneno yake. Hakuwahukumu walidhaifu. Alizungumza ukweli kwa njia ya upendo. Aliukemea unafiki, kutoamini na dhambi ila machozi yalilinga kwenye sauti yake. Maisha yake yalikuwa ya kujikana na kuwajali wengine wengi. Kila mtu alikuwa wa thamani machoni pake (Steps to Christ uk 11-12)

Yesu pekee ndiye mtu aliyewahi kuishi ambaye maisha yake yalilengwa na vivuli vya wahusika wengine kwenye Bibilia.

1. Anaitwa Adamu wa pili Warumi 5:14, ii Wakorinto 15:45) kwa sababu kama Adamu wa kwanza ambaye ubavu wake ultwaliwa ili kutoa uhai kwa mkewe, ndivyo ubavu wa yesu ultwaliwa msalabani ili bi harusi kanisa liwe na uzima wa milele.
2. Yakobo aliota kuhusu ngazi iliyotoka duniani hadi mbinguni (Mwanzo 28:12). Yesu alisema kwamba yeze ndiye ngazi imuunganishayo mwanadamu na Mungu (Yohana 1:51)
3. Kwa chuki, nduguze Yusufu walimuua utumwani, lakini Mungu akatumia usaliti huo kuiokoa familia yao, (Mwanzo 45:5) kwa njia yiyo hiyo yesu aliuzwa kwa maadui zake na kusalitiwa kwa chuki lakini Mungu alimtumia kwa hilo kuokoa ulimwengu. Kama Yusufu alivyokuwa Bwana juu ya nduguze ndivyo Yesu alivyo Bwana juu ya ulimwengu.
4. Musa alisema Masiha atakuwa kama mimi (Kumbu 18:18). Musa akiwakomboa wana waisraeli kutoka Israeli

- aliashiria Kristo akikomboa kanisa toka utumwa wa dhambi na kuzimu.
5. Neno la Kiebrania Yoshua laamanisha Yesu katika Kiyunani jinsi Yoshua alivyoshinda maadui wa Waisraeli na kuwapa milki ya Kanani ya duniani, ndivyo yesu alivyoshinda maadui na kutumilikisha Kanani ya mbinguni.
 6. Samsoni aliyeawa watu wengi katika kifo chake kuliko alivyowahi akiwa hai anamwakilisha Kristo aliyeafikia ushindi mkubwa katika kifo chake msalabani kuliko alivyowahi katika maisha yake.
 7. Daudi anamwakilisha Yesu, maana Kristo anaitwa Daudi katika Hosea 3:5. Ilitabiriwa kwamba Kristo ataketi kwenye kiti cha ufalme cha Daudi(Isa 9:7)
 8. Kama Suleimani alivyojenga hekalu la utukufu kwa amani (I waf 6:7) ndivyo Yesu alivyojenga hekalu la Kiroho-kanisa kwa amani na wala si kwa vita.
 9. Yona alivyokuwa tumboni mwa samaki kwa siku tatu iliashiria mda Kristo angekaa kaburini (mat 12:40)
 10. Jinsi kuhani mkuu alivyoingia patakatifu pa patakatifu, mara moja kwa mwaka akiwa na damu ya upatanisho, ndivyo Yesu alivyoingia mbele za Mungu na damu yake ili kusafisha dhambi za ulimwengu (Winreania 7-10)

Katika sura za kwanza za injili ya Yohana, Kristo alizungumzia vivuli na mifano kumhusu inayopatikana kwenye agano la kale. Hii ni pamoja na ngazi ya Yakobo, hekalu, nyoka ya shaba, maji kutoka mwambani, manna, wingu la moto n.k.

2: Ulimwengu Wa Yesu: Mahali, Watu Na Wakati

Palestina I Kusini Magharibi pembezoni mwa hilali yenye rutuba inayounganisha bonde la Uephrates-Tigiris na lile la Nile. Na daraja la ardhi liunganishalo bara la Uropa na Afrika na lile la Asia na Afrika.

Mipaka ya Israeli ilikuwa jangwa milima ya Yordani, bonde la Yordani iliyo Mashariki, Jangwa kuu na la ajabulikiwa kusini, bahari ya Mediteranean ilikuwa Magharibi na milima ya Lebanon ikiwa kaskazini.

Ukubwa wa nchi unakadiriwa kuwa kilomita 225 urefu. Takriban kilomita 40 upana kwenda kaskazini, na kilomita 130 upana kwenda Kusini.

Visima, chechemi za maji, mito bahari na mvua ilirubisha ardhi katika siku za Kristo. Iljawaa miti na ikawa maarufu kwa matunda, mtama, ngano, mizabibu na makomanga ni mionganii mwa yaliyopatikana kwa wingi bonde la Jordani ni mita 208.

Zaidi ya aina elfu tatu ya jimbi na miti iliyolala imehesabiwa kupatikana Palestina. Hii ni kutokana na utofauti wa hali ya anga na udongo. Mimea kutoka sehemu kame inaweza kustahimili huko. Huku asilimia kubwa ya mwaka sehemu za milima zilizo na mawe zinazalia tasa. Wakati wa kipupwe sehemu za mashambani zinastawi. Zamani, samba dubu na viboko walipatikana kwa wingi palestina. Leo hii 133 wanyama tofauti tofauti wanyonyeshao wanapatikana huko, aina 348 ya ndege, aina 90 ya wanyama watambazi aghalabu waishio majini na ardhini bila kusahau samaki waishio kwenye maji manana.

Yerusalem ilikaa katika nyika ilozungukwa na milima. Wengine wanauita mji wa milima saba. Ubora wake

unarejelewa kwenye maandiko na wanaosafiri huko wanaelezwa kama “wapandao kwenda Yerusalem”

Kwa hakika ni mmoja kati ya miji iliyoo juu ulimwenguni umeharibiwa na hujengwa mara kadha labda kuliko- mji wowote ule. Maana kifusi cha kuharibiwa kwake hawa msingi wa jingo jingine.mji ambao kwao Kristo alitembea, ni bora zaidi kuliko ulivyo sasa.

Nazareti, kijiji ambacho kwacho Yesu aliiishi kwa sehemu kubwa ya maisha yake ya utoto, ni mojawapo yamandhani bora duniani. Iko kwenye tambarare kaskazini mwa Magiddo ndani ya bunde lilofanana kikombe nusu baina ya bahari ya Galilaya na ufuo wa Meditteraneanan. Ingemchukua mtu takriban saa saba kutembea kutoka Nazareti kwenda Meditteraneanan na saa tano kufika Tiberia unapopatia baharini mwa Galilaya; na siku tatu kufika Yerusalemu.

Nyuma ya kijiji hiki pameinuka mlima wa urefu wa mita mia moja hamsini na mbili (152) kutoka kwenye muuniko huu nimeona mojawapo ya madhani bora zaidi duniani- milima ya Galilaya; huku mlima Hemoni ikipakana nayo katika upande wa kaskazini.

Kilele cha mlima wa Karmeli, Pwani ya Tiro, na mpwito wa maji ya Meditteraneani upande wa magharibi, ilhari mashariki eneo la msitu wa Tabora na tambarare maarafu la Esdraeloni kutoka upande wa kusini Bila shaka Yesu akiwa mototo mara kwa mara aliyatazama madhani haya kwa kumbukumbu ya unabii wa siku sijazo.

Watu Wa Palestina

Palipita miaka mia nne baina ya kitabu cha mwisho cha agano la kale na habari za kitabu cha kwanza kwenye agano jipya. Katika mda huu palitokea mabadiliko makubwa Palestina

lughya ya wayahudi ilibadilika na tamaduni mpya, mawazo, makundi ya kidini, na taasiri mpya zilianzishwa.

Aidha kulitokea mabadiliko ya kisiasa kutokana na kuchukuliwa mateka Babeli, makuhani walongoza nchi, japo warumi waliingia wakibadilisha yote na sasa Herode akiongoza Yerusalem akiwa kibaraka wa utawala wa Kirumi.

Palestina iligawanyika vipande vipande huku ikitawaliwa na wafalme wadogo wadogo.

Wazee wa dini walikuwepo kama taasisi ya utawala wa wayaudi ila mamlaka yao yaliodhibitiwa na Rumi. Hekalu ilikuwa kiini cha sherehe za kidini ila sinagogi zilidhaminiwa zaidi na zilitapakaa kote walikoishi wayaudi. Ukizingatia kwamba wayaudi walikuwa asilimia kumi ya watu wote lakini wenye mvuto mkubwa uliozidi idadi yao.

Makuhani walikuwa maelfu na walidai utiifu wa watu wa kawaida ambao hawakuwa na uwezo wa kusoma Kilbrenia isipokuwa Manabii.

Neno Rabii lina maana ya Bwana wangu. Viongozi wa dini waliotukuka walikuwa Mafarisayo ambao ni wazalendo wa tamaduni. Wengi wao waliamini kuwa mbingu ni yao jambo ambalo liliwafanya kuwadharau watu wa kawaida waliowafikiria kwamba hawafai kuokolewa.

Mafarisayo walidhamini sana imani ya mafundisho ambayo hayapo kwenye Bibilia. Wengi wa waandishi walikuwa mafarisayo ambao walifurahia kuwatwika watu mizigo ya kidini iliyokuwa mizito kubeba sheria zao kuhusu kutunza sabato zilikuwa ngumu. Lakini walitazamia kuja kwa masihi.

Kinyume na mafarisayo walikuwa Masadukayo waliopuuza tamaduni nydingi mradi waishi kwa raha mustarehe. Walitangamana na wasio wayaudi huku wakikumbatia utamaduni wa kiyunani na hawakuamini swala la ufufuo.

Wakwasi kuliko Mafarisayo na waandishi ,wasadukayo walimdharaau yeote ambaye hakuwa kiwango chao.

Hata hivo, badala ya kupata taifa lililoshikilia manabii wa zamani, Kristo alipata taifa lililoja tamaduni na upaguzi na huu ndio “mlima” alokusudia kuutupa baharini.

Wakati

Mtume Paulo alisema kwamba yesu alikuja ulimwenguni, ulipowadia utimilifu wa wakati (Wag 4:4) katika sura ya kwanza, Mariko anatwambia kwamba maneno ya utangulizi ya Yesu yalikuwa, “wakati umetimia”, (Mariko 1:15)

Ni dhahiri kwamba kabla ya kuzaliwa kwa Yesu, walimu kwa karne nyingi walikuwa wametabiri kuhusu kuja kwa Bwana Mkuu ambaye angeanzisha kizazi kipy. Wasomi wameweka kumbukumbu ya tabiri hizo kama zile zipatikanazo katika vitabu vya Rumi kabla ya ukristo, la muhimu mno liko kwenye maneno ya plato aliyetabiri hatima mbaya ambayo ingempata mtu wa unzuri usio wa kawaida.

Vigil alikwishaandika kuhusu kuja kwa mwana wa peke, lakini plato aliyeemuata kwa karne kadhaaa altabiri kufa kwa masihi msalabani. Akishazungumza kuhusu mtu mkweli na wa haki aliyeishi maisha ya kawaida plato alisema kwamba mtu huyo angeshtakiwa kuwa mtu mbaya zaidi ya wote, angedhiihakiwa kutezwa, kufungwa, macho yake kutobolewa, na hatimaye kuangikwa.kizazi ambacho kwacho Yesu Kristo alizaliwa kilikuwa kimekata tama.

Dunia yote ya wakati huo ilikuwa imepoteza maadili, imetamaushwa na kukosa matumaini na hapakuoneka namna ya kujisalimisha. Katika ufalme wa Kirumi wakati huo, kulikuwa na watumwa zaidi ya milioni sitin i(60,000,000), na hii ilikuwa idadi kubwa ya watu duniani wakati huo. Na panapo utumwa, maisha ya watu na haki zao hazidhaminiwi ipasavyo, kuijua

kulishamiri sana, ndoa na familia zilizambaratika, dini ilikuwa ni kama uchawi, philosophia haikuwa na maana. Hakika duniani ilikuwa tayari kwa kuja kwa masihi.

Amani baada ya vita, urahisi wa kusafiri, umoja wa lugha ulimwenguni (Koin Greek) Msongo wa kibinafsi uliosababisha watu kuanza kuzingatia umilele wao, kutapakaa kwa wayaudi na vitabu vitakatifu, yote haya yalienda nji kwa kuja kwa Yesu na habari zake njema.

Unabii wa kimasih wa Danieli 9:24-27 ulikuwa chimbuko la faraja kwa wale waliotazamia kuja kwa Masihi. Ilifunua ya kuwa karibu ndani ya miaka mia tano baada ya wayahudi kurejea kutoka utumwani, mkombozi mtarajijiwa wa mda mrefu atatokea.

3: Ubatizo Wa Yesu Mpaka Juma Lake La Mwisho

Kuzaliwa Kwake Na Ubatizo Wake.

Kwa waliojiweza alikuwa mmoja ambaye kwake ulimwengu ulikosa chumba chake. Alikuwa uchi bila msaada alipendwa sana lakini vilevile akachukiwa zaidi. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa pale kalvari.

Ijapokuwa mbingu ilijidhihimisha kupertia katika ile nyota elekezi mfalme Herode alipanga kumuua. Msalabani mbingu tena ilionyesha upekee wa Yesu kupertia lile giza nene kwa masaa matatu, hata hivyo wasulubishaji hawakutupu. Kule Bethlehemu, majuzi walimletea Yesu manemanne, na ubani ile ile ilitumika kusitiri mwili wa yesu baada ya kifo chake.basi ndivyo ilivyokuwa, ya kwamba siku za kwanza za Kristo zilitoa taswira has ya kifo chake.

Basi ndivyo ilivyokuwa, ya kwamba siku za kwanza za Kristo zilitoa taswira hasa ya kifo chake.

Ubatizo

Pale ubatizoni, Yesu alitua zana zake za useremala na kuchukua kazi ya huduma ya kiroho ambayo ingemchukua karibu miaka mitatu. Roho alimwongoza Yesu jangwani ili ajaribiwe na mwovu (Mk 1:12-13). Baada ya majuma sita ya kufunga, shetani alimujia na majaribu matatu makuu, shetani hakumjaribu Yesu ati atumie asili yake ya chini (km kuzini), maana hakuwa wa chini. Ibilisi alimjaribu atumie asili yake ya juu (kubadilisha mawe yawe mikate) ili kukidhi hitaji la njaa, lakini aliyejfanya sawa nasi alikataa kutumia mamlaka yoyote aliyokuwa nayo kwa ajili manufaa yake.

Kulingana na Yohana mwaka wa kwanza wa huduma ya yesu ulimalizia Yudea. Huko ndiko alikowaita wanafunzi wake wa kwanza, ndiko alikotakaza hekalu, na ndiko alikofanya mkutano wa usiku wa faragha pamoja na Nikodemu.

Kitabu Cha Yohana

Kitabu cha kiroho zaidi kilichowahi kwandikwa ni injili ya Yohana huku vitabu vya kwanza vitatu vya injili (Matayo, Mariko, na Luka) viliandikwa kwa ajili ya wayaudi, Warumi na Wayunani mtawalia. Injili ya Yohana iliandikwa kwa ajili ya kanisa.

Yohana alilitumia hekalu la wayunani pamoja na matabau yake ya kafara, bakuli la kutawadhia, meza ya mkate, kisimamia dhahabu cha taa pamoja na taa zake saba, matabau ya dhahabu ya kuchomea ubani, ubao mtakatifu ubebao sheria kumi na kifunko kitakatifu cha agano cha dhahabu katika ule ubao mtakatifu kama ramani ya mchecheto wa injili yake.

Basi Yohana anaeleza kwa lile bakuli na maneno, hakuna atakayeingia ndani ya ufalme wa Mungu pasipo kuzaliwa kwa maji na katika Roho (Yohana 3:5). Akieleza kwenye meza ya mkate, Yohana anamwashiria Yesu akisema, “mimi ni mkate wa uzima” (Yohana 6:35).

Kama vile ubani ichomwavyo katika matabau ya dhahabu ilipanda juu ya kitambaa mpaka kwenye awepo Mungu, ndivyo maombi ambayo tunayofanya katika jina la Yesu yanapanda mpaka kwa Mungu (Tazama Ufu 8:3-4) yesu alisema “Nitafanya kila mwombalo katika jina langu....mkiomba chochote katika jina langu, nitafanya” (Yohana 14:13-14)

Sura ya 18 na 19 za injili ya Yohana zinamwonyesha yesu mfano mwingine wa injili ya Yohana ni msisitizo uliokitwa kwenye miujiza saba ya kabla ya msalaba. Hii huangazia nguvu zibadilishazo za yesu katika maisha yetu.

Katika miujiza hii, tunakumbana na mabadiliko kutoka kwenye huzuni kwenda kwa furaha, kutoka kwa magonjwa kwenda kwa afya, kutoka kwa kupooza kwenda uimankaji kwa nguvu nyingi, kutoka kwa njaa kwenda kwa utele, kutoka mawazo kwenda kwa utulivu, kutoka kwa giza kwenda kwa mwanga, na kutoka kwa kifo kwenda kwa uzima.

Katika miujizi hii tunapewa picha ya mabadiliko yaliyotendeka ndani ya maisha ya kila mtu ajaye kwa Yesu.

Hii miujiza saba zafunua nguvu za Yesu juu ya kila hali na mazingira. Yeye ndiye Mungu wa ubora (alibadilisha maji yakawa divai, yeye ndiye Mungu wa utele (aliwalisha wanaume elfu tano, ukijumulisha wanawake na watoto, akitumia samaki wawili na vipande vyta mikate vitano), Yeye ndiye Mungu wa Wakati, (alimponya mtu aliyeugua takriban miaka thelathini na nane). Yeye ni Mungu mahali (akiwa Cana, alimponya kijana wa Kapernaumu), Yeye ni Mungu wa Uumbaji (alituliza mawimbi ya Galilaya), Yeye ni Mungu juu hali(alimponya mtu aliyezaliwa kipofu), na tena Yeye ni Mungu wa kifo na maisha (alimfufua Lazaro kutoka kwa wafu). Hii miujiza inadhihirisha kuwa vitu vyote viko chini ya utawala wa Yesu.

Hoja kuu kwa ajili ya kila mmoja wetu ni kwamba neno libadishalo la Kristo ni imara na sahii kama vile ulivyo uwepo wake halisi. Bila hata kugusa yale maji yalokuwa, ndani ya vibuyu kwenye ile harusi ya Cana, Yesu, kwa neno tu aliyageuza maji yakawa divai. Baadaye, alizungumza neno kule Cana na kumponya kijana wa Kapernaumu. Na neno lilo hilo lilimwita mfu kutoka kaburini.

Hilo neno bado lipo ili kufanya muujiza wa wokovu katika maisha kwa muumini hata Yule mnyonge zaidi maadam anamwita Kristo kwa imani.

James Staiker anangazia kwamba miujiza ya Yesu katika injili ya Yohana inaitwa ishara. Alipouponya upofu wa kimwili,

ilikuwa ishara kwamba ana uwezo wa kuponya hata ile halimanya zaidi- upofu wa kiroho. Alipowafufua waliokufa kimwili ilikuwa. Ishara kuwa ana uwezo wa kuwafufua waliokufa kiroho. Alipotakaza yule mkoma ilikuwa ishara kuwa ana uwezo wa kuondoa ukoma wa dhambi. Alipolisha umati kwa vipande vya mkate, ilikuwa ishara ya kwamba Yeye ni – mkate wa uzima ambaye angevunja kwa ajili ya dhambi za ulimwengu angetulisha na mkate wa uzima. Alipoituliza bahari ilikuwa ishara ya kuwa ana uwezo wa kuleta amani juu ya madhara ya kuchanganyikiwa.

Watu wengi wanakebe miujiza iliyofanywa miaka elfu mbili iliyopita. C.S Lewis ameandika kwa ufasi kuhusu mada hii. Anasema kwamba hakuna kitu katika injili zote kijitokezacho kama hekaya za miujiza, ambapo vitu vya ajabu ajabu vilifanyika kama vile wanyama kugeuka kuwa wanadamu, au miti kuzungumza, meli kugeuka kuwa miungu ya kike n.k. miujiza ya maandiko ya Bibilia ndiyo ingetegemewa kutokea ikuwa Mungu mwenyewe aliitembelea dunia. Kila mmojawao unabeba sahihi ya Mungu mwenye upendo na wa kufikirika.

Miujiza ndiyo iliyounda na kujenga historia ya Yesu kiasi kwamba miujiza ingeondolewa, na historia basi ingeangamizwa kuna uhusiano wa chanzo na nguso baina ya miujizi ya ajabu ya yesu na ule mguso miujiza ilileta juu ya watu walioishuhudia.

Mujiza wa ufufuo wake mwenye kutoka kwa wafu uliwabdalisha ndugu zake, na kuhuisha na kuwatia nguvu wanafunzi wake kupeleka habari njema kwenye nchi za mbali za ulimwengu usiojulikana.

I Wakorinto 15:46 inatupatia kanuni inayotoa mwanga juu ya sura ya tatu ya injili ya Yohana. Cha kiroho hakikuja kwanza, bali cha kimwili na baadaye cha kiroho. Hali yetu ya kimwili ya

kwanza haikuwa ya kiroho, na ikiwa tutapata uzima wa milele katika miyojo yetu.

Kama hata Nikodem, mwalimu mkuu wa dini katika Israeli, mtu aliyekuwa na tabia isiyodosarika na mwenye wema wa nje, aliiitaji kuzaliwa tena kiroho, sembuse sisi?

Katika sura ya tatu ya injili ya Yohana, yesu yuzungumza na Myahudi, ila katika sura ya nne, azungumza na mtu wa mataifa. Katika sura ya tatu, mtu anayemzungunzia ni wa mvuto mkuu, katika sura ya tatu ya Yohana, Nikodem anambiwa kwamba lazima azaliwe tena ila mwanamke anapewa tu zawadi ya kuchukuliwa. Kuna sababu nzuri sana kuhusu hili. Nikodemo alishikilia haki ya ubinafsi wakati mwanamke yeeye alikuwa na hitaji la kutoka ndani. Nikodemo ndiye alimtafuta yesu, lakini mwanamke alitafutwa na Kirisito.

Kiongozo wa kiyahudi alikuja kwa yesu usiku, lakini mawasiliano ya yesu na Yule mwanamke yalifanyika mjana mweupe.

Yohana sura ya nne imetokea kuitwa mwongozo wa kuongea roho maana inatoa hatua za kutoka kwenye kutokwamini mpaka kufikia kwamini.

Soma hiyo sura na upate mafungu yanoyofunua vile ambavyo yesu alifikia Yule mwanamke msamaria kumsikiza, haja yake, hitaji lake, kuguswa kwake na tendo lake.

Katika sura hiyo hiyo kuna kisa cha uponyaji wa kimiujiza wa mototo wa mtu tajiri. Baada ya kutembea na Yesu, baba mototo yu na uhakika ya kwamba Yesu ameponya mototo wake ndipoza hakujali kuharakisha nyumbani. Hiki kisa kinatufundisha namuna ya kushughulikia matatizo yetu yote. Kwanza usikatae hitaji, kubaliana lipo. Pili, peleka shida kwa Yesu, tatu kubali ahadi yake ya kwamba ameweka suluhisho la hitaji lako na anazo njia elfu za kutatua matatizo yako ambayo kwayo hujui chochote. Nne nenda zako ukitegemea ya

kuwa kwa wakati Yesu na kwa mbinu yake, yote yatakuwa barabara. Mara nyingi hii hatua ya nne ndio inakuwa ngumu zaidi.

Wale amao wanasona sura za kwanza nne na injili ya Yohana watakumbana kile ambacho kijulikanacho sana hasa kuhusu mwaka wa kwanza wa huduma ya KRISTO – Mwaka.

Tunachokielewa ni kwamba karibu na mwisho wa mwaka wa kwanza wa huduma ya yesu, Yudea na Yerusalem ziligungubikwa na wingu ina makosa ya kustaayabisha yaliyowahi kufanywa; wayahudi kumkataa na kumsulubisha Mungu wao aliyejukwa kwa njia mwili.

Mwaka Wa Umaarufu

Katika mwaka wake huko kusini, Yesu aliondoka kwenda Galilaya katika kaskazini mwa nchi. Katika eneo hili ambalo kidogo haikuwa ngumu, madharau yangekuwa kidogo kinyume na kule ambapo utawala wa kidini uliweka makao yao makuu.

Katika huu mwaka wote, Yusu anafundisha wanafunzi wake. Pamoja na kwamba kazi yake ilifanyika wakati wote, na kwa ulimwengu wote, ulimwengu wote, isingema lizwa na yeye mwenyewe. Ndio maana akawaita kumi na wawili ili waweze kuindeleza kazi yake hata baada ya yeye kurejea mbinguni.

Mwanzo pamoja na mwisho wa mwaka huu Kristo alitembelea mji wa nyumbani alikokataliwa na kutishiwa mauti. Alichokisema ni kwamba nabii haheshimiki kwao.

Lakini sehemu kubwa ya mwaka iliyosalia, nje ya Nazareth kilitokea fuhara, uponyaji, mafundisho, na sifa kutoka kwa maelfu hata kumi ya maelfu makutanoni kwingine. Wale ambao kama krisito wanoishi sawa na mapenzi ya mungu watakuwa mpaka itakapomalizika kazi yao.

Wito wa wanafunzi wa kwanza katika taalamu yao ya uvuvi yaweza kufananishwa na kisa kinachoitimisha injili ya yohana.

Utathimini wa katika Luka 5, unaashinia kazi ya kanisa lionekanalo likiwa katika udhaifu, na hatari zake:Hata baada ya mbaraka wa kristo, samaki wengine watoroka kupitia kwenye neti zinazokatika. Sivyio ilivyo katika kisa cha pili ambacho kinaturelekeza kwenye kanisa la kweli lisiloonekana na wokovu timilifu, na usalama wa wote wakusanywao kwenye neti ya injili.

Mara nydingi, wavuvi wa injili wa Kristo wanang'ang'ana katika masaa ya usiku na hawapati chochote. Ni kwa agizo la Kristo ambalo kwalo hali zote mbili mambo yanabadilika. Yeye ndiye yote tunayohitaji. Lile tukio ambalo lililoanzisha huduma ya wanafunzi linasema kwamba neti ilitupwa kilindini, lakini mwishoni hajulikani, lakini takribani samaki 153 wanashikwa baada ya ufufuo wa Kristo. Hesabu hii inajengwa kutokana na uzidisho wa 12 ukijumulisha uzidisho wa utatu mtakatifu. Wanafunzi wa Yesu wakifanya kazi wakishirikiana na utatu mtakatifu wanavuna kwa ajili ya ufalme huku 12 ikiwa hesabu ya kibibilia ya ufalme.

Yule mtu aliyeooza wa kaperanauma (mat9) , na yule kiwete wa Bethsaidia (Yohana 5). Wanatukumbusha kwamba pasipo Kristo hatutaweza kutembea itupasavyo. Katika matukio yote mawili waandishi wa injili wadokeza kwamba hawa watu walikuwa na shida waliojiletea wenyewe, japo hili halimtoi inji yule tabibu mkuu. Zingatia kuwa katika Luka 5:20, Kristo kwanza anaonyesha msamaha wake kwa ajili ya dhambi. Ni hakimu mkuu wa ulimwengu peke yake anayeweza kusamehe dhambi, na hakimu huyo anao huruma hata kwa wanguao wabaya zaidi.

Baada ya Kristo kuteua wanafunzi kwa ajili ya huduma, anahubiri hubiri kuhusu uteuzi itubiri la milimani. Hili ndili hubiri lefu zaidi lililonakiliwa. Ni muhimu kuzingatia hapa kuwa, mwanzoni katika huduma yake, kileleni mwa hubiri lenyewe, anaagiza watu kutubu dhambi (Mat 4:17), na kasha kufundisha

maana ya kutubu na faida inayopatikana kutokana na kufanya hivyo. Mahubiri ya Yesu yanaangazia kiunaga naga maisha ya Mkristo yapasavyo kuwa, kumwelekeza msikilizaji kupaza sauti “ole wangu maskini mimi ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?” (War 7:24). Si kwamba ni sadfa kuwa mahubiri haya yanafuatwa na uponyaji wa mkoma, kwa kuwa hakuna mtu mwenye moyo mwema takayesoma mahubiri haya pasi na kuijisi mkoma na kuhitaji uponyaji.

Huku Matayo 5-8 ikiangazia maneno makuu ya mwokozi, sura zifuatazo zinatwambia kuhusu matendo yake! Huenda katikati ya huu mwaka, Bwana anadhihirisha mamlaka yake juu ya uumbaji pamoja na mapepo.

Ni muhimu kuzingatia alivyotuliza mawimbi ndani ya mioyo ya mitume kabla ya kuteliza mawimbi ya baharini na mawimbi ndani ya moyo ya mtu aliyepagawa. Miujiza inayohusishwa na mvuko wa mto Galilaya (Mat 8) ni ya kihistoria, lakini pia ni mifano ya matukio ya kiroho.

Katika kila maisha, mawimbi na dhoruba huingilia zikitisha kutuangamiza. Misingi ya ufahamu wetu ni

1. Maisha ni mchafuko
2. Sisi ni wadhaifu
3. Matendo yana gharama.

Hivyo basi shida za mara kwa mara hutarajiwa. Na mara nyingi tunapigana na dhoruba kana kwamba tu peke yetu, huku tukisahau kwamba tunaye mmoja awezaye kutusaidi. Ikiwa tutamwita atajibu kwa namna ya ajabu. Chunguza mamlaka ya neno la Kristo kwa hilo aliumba mbingu na nchi, akakemea mapepo, akatuliza bahari na kufufua wafu. Neno lake daima lilikuwa na nguvu, na iwapo totalishikilia, kuliamini, kulitii, nguvu zile zile zitafanya kazi kwetu na kutuliza kila mawimbi.

Kwa kawaida wimbi la ndani la hofu, shaka, na upweke ni mbaya zaidi ya wimbi la nje. Lakini hapa tena neno la Kristo ndilo jibu “maana Mungu hakutupa roho ya wogo bali ya nguvu na ya upendo, na ya moyo wa kiasi (Timot 1:7). Imani huja kwa kusikia ujumbe na kusikia huwa kwa neno la Kristo” (War 10:17) chochote kipatacho mawazo yetu hutupata. Ni kitu gani tunachopatia mawazo yetu- ni hofu yetu, au upendo wake, neema na nguvu? Tazama waifilipi 4:6-8. soma aya hiyo ukirudia, Ikariri, ishi kwayo, usihofu chochote. Omba kuhusu yote, na ushukuru kwa chochote. Basi inaweze kana kufurahi katika Bwana licha ya masumbu ya ulimwengu (wafilipi 4:4).

Ni katika huu mwaka Yesu aliwapeleka wanafunzi wake kwenye safari za kuhubiri huenda kuna miujiza mingi ilofanyika zaidi ya iliyorekodiwa kule Yerusalem, Yudea, mtu aliekuwa kipofu tangu utotonii alijifunza upesi na kwa furaha Yesu ni nani. Mwanzoni anamtaja Yesu kama mtu. Baadaye anamwitaa nabii. Na mishowe anamkiri yesu kuwa Bwana na anamwabudu (Yohana 9)

Katika wakati wa pasaka, Yesu alikuwa Yerusalem, na huko alimponya mtu alieugua kwa miaka 38. tazama Yohana 5. huyu mtu kielelezo cha Israeli ya zamani, ambayo kwa kutoamini waliangaika janguani kwa miaka 38 bila nguvu na heshima. Mtu huyu aliponywa siku ya sabato jambo lilitozua mtafaruku kwa Yesu.

Inashangaza ni mara ngapi tusoma kuhusu vita dhidi ya sabato katika mwaka huu wa umaarufu Kristo hakukubali tamaduni ambazo zilifanya sabato kuwa muhimu kuliko binadamu. Na hilo liliwatia furaha watu wa kawaida ila liliwafanya viongozi wauaji. Alifunza kuwa sabato ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu bali si mwanadamu kwa ajili ya sabato. Na alileta pumziko la sabato kwa wale aliowaponya.

Alijidai kuwa Bwana wa sabato na akaipa siku umurwa usioisha. Akitupitia siku hamsini na mbili anana na bustani hamsini na mbili za kufana na kupendeza.

Bwana alihisha taasisi za ndoa na sabato na kurejesha wasikilizaji wake kule Edeni akiwa anazungumzia zote mbili. Alielewa kwamba itikadi za dini ya wayahudi zingefika mwisho, ila alitambua kwamba kanuni na taasisi zote kutoka Edeni zingedumu milele. Alihatanisha huduma yake na maishaa yake alipofanya miujiza katika siku takatifu (miujiza saba imeokodiwa) lli kuonyesha kuwa utunzaji wa kweli wa sabato uliletä mibaraka wala si jerahu. Hakuwai tetea taasisi yoyote ambayo ingepita. Amekimia kwenye swala kuhusu jinsi ya kutunza itikadi tamaduni za dini ya wayahudi. Na anamwambia yule mwanamke kule sychar kuwa hizi njia za ibada ya wayahudi zingepoteza maana (Yohana 4:21)

Kanuni zilizotolewa katika amri kumi zingesalia milele (Matayo 24: 20, Luka 28:56)

Mwaka Wa Upinzani

Sasa kasi inaongezeka na upinzani umechacha huku viongozi wakizidi kutamaushwa kwa umaarufu wa Kristo mwanzoni ilionekana kwamba Galilaya yote ingemgeukia Kristo, ila mawazo ya waGalilaya yalikuwa magumu kama jiwe, umarufu wa kwanza ulikufa polepole na badala yake kukajashauku na upinzani. Kristo alikuwa mtoro akisafiri mbali na mahali pageni. Pamoja naye sasa ule umati mkubwa wenye jazba ulipungua mno na wanafunzi wake wakawa wachache tu. Lakini ishara zake za miujiza ziliongezeka kama vile, kuwalisha watu Elfu tano. Ilikuwa mfano wa usambasaji wa injili- kristo alipokea chakula kutoka kwa Mungu kisha akawapa mitume ambao waliwapa umati wa watu walioshiriki wa kwa wao.

Tazama vile yesu aliwajaribu wanafunzi kwa wakati huo. Alimpa changamoto filipo kuwalisha maelfu ya watu bila chakula, na Filipo alikiri kuwa hakuwa na namna ya kuwasaidia Andrea aliangalia uwepo wa mikate michache na samaki naye akakosa tumaini kama Filipo- lakini kijana mdogo aliyebeba chakula chake, alimwangalia yesu na hilo likasuluhisha kila yesu kitu. Ni muhimu kiasi gani kwamba yesu akiwa na upungufu wa rasilimali (mikate tano na samaki wawili), aliwalisha zaidi na kasaza chakula zaidi (vikapu kumi na viwili). Kwa wale 4000, alikuwa na mikate saba na samaki wacheche, lakini alilisha wachache na kukachazwa vikapu saba. Angelifanya katika I Wakorinto 1:26-31.

Mungu huchagua wadhaifu, waliopuuzwa na wapumbuvu kufanya yasiyowezekana. Kuna tumaini kwetu zote.

Utengano

Akiwacha umati ili ajiandae kwa MSALABA, Yesu hazingwi tena na umati. Ila mjumbe alitangulia miezi miwili kabla ya kusulubishwa na akasema: Bwana, yule umpedaye yu mgonjwa” (Yohana 11:3). Waumini huugua na wanajua maumivu. Ndivyo ilivyokuwa kwa Ayubu, Hezekia, na mwivi msalaba na wakati kamaa huo, muhimu zaidi kuliko upendo wetu kwa Yesu, ni upendo wa Yesu kwetu.

Cha kushangaza zaidi, Kristo aliubiri siku mbili zaidi kabla ya kwenda kumhudumia yule rafikiye mgonjwa. Faraja ambayo amewapa mamilioni ya wahumini wanaoteseka tangu wakati huo. Ni bora zaidi kufufuliwa kutoka kaburini kuliko kitandani hilo ndilo Lazaro na dadaze walikuja kuamini. Walitiwa nguvu kukabiliana na shida za baadaye kwa sababu Yesu alikawia kuwasaidia kwa tukio hili.

Juma La Mwisho

Sasa twaligeukia juma la muhimu la kihistoria. Linalo kamilika kwa kufu na kufufuka kwa Yesu. Ujumbe mahususi wa juma hili ni kwamba Mungu atesekaye yu kwenye kiini cha Ukristo. Wakristo tu huabudu Mungu aliyejeuhija kwa ajili yetu.

Hakika juma hili linaanza Jumamosi usiku wakati kulikuwa na karamu katika nyumba ya Simion kusherehekeua ufufuo wa Lazaro. Siku ya wayahudi ilikuwa inaanza jioni na kwa muktadha hii ilikuwa jioni ya Kiyaudi maana baada ya sura hii, Yohana hanakili huduma nyingine yoyote kwa wayahudi wasioamini, isipokuwa maneno ya hukumu. Maneno yake yote ya kutia shime ni kwao walomfuata iwe anajaribu maswali, anatoa hadithi au kuvuta mawazo kwa matendo ya miigizo, maudhui yake ni sawa. Siku ya kiama yaja. Kuna karamu mbili katika juma hili la mwisho; aliyetubu, Mariamu anampaka mafuta Bwana wake mbele ya kakaye Lazaro na mbele ya wanafunzi wake pili sherehe ya pasaka usiku wa kusalitiwa kwa Yesu.

Ni usahi wa ajabu kiasi gani uliopa kwenye tukio la ufunguzi la juma hili la mwisho! Mdhambi kwa gharama kuu anavunja chomba cha marashi ya thamani na kumpaka mwokozi wake. Kile chombo kilichovunjwa kiliashiria mwili wa Yesu ambaa ungevunjwa msalabani – zawadi ya utele wa Mungu kwa binadamu kama vili ile zawadi ya marashi ya Mariamu ilitabakaa nyumbani kote (si chumbani tu) ndivyo marashi ya upendo wa Mungu ultoka kule msalabani na kujaza ulimwengu wote.

Sura hii ikijawa na heshima alizofanyiwa Kristo, inaanisha ufunguzi wa sura iliyo tangulia ambapo viongozi wa kiyahudi waliitisha kikao na kumhukumu Kristo kama msaliti ambaye apaswa kufa. Lakini, Yohana 12 inamwanyesha kama aliye heshimiwa kuititia zawadi akiwa anaingia Yerusalem kwa

usafiri wa punda, kupitia wayunani wanootaka kukutana naye, kupitia sauti ya Mungu kutoka mbinguni, na kupitia mawazo mazuri ya viongozi Fulani mashahuri.

Kile kitendo kisicho cha ubinafsi cha Mariumu kinatukumbusha kwamba kumtumikia Yesu kutoka moyo kunaweza kusababisha kukemewa na kutoka kwa watu wengine wa dini ambao wanafikiria kuwa tungefanya vinginevyo. Na katika tukio hili Mariumu alisikia Yuda akisema "mbona marashi haya yasingeuzwa na pesa zigagwiwe maskni? Sio kwamba Yuda aliwajali maskini, maana alikuwa mwizi. Lakini yesu pamoja na kwamba alimpenda Yuda, alimtetea Mariamu akisema kwamba alichohi mfanyia Mariamu kilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu hawakuuelewa bado" (Yohana 12:7)

4: Yesu Aingia Kwa Kishindo

Siku nyingine umati mkuu uliokuja kwenye sherehe, walisikia kwamba Yesu yu njiani kwelekea Yerusalem. Wakachukua matawi ya mitende na wakaenda kumlaki huku wakipiga mayowe, Hosana! Heri ajaye kwa jina la Bwana. (Yohana 12:12-15)

Alichofanya Yesu katika tukio hili ni tofauti na namna ya kawaida ya utenda kazi wake. Ni dhahiri kwamba nia yake ilikuwa ni kuvuta umati kwenye madai aliyoafanya kwa maana saa ya kuondoka kwake ilikuwa karibu. Lakini kinyume na matarajio ya watu, haji kwa farasi wa vita kuwavumisha wakaaji wa kirumi katika Israeli, ila kama mfalme wa amani aliyepanda mwanapunda.

Siku ilifika kileleni alipotakasa hekalu isiyokuwa ya wenye dhambi wa mataifa bali ya wenye dhambi wayaudi- na gadhabu ya kuhani mkuu na watawala ilitokota. Matayo anaripoti, walikasirika (Matayo 21:15).

Miaka elfu moja kabla, wakati ambapo mfalme Daudi alielekeea Yerusalem kwa mayowe na nyimbo, Bibi harusi ambaye alikuwa tayari kumwachia ufalme wake alichungulia kutoka kwenye dirisha na kumwona Bwana harusi wake akiwa nusu uchi akitakuza na kucheza mbele ya Bwana. Alitoka nje na kumkejeli, hakika leo ulikuwa mkuu!" ulifanya kama mzee mpumbavuachezaye nusu uchi mbele ya wasichana wa vitwana wake.

Lakini mfalme alijibu ni mbele ya Bwana aliyenifanya mtawala juu ya watu wake nilicheza, na kama nilifanya hivyo kwa namna ya kuudhi, bado hao vijakazi unaowasema wataniheshimu tu.

Ndipo kukafuata laana – mikali hakuzaa wana (Il Samwelii 6:20-23)

Kwanini tunanukuu historia hii ya zama? Kwa sababu pindi tu baada ya viongozi wayahudi kwa kumkomea Yesu kwa vitendo vyake alilahani ule mti tasa- ishara ya Israeli- na kutangaza, "Usizae matunda tena (Matayo 21:15-19) Na kwa miaka elfu mbili bi harusi wa Kristo aliyependekezwa, Israeli imekuwa tasa kiroho.yote haya yalitabiliwa katika siku ya Daudi na mikaeli.

Ni huzuni ulioje, kwa maonyo ya rekodi za zamani. Ni kanuni nzuri nay a busara kuwa na kiasi katika vitu vyotisipokuwa kumpa Mungu wetu mahali pake. Mtu hapaswi kuwa na kiasi atorokapo nyumba inayoteketea au kufunga mkanda iwapo meli yazama. Maisha yetu kibinafsi yananninginia kwa uzi wa neema na tunawenza kuukata uzi huo kwa kujizamisha kwenye mambo ya ulimwengu kuliko kwa muumbaji na mkombozi. Mungu alizuia kwamba vitu vitupavyo amani vifichwe mbali na macho yetu.

Luka anarekodi, 'Machozi aliyolia Yesu alipoona mji mtakatifu- mji uliyolia Yesu allpoona mji mtakatifu- mji uliopanga kumuua haraka iwezekanavyo. Alipokaribia Yerusalemu aliulilia akisema, hata wewe ungelija kitakachokuletea amani- ila sasa kimefichwa mbali na macho yako, kwa kuwa siku zitakuja adui zako watakapokujengea boma likuzunguke. Litakuzingira na kukuhusulu pande zote, watakwangusha chini wewe na watoto wako wasikwachie jiwe juu ya jiwe kwa sababu hukutambua majina ya kujiliwa kwako' (Luka 19:1-44)

Miaka arobaini baada ya Yesu kutabiri haya, majeshi ya Kirumi waliharibu jiji la Yerusalemu na hekalu yake. Mamia ya maefu ya wayaudi waliangamia katika utekaji nyara huo na wengine waliuzwa utumwani.

Injili iliubiriwa kwa wayahudi kwanza, na hivyo ndio wa kwanza kuhukumiwa na Mungu. Na hivyo, ni onyo kwa mataifa

ambapo injili imehubiriwa, kwa maana Mungu atawahukumu nao pia. Yesu basi alionyesha kiini cha Mungu na umuhimu wa injili yake, ambayo ni upendo kwa waliopotea.

Tunaweza kumtumaini mwokozi aombolezaye. Majozи yake yanafaa kuondoa hofu yetu. Baada ya haya, mwili wake uliovunjwa ubebao uzito wa dhambi zetu uliangikwa msalabani. Huyu ndiye Mungu aombolezaye tu, ajulikanaye kwa wanadamu. Mungu aliyejeruhiwa Mungu pekee aliyejitoa kafara kwa watu wake.

Alipoingia jjini, Kristo allingia hadi kwenye kitovu chake-hekalu. Alitoa hukumu alipoanza na alipokamilisha huduma yake. "Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiiza na kununua hekaluni, akazipindua meza za wabadili fedha na viti vyao waliokuwa wakiiza njiwa. Akawambia imeandikwa, 'nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala bali ninyi mmeifanya pango la wanyanganyi (Matayo 21:12-13).

Dini nzuri ndicho kitu bora ulimwenguni kama ilivyo kweli dini mbaya ndicho kitu kibaya dunuani. Kwa bahati mbaya, dini mbaya ndiyo iko kwa wingi. Na kitendo cha Yesu cha kutakaza hekalu kinaashiria hitaji la kila mara la kuuhisha kanisa.

Mtu hawezi kuwa mkristo wa kweli kwa kuhuduria kanisani kuliko ambavyo mtu anaweza kuwa gari kwa kulala katika Garage Mkristo wa kweli ni mtu aliye na Mungu katika maisha yake. Pindi kitu chochote ambacho si Yesu, kinapopewa kipaumbele katika maisha ya mtu au kanisa, dini inageuka kuwa mbaya na lazima kuwepo na uuhisho. Vita vyta zamani baina ya Kristo na kayafa huwa vinajirundia milele.

Fikiria tukio la nyuma ambapo kayafa mrefu na kiongozi mzee angesema ni bora mtu mmoja kufa kwa ajili yaw engine kuliko taifa lote kungamie. Huu ndio uliokuwa uyahudi ambao kwa mamia ya miaka ya historia ya utakatifu, iliyonuliwa kiungu

ili kuandaal ulimwengu kwa kuja kwa masihii lakini tayari kumsulubisha Mungu waliyemwabudu.

Kila mwanaume na mwamke mkweli wa wakati huo angechagua baina ya Kristo na kayafa- baina ya muungano na itifaki zake zote, na historian a tamaduni zake au Yule mnyenyekevu aliyekuwa njia kweli na uzima.

Kila kanisa lazima lipime kila tamaduni, kila tendo kwa maneno ya mwana wa Mungu. Jaribio daima ni Yesu, utu wake na ukweli wake.

Waweza kuwa umetambua kwamba katika kuingia kwa Yesu Yerusalem, maneno ya huduma yake yamebadilika. Vitendo vyake na maneno yake ni juu ya hukumu. Baada ya kutakaza hekalu methali na maonyo yake juu ya Israaeli yanakuwa makali nay a dharura.

5: Yesu Afundisha Injili Kwa Mataifa (Wayunani)

Viongozi wa kiyahudi – wakitamani anaswe na watu wakiyahudi na ili wamtie yesu kwenye shida na Rumi walimuunjia na swali watoe ushuru kwa Rumi ayu la?

Yesu akawambia, nionyesheni dinari ina sura na anwani ya nani? Aliuliza.

Ya kaisari,wakajibu (Luka 20:20-26)

Akawaambia,mpeni kaisari viliyvo vya kaisari,na mungu viliyvo vya mungu.

Hatupaswi kamwe kuvitenganisha alicho kiunganisha kristo. Hatutakikani kuvikanyagia chini vitu vya Mungu ili kupendeza serikali, wala hatusitahili kukosa kutimiza wajibu wetu kwa serikali kwa sababu sisi ni wakrisito.

Baada yasiku ya siku ya kubishana na viongozi wa kiyahudi, Krisito aliwageukia na kuwaliza, “Je mnafikilia nini kuhusu masihi? Yeye ni mwana wa nani?” (Matayo 22:42)hili ni swali moja ambalo likijibowi vizuri litayajibu maswali mengine yote. Walijibu mwana wa Daudi. Ndipo Kristo akauliza swali la pili kama Daudi anamwita masiha bwana, je ikawezekanaje awe mwanake?.

Kabla ya kuwepo mwana wa mungu, mwana wa Daudi alikuweko na ndiye Bwana wake mlezi. Tangu siku hiyo kuendelea hapakuwepo na mtu aliyethubutu kumuliza maswali zaidi. Ilikuwa ni jambo la bure kuendelea kubishana na mtu ambaye daima alishinda hoja. Siku moja swali la kristo la kwaza litageuzwa kwako “Je kristo ananifikiliaje?”

Injili Kwa Mataifa (Wayunani)

Mwanzoni mwa maisha yake ulimwenguni, maajuzi kutoka mashariki walikuja kumqona yesu. Sasa, karibu na mwisho wa maisha yake maajuzi walitoka magharibi kwa kusudi lilo hilo.

Na yesu kwa kinaga ubaga aliwafaamish kila wa lopaswa kujua. "Saa imefika hili mwan wa adamu atukuzwe. Hakika nawambia chembe ya ngano isipoanguka katika nchi ikafa, hukaa hali iyo hiyo bali ikifa hutoa mazao mengi." Mtu apendaye maisha yake atyapoteza bali asiyeyapenda katika ulimwengu huu atayahifadhi katika umilele. Anitumikiaye apaswa kunifuata na popote nilipo ndipo atakakokuwa mtumwa wangu. Baba yangu atamheshimu yejote anitumikiaye (Yohana 12:23-26).

Kifo kwetu ndiyo njia kwelekea maishani. Na hili hufundishwa na kila moja ya mbegu trillioni ulimwenguni. Hakuna mavuno pasipo kufa kwa mbegu. Swali ni, "twapaswa kuishije?"-Swali lililopendwa na wayunani kwa karne nydingi lajibowi na yesu. Nasi, kama wayunani tunaufafuta utukufu, lakini kwanza lazima kuwepo na kuangikwa. Mungu hatudai kusulubisha chochote ambacho tunakidhamini, ila kuna vitu bingi tu vipendavyo na mwishowe vinatudhuru.

Ni kanuni ya msalaba wa kristo tu, abayo itaelekeza miyo yetu, mawazo yetu, na nia zetu kwa kweli. Nasi, kama yesu, tunapokubaliana kusulubisha ubinafsi na kutoa nafsi zetu kafara kwa ajili ya wengine, basi tunaanza kuishi kwa uhakika. Hakuna njia nyinine.

Ni ujume huu ambaao wakristo watatangaza kwa nguvu za kipentekote katika siku za mwisho za historia ya ulimwengu.

NI katika wakati huu yesu anatangaza, "Sasa hukumu ya ulimwengu ipo, sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje. Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu.

Ajabu ya maajabu: Badala ya ulimwengu mdhambi kwenda msalabani kwa ajili ya adhabu yake, mwana wa Mungu asiyie na hati anakwenda pale. Ulimwengu unastahili hukumu kwa uasi wake dhidi ha yaliyo mema, haki na huruma, lakini Kristo atachukua dhambi za wote wamwaaminio na kufa badala yao?

Ni kwa sababu msalabani, angehukumiwa na kulaaniwa kwa dhambi zetu. Hii ina maana kwamba wote wawekao imani yao katika kafara yake kwao hawatahukumiwa katika siku kuu ya hukumu kwa sababu yesu amehukumiwa tayari badala yao. Na Mungu hadai malipo ya jambo mara ya pili.

Kuna kuja mara bili kwa yesu: Mara yake ya kwanza, kristo yesu alikuja ulimwenguni kuokoa wenyе dhambi(1Timotheo 1:15). Na atatokea mara aya pili si kubeba dhambi ila kuleta wokovu kwa wale wamngojao(Waebrania 9:28).

Kama ambavyo kuna kuja mara mbili, kuna hukumu mara mbili pia. Katika kuja kwake mara ya kwanza , yesu alihukumiwa na kulaaniwa kwa dhambi za wote walioweka tumaini kwake. Katika kuja kwake mara ya pili wote waliokana kafara yake ya upatanisho kwao, watahukumiwa na kulaaniwa kwa dhambi zao. Kama vile yesu alitengwa na mungu kule msalabani (mat. 27:46), ndivyo wanadhambi wasiotubu watakavyotenganishwa na mungu na maisha katika kuja kwa mara ya pili kwa yesu (2wathes 1:7-9).lakini hawa wenyе dhambi hawata fufuliwa kwa uzima wa milele kwa sababu dbambi lko ndani yao.wakati yesu alikufa kwa ajili yetu,dhambi yetu ilikuwa juu yake lakini sio ndani yake.kwa sababu dhambi haikunajisi tabia yake ,mungu aliweza kumfufua kutoka kwa wafu .

Tusipoweza kuambatanisha kuja kwake yesu mara ya mbili katika mawazo yetu, kamwe hatutaweza kuwa tayari kwa ajili ya kuja kwake kwa mara ya pili.kufikiria kuhusu kuja kwa yesu duniani kwetu kama hakimu bila kumjua ye ye kama mwokozi itakua kitu cha kustajabisha. Kufikiria siku ya kiama bila kwanza kufikiria kalvari ni hatari kubwa.

Katika yohona (12:31-33), wakati yesu alitabiri kifo chake kule kalvari aliweka matukio mawili pamoja juu ya lingine.alisema “sasa ndio wakati wa hukumu ya ulimwengu”,

kalvari katika kalvari mahali ambapo kristo angeinuliwa juu baina ya mbingu na dunia ,alikua hakimu wa wanadamu akitenganisha kila mmoja kwenye makundi mawili – waokolewao na wapotevu-vile ambavyo aliwatenganisha wale wezi wawili aliasulubishwa nao.

Injili ya yohana inafundisha kuwa wakati wetu-ndio siku ya kiama kwa wote waisikiayo. Wale wanaokubali mauti ya kristo kwa niaba yao wanahukumiwa na kuwekwa huru katika wakati huo. Biblia inasema “amwaminiye hataukumiwa ,bali ye yote asiye mwamini tayari amehukumiwa maana hajaamini” (yoh3:18)

Hukumu hii iliazia kule msalabani na itaisha yesu ajapo tena. jina lako hutokea hukumuni punde usikiapo habari njema kuhusu yesu anayekufa kwa niaba yako,ili kulipa gharama yote ya dhambi zako.Biblia inasema `kristo alikufa kwa ajili ya waovu na wakati tulikuwa ni wenye dhambi ,kristo alikufa kwa ajili yetu (warumi5:6,8)

Mwitiko wako kwa kifo cha kwake ndio utakao hakikisha hatima yako

Ikiwa utakubali kafara kwa ajili yako,utapewa kutokufa yesu atakaporejea. Ikiwa utakataa kafara yake kwa ajili yako utanyimwa uzima wa milele siku ile. Hukumu itakayofanyika wakati kristo anakuja itamaanisha kwako ile hatma uliyochagua wakati uliamua kumkubali au kumkataa yesu kama bwana na mwokozi.

6: Hukumu Ya Yesu Kuhusu Dini Mbaya

Sasa tunaingia kwa ujumbe wa mwisho yesu alihubiri kunatamnasi. Baadaye tunamkuta akiwafundisha wanafinzi wake farahani.

Katika Matayo 5 Yesu alianza huduma yake kwa mibaraka nane. Hapa katika matayo 23 Yesu anaitimiza huduma yake ya handarani kwa hukumu nane.

Mahubiri ya Yesu hapa ni vita vilivyo vyta kawaida kwenye dini mbaya- usisahau hili.

Dini nyingi ni mbaya isipokuwa dini yangu inafanya nifanane Kristo, kusamehe, kunyenyeka kuvumilia na kuwa mkweli, basi haitakuwa ya Bibilia ikiwa wataka kujua kama dini unayoiensi ni dini ya mbinguni au kuzimu, sura hii Mat. 23 itakufahamisha .

Wengine wetu tumeipata sura ya 23 ya kututia moyo, kwa maana inaweka dhahiri kwamba ni dini ya uongo inayodhibiti na kulazimisha watu.

Yesu alisema kuhusu viongozi wa dini wa kisasa wanawatwika watu mizigo ambayo wao wenyewe hawanyoshi angalau kidole kuwasaidia 9mat4). Hii ni namna ya Yesu ya kusoma ukiwa na imani ya kweli- dini ya kweli – haitakuwa mzigo, haitakuwa ngumu kubeba.

Dini yoyote iliyojengwa kwenye sheria na masharti, ni dini ya kifarisyao. Dini ya kweli inakuotesha mabawa wala sio uzito. Inafanana manyoya kwa ndege na nanga kwa meli.

Kiini cha dini ya kweli ni kusamehewa dhambi, upendo na huruma na hekima na nguvu za baba wa mbinguni kutuokoa na kutusaidia. Dini ya kweli ni kuhusu imani, tumaini na upendo (IWakorinto 13:13)

Kristo anahoredhesha vitu vilivyo vibaya kwa dini ya shetani moja na majivuno ya kidini yasababishayo viongozi kuchukua

utukufu wa Mungu (Mst 1-12). Majivuno hayo huwafanya kubuni sheria na mafundisho mambo yasiyokuepo kwenye bibilia. Siku yaja wakati hayo yatangolewa na mizizi yao (Mat 15:13) Pili, badala ya kufungua milango kwa Mungu na kwa uzima wa milele, wanaifunga huku wakifungia watu nje ya mbingu. Tatu, wanasaferi majini na ardhi kuongoa roho moja, na wanapotafuta wanafanya mara dufu mwana wa Jehanamu kama walivyo. (Mst 15) kuna makundi mengi yaliyo na uchi wa kuwavuta watu kwa dini yao, lakini wakristo huwavuta watu kwa Yesu. Hakuna swala la wokovu kwa dhehebu. Ni wokovu kwa imani ndani ya Yesu. Wajibu wa kanisa ni kuwafanya wafuasi kwa mtazamo wao kwa Kristo.

Onyo la nne la Yesu ni kuhusu matumizi mabaya ya viaapo vya wakati huo. Mafarisayo walifunza watu kuwa ni vyema wakati mwingine kusema uongo. Yesu anaangazia umuhimu wa kula kiapo na anasisitiza kuwa watu waseme ukweli wakati wote.(mstari 16-22)

Onyo lake la tano ni kwa wale wanafanya vidogo kuwa vikubwa na vikubwa kuwa vidogo. Anawaonyesha walimu wa kiroho kama viongozi wapofu wanaohangaika kutapika nzi huku wamemeza ngamia. Wanampa mungu zaka ya bizari kutoka shambani kama vile mnaazi, bizari, na jira, lakini umeacha mambo makuu ya sheria yaani adili na rehema na uaminifu. Ishara ya kweli ya dini ya uongo ni kutiwa chuku kwa maswala madogo na kupuuzwa kwa maswala makuu ya mafunzo ya Yesu kama vile imani, tumaini na upendo.

Onyo la sita la Yesu ni dhidi ya dini izingatiayo mapambo ya nje kuliko mioyo ya wafuasi wake. Dini ya uongo ina sura nzuri ya nje ila ndani hamna chochote bali ulafi na ubinafsi Yesu alisema, vikombe huwa safi tu ikiwa ndani yao ni safi na wala si nje tu (mst 25-26).

Onyo la saba ni dhidi ya dini ipatoshayo watu waliojiusisha nayo. Alsema viongozi waliopatokwa maadili ni kama makaburi yaliyopakwa na mifupa ya wafu na miili iliyooza. "Hivyo ndivyo mlivyo" Yesu aliwaambia "nje mwapendeza ila ndani mu waovu" Yesu aliwahimiza kubadili mioyo yao (mst 27-28)

Onyo la mwisho la Yesu ni kwao wanaojenga makaburi ya manabii wakidai kwamba wao wenyewe wasingeungana na babu zao kuwaua manabii waliotumwa na mungu.

Mababu zao waliwaua manabii kwa sababu waliingia tamaduni zilizo kuwa mbaya. Kama vile Yesu alivyoshambulia matendo machafu ya wafarisayo na walimu wa dini. Wanafiki hawa waliodai kuwa hawangewaua manabii ndio walimuua Yesu. (mst 29-35).

Katika fungu la 36, Yesu alitangaza kuwa hukumu ingelipata taifa la wayahudi wa wakati wake kwa sababu ya mambo haya yote. Hukumu ilikuja wakati askari wa kirumi walivamia nchi wakawateka nyara mijji yake yote, wakaua au kuwapeleka utumwa wakaaji wake wote.

Kwa kukamilisha Yesu alisema kwa huzuni " Yerusalem, Yerusalem! Watu wako wamewaaua manabii na kuwapiga mawe wajumbe walotumwa kwako. Nimejaribu kuwakusanya vifaranga wake ila haukuniruhusu. Na sasa hekalu lako litakuwa ukiwa bila uwepo wangu. Hautaniona tena hodi utakaposema, " amebarikiwa mtu ajaye kwa jina la Bwana" (mst 37-39.

Huyu si mtu wa kawaida azungumzaye hapa. Kristo mara nyingi alijaribu kutetea Yesusalema kutokana na shida kama kuku ahifadhivyo vifaranga wake ndani ya mbawa zake. Yeye ni Mungu mnyenyekevu na mupole. Hakika hili ni neno tamu zaidi la huruma ya kimbingu lisemwalo kwa dini iliyochafuka kama hiyo. Twaweza kuhitaji hukumu zake bali hatuwezi

kuzuia upendo wake. Kunao siku zote upendo kwetu ndani ya moyo mmoja. Siku zote yupo kutusaidia ikiwa tutamtafuta.

Ni picha bora kiasi gani Yesu anatupatia mwishoni mwa sura ya 23. hapo tunaye kuku mzazi. Anapogundua hatari, anatoa kelele kidogo na vifaranga hukimbia kwake. Wanapigania nafasi kifuani kwake na kung'ang'ania kujisitini mabawani kwake kuliko na usalama. Yule mwewe aliye juu angani hawezi kuwafikia. Wamesitiriwa mbawani mwa mama yao. Wako salama salimini na wanafuraha kamili. Ni bahati kwetu kuwa kama hao na tunaweza kuwa ikiwa tuna picha halisi ya Mungu.

7: Unabii Wa Yesu Kuhusu Siku Za Mwisho

Ujumbe wa unabii wa Yesu katika Matayo 24 na 25. Luka 21 naMarko 13 unafahamika kama hubiri la mlimani kwa maana ulitolewa katika mlima wa misaiutuni ulio mkabala na jiji la Yerusalemu. Katika ujumbe huu, anawaambia watu wake kuhusu mwisho wa dunia yao na watakachofanya kwa wakati huo. Yesu alitoa ujumbe kwa namna ambayo haikuashiria uharibifu wa Yerusalemu tu, lakini pia matukio ya mwisho wa dahari. Kwa maana nyingine kile kingelitokea kwa Yerusalemu ndicho kitakachotokea katika ulimwengu wa dini lakini kwa namna kubwa zaidi.

Hubiri la mlimani linamlenga Yesu kwa sababu mwisho utafika tu baada ya habari njema kuhusu kufa kwa Kristo kwa ajili yako na mimi mumehubiriwa ulimwenguni kote (Matayo 24:14). Ni mfalme na Bwana wa mabwana aliyetufia na ambaye atarejea hivi karibuni kwa utukufu. Hili linatoa umuhimu mkubwa kwa sura zitakazofuata.

Kinachoonekana kutoka mwanzo hadi mwisho katika hubiri la Yesu ni ujumbe wa maonyo himizo la kuwa sawa kuliko kujua tu na kukiri kuwa u sawa.

Kunao mfumo wa matukio yajayo kutokujali kwa dini na mateso kuongezeka kwa kuchanganyikwa wa taifa na kimataifa, mitemeko ya ardhi, uenezaji wa injili ulimwenguni, uasi wa kidini, jaribio kuu, kuja kwa mpinga Kristo, na ishara za kiasili kuuashiria kuja kwa Kristo kukusanya watu wake.

Kwa sehemu kubwa, ujumbe huu umegawanyika katika sehemu tatu za wakati: Matukio kabula ya wakati, wa shida, wakati wa shida wenyewe, na ukombozi wa Yesu kwa wateule kutoka kwenye wakati wa shida. Mwanzo wa wakati wa shida utaashiriwa kwa kuja kwa uharibifu usimamao kwa patakatifu. (Matayo 24:15)

Tunapounganisha aliyopitia Yesu na maonyo yake, na jujumulisha maelezo yaliyomo katika unabii wa 2 Wathesalonike 2, na Ufunuo, na maandiko mengine, ni rahisi kupata taswira ya mambo yajayo. Kinachofuata ni pendekezo tu bila nia ya kutatanisha sisitizo letu. Kwamba sababu ya unabii ni ya kiroho wala si ya kiusomi, na maneno ya unabii yanakukwa wazi pindi yatimiswapo.

Kwanza, uihisho wa kweli na wa uongo utaonekana katika uso wa dunia ya kidini. Hali itakuwa sawa na ya ulimwengu wa kirumi wa karne ya kwanza kwa uovu na kukata tama. Itakuwa wakati wa kuongezeka kwa mvutano wa kimataifa na kusambaratika kwa maadili ya mataifa. Haya yote yatadhihirishwa na ishara katika dunia, angani na baharini.

Matukio yajayo yatawaweka watu kwenye mazingira yatakayosababisha na kulazimisha kukomaa kwa kiroho. Mema na mabaya yatakomaal upesi katika hali hii. Kadiri injili inavyohubiriwa kwa kila taifa, itachochea kukukataliwa na watu wa kawaida bali kukataliwa na viongozi wa kidini. Msisimko wa ljumaapili ya mitende utarudiwa kila mahali.

Katika tukio la kinafiki la kidini dini za uongo zitaongezeka na kushamiri itakuwa kama karne ya kwanza ambapo dini za kishenzi zilipigania uwepo wao huku injili ya Yesu ikishambulia imani hii ya uongo iliyokuta mzizi.

Wale ambao hawajajengwa kwa ukweli wa maandiko watakosea kwa maamuzi yao na wengine ambao wamekuwa na njaa ya neno watasikia sauti ya mchungaji wa kweli na kushikilia injili yake. Na watambia wengine kile ambacho wamepokea.

Kama ilivyo kuwa wakati wa Yesu makundi ya kidini na Filisofi, yalikuwa yanapingana yenyewe, yataungana ili kuushawishi ulimwengu kuunga umoja wa kidini kwa lengo la kutatua matatizo ya kimataifa. Viongozi wa kidini wataomba

kuungana na selikali ili kupata nguvu katika kutoa sulufi juu kwa ulimwengu wote.

Mafundizho na imani ya kishetani itashamiri kwa wengi wa wakaaji wa dunia. Sehemu kubwa ya sheria ya Mungu itashikitiwa tu kwa nje kama Herode aliyefanya mambo mengi mema kwa furaha lakini akamuua Yohana, ndivyo itakavyokuwa katika ulimwengu wa dini. Lakini jaribio itetao uharibifu muungano wa dini na serikali- hatimaye utawavamia wachache waliodhunauliwa ambao wanazitunza sheria za Mungu na kuwa waaminifu katika Kristo.

Kwa sababu ya miyo migumu, dunia imeachwa kwa uasi na udanganyifu mkuu huku, kuja kwa Kristo kukiingizwa katika sehemu mbali mbali duniani(II Wathesolonike 2:1-12). Kwa wakati huo watu wa kweli wa Mungu watatambuliwa kwa kuhasi kwao kufa kwa ajili ya Kristo. Watatiwa muhuri na roho wa Mungu kwa ajili ya umilele.

Wakati wa shida kwa wale walio na imani kwa Yesu, unakuwa pia wakati wa shida kwa ulimengu pindi ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa na watu ianguikapo. Ulimwengu wote utagawanywa katika makundi mawili. Kundi kubwa laonyesha picha ya bwana wake, shetani kama yeye (shetani) ni wauaji na wadanganyifu. Kundi dogo linaonyesha mfano wa Kristo. Wanawaombea wateai wao. Ulimwengu unatazama mamna na mabaya yakiwa yameiva tayari kwa mavuno. Ndipo kunaonekana ishara ya mwana wa Adamu angani, na mataifa yote yataomboleza kwa uchungu kwa ajili yake, hiyo ni kusema wale isipokuwa wafuasi wa Kristo wanaoshangilia kwa sababu saa ya ukombozi wao umefika.

Lazima ikumbukwe kwamba uenezaji wa injili kote duniani ndiyo ishara hasa ya kukaribia kuja kwa Kristo (Matayo 24:14) pia la muhimu sana kwa wakati huo ni onyo kwamba jamii

itakuwa kama mzoga uliooza mwishoni mwa toleo la mwisho la neema (Matayo 24:28).

Unabii huu unawakilisha ishara ya mpinga Kristo, jambo liletao uhambifu na ishara ya Bwana yetu arejeaye, ishara ya mwana wa Adamu mbinguni (Matayo 24:15,30)

Jaribio liletao uharibifu ni neno linalomaanisha muungano wa kanisa na serikali. Inamaanisha mamlaka ya kuabudu Miungu yaabudwayo na wasioamini, wanaotesa na kuharibu. Muungano wa kanisa na serikari katika siku za mwisho utajenga jaribio la uharifu ambalo litaangamiza watu wa Mungu.

Je, kulikuwepo na lile jaribio liletao uharibifu. Katika juma la mwisho la Yesu?hakika lilikuwapo. Lilitimizwa kwa Yudas, msaliti aliyewaomba mamlaka ya kiyaudi na askari wa Kirumi wamsaidie kumfuma Yesu ili amsaliti Bwana wake. Je, haupati picha? La! Uenezwaji wa injili na ulinzi wa Bwana umeahidiwa kwa wateule wake (Matayo 24:14,22-31)

Kwa kuongozea, visa vitatu vya mwisho katika sura zifuatazo, Matayo 25, zimejaa tumaini kwa wateule na maonyo kwa wanaojidai kuwa wakristo lakini huwana Kristo aliyeishi ndani yao.

Fungu la 35 katika matayo 25 ni hakikisho kwamba utabiri huu utatimizwa fungu hili pekee ni tosha kuonyesha kwamba Kristo ni masihi na injili yake ni ya kweli milele.

Matayo 25.

Usisahau kwamba sehemu ya pili ya hubiri la Yesu la mizaituni li katika matayo 25, ujumbe ni sawa (uleule) katika visa vyote vine na unalinganisha maneno makuu ya hubiri kama vile linda na kuwa tayari. Hukumu imekaribia na haiwezi kuepukika.

Kilele cha kisa cha kwanza katika fungu la 45-51 katika sura 24 ni swali: “Ni nani basi mwaminifu na mtumwa mwelevu?”

Swali ladekeza kwamba mtu wa namna hiyo ni adimu. Mwawazoni, Yesu aliona siku za giza zijazo wakati ambapa viongozi wasomi wa kanisa lililo potoka lingekuwa na hatia ya Jehuri na ukali upitao kiasi kama uloonyeshwa na kitendo cha Yule mtumwa mwovu.

Kisa cha mwisho katika Matayo 24 na cha kwanza katika matayo 25, chaonya kwamba kuja kwa Yesu hakungefanyika wakati walitarajia ila kungekawia katika mfano wa wanawali kumi, Bwana harusi (Yesu) haji saa nne au hata dakika tano kabla waliomngojea wanalala, lakini hawalaumiwi kwa hilo. Lawama hii kwa wale hawajajiandaa kwa kukawia kwake. Kila mwanamwali amewakilishwa na taa yake, ambayo inafanya kazi vyema ikiwa imetiwa mafuta yanayowakilisha roho mtakatifu wa Mungu. Wale wanawali wapumbavu waliopuuza kubeba chupa moja ya ziada ya mafuta wakifiria walikuwa na ya kutosha kukidhi mahitaji yao. Lakini alipokawia Bwana harusi kinyume na alivyotarajiwa, taa zao zilizima- wanawali watano tu waliokuwa na mafuta ya ziada waliziacha taa zao zikiwaka kwa bahati mbaya wale wajinga wakiwa wanasubiri kupata mafuta nyingine Bwana harusi aliwasili. Yeye pamoja na wale watano werevu walienda kwenye sherehe ya harusi na mlango ukafungwa.

Nusu ya wanawali waliokuwa wanasubiri maana yake, nusu ya wakristo watatupwa nje kutoka kwa uzima wa milele atakapokuja Kristo kwa sababu hawatakuwa na Roho mtakatifu wa Mungu (Mafuta) katika maisha yao (taa). Ni kundi gani unahesabiwa kwalo.

Mfano wa talanta (Matayo 25:14) unadokeza kwamba hesabu ya talanta ambazo Bwana hutoa zinakuwa tofauti kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Hata hivyo, hakuna atakayehukumiwa kwa hesabu ya talatha anayo ila kwa namna ambavyo alizitumia. Kunao wale wanaotaka kumheshimu

Kristo kwa talanta zao atakavyorejea na wanaofanya hima kuziimarisha. Kuna wale wanaotaka kumheshimu Kristo atakaporejea bila kufanya hima kuziimarisha na kuzidisha. Hakuna mahali pa watu wa kundi hili la pili katika ufalme wa Mungu.

Hebu sasa na tutazame fungu la 31-46 kuhusu unabii wa siku ya hukumu wakati Kristo ajapo kwa utukufu wote akisindikizwa na malaika wa mbinguni. Ni siku ya kushangaza namna gani itakavyokuwa. Hakuna maelezo katika vitabu yanayosisimua kutamausha kama haya. J.Manro- Gibson anasema, hakuna hata neno moja litakalobadilishwa hakuna hata sentensi itakayoachwa hakuna wazo litakaloangezwa. Hii siku inabeba alama za ukamliju iwe tunaiangalia kwa mtazamo wa uungu wa mzungumzaji au kwa mtazamo wa uanadamu wake(kitabu cha maelezo katika Matayo Uk 366).

Katika mfano huu wa Mbuzi na Kondoo, Yusu anajundisha kwamba atahukumu watu katika siku ya mwisho kwa kutumia jinsi ambavyo waliwahudumia wale wasiojiweza katika jamii. Katika siku hiyo atasema, kama mlivyowafanyia hawa ndugu zangu wadogo, ni mimi mliyofanyia (Matayo 25:40)

Lengo la hukumu ya kwamza mwishoni mwa sura ya 24 ni kwa viongozi wa kanisa. Lakini mfano wa pili na wa tatu ni kwa washiriki wa kawaida wa kanisa. Yesu atakaporejea hutahukumu kwa imani ya mafundisho, ila kwa kufanana au kutofanana kwako naye katika upendo na upole.

Mfano wa kondoo na mbuzi ndio wakati tu ambapo Yesu anajuta mwenyewe mfalme. Angalia pengo kuu liliopo baina ya maneno makuu ya mfalme. ‘Njooni kwangu’ – tokeni kwangu swala kuu ni umemfanyaje Yesu Kristo? Swali lingine umewafanyaje maskini wa Kristo? Kila mtu aje hapo kulijibu lile swali la kwanza.

8: Yesu Awatawadha Wanafunzi

Katika Yohana 12, tunasoma kuhusu kupakwa mafuta kwa miguu kwa manukato na kutawadhwaa kwa majozi hapa katika Yohana 13, Yesu atawadha wanafunzi

Wake sura hii inaanza na yesu kuwaonyesha wanafunzi wake upendo wa dhati.

Licha ya Yesu kujua kwamba wanafunzi wake wangemwacha masaa machache yafuatayo, hakuchi kuendelea kuwapenda. Yesu aliihuka kutoka katika meza, alivua nguo yake ya nje, akajivunga taulo kiunoni. Akamimina maji kwa basini na kuanza kuwatawadha wanafunzi akiwapanguza na taulo aliyoifunga kiunoni.

Alichokifanya Yesu katika tukio ulikuwa ni mfano ulioigizwa katika huduma yake. Aliacha karamu ya mbinguni, akavua utukufu wake wa nje akajifunga ubinadamu akainama kuosha uchafu wa maisha yetu ya kila siku kwa wale wanaodinda kumuruhusu Kristo kuosha dhambi zao asema, nisipokuosha hauna sehemu nami (Yohana 13:8). Katika huduma hii, Yesu ni kielelezo cha vile itupasavyo kuhudumiana. hatujateuliwa kukejeli uchafu au miguu ya wenzetu. Tumeteuliwa kuwasaidia kwa unyenyekevu wakubali utakazo wa Yesu.

9:Yesu Aeleza Kuhusu Pasaka

Yetu ni dunia ya uovu na mauti. Ni kitu gani wasomi wakuu duniani wamefanya ili kutusaidia kuelewa na kushinda tatizo la dhambi na mauti.? Socrates alifundisha kwa miaka 40, plato kwa miaka 50, na Aristotle kwa miaka 40,- takriban miaka 130. lakini mchango wao ili kutatua matatizo hayo hayafikii kitu chochote. Ndipo akaja Yesu wa Nazareti, aliyefundisha zaidi ya miaka mitatu na akatupatia suluhisho la matatizo ya uovu na mauti. Suluhu kwa matatizo haya yote ni yeye mwenyewe!.

Hapa tunayo rekodi ya maneno ya Yesu katika sura ya 14:22-24. walipokuwa wakila, Yesu alitwaa mkate na baada ya kushukuru akaumega na kuwapa wanafunzi wake akisema, “twaeni, huu ni mwili wangu” kisha akachukua kikombe baada ya kushukuru akawapa na wote wakakunywa kutoka mle “hii ni damu yangu ya upatisho imwagikayo kwa ajili ya wengi” akasema kwao.

Hebu fikiri kuhusu hili kwa mda kidogo. Hapa kuna mgalilaya mkulima ambaye anakaribia kuuwawa kama jambazi na anafutilia mbali ahadi ya Mungu kwa watu wake iliyodumu kwa miaka elfu moja mia tano! Kama hangekuwa zaidi ya mwanadamu, watu wangemcheka, alivyo mkakamavu. Lakini hawasemi, “anafikiria ye ye ni nani? Au huyu mtu ni chizi?”

Kwa sababu ya kuwa ye ye, maneno ya Yesu hayahitaji kusahihishwa mahali Fulani alialika ulimwengu uweze kumtwika mizigo yake (Mat 11:28) na katika Yohana 15:5 aliwaambia wanafunzi wake kwamba hawangefanya lolote kwa muda bila ye ye.

Kama mwanadamu wa kaiwada angethubutu kudai hivyo, angechekwa lakini si Kristo.

Mambo mengine ni dhahiri kuhusu pasaka. Yesu kawaida alijiona kama mwanakondoo wa pasaka ambaye

angepatanisha dhambi za wote ambao wangejitoa chini ya ulinzi wa damu yake ilomwagika.

Kuna njia nyingi za kufa bila kumwaga damu kama vile kujitia kitanzi, kunywa sumu, ila yesu alikufa kwa njia ya kumwaga damu kama kondoo wa pasaka. Ni kwa imani katika damu ya Yesu tunahesabiwa haki. Kuhesabiwa haki huku hakutufanyi kuwa haki ila kunatangaza kuwa tu haki. Yesu anatupatia haki hii kwetu kama karama ya bure ya Mungu ibadilishavyo na dhambi zetu. Ili tusilipe alikufa ili tuishi.

Ili tufike mbinguni, tunahitaji kuhesabiwa haki na Mungu. Haki ya kuhesabiwa ambayo Yesu anataka kutupa kama karama ya bure, ni asilimia mia moja. Haki ya kutakaswa ambayo ni matokeo ya matendo yetu mema si asilimia mia moja. Kwa sababu tunahitaji asilimia mia moja ya haki kupata uzima wa milele, lazima tukubali kwa imani zawadi ya Mungu ya bure kutoka kwa Yesu. Wale wawekao imani yao kwenye haki yao watakosa kwa sababu chini ya asilimia mia moja ni alama ya kukosa. Si swala la nini tulicho bali nani tuliyeha naye.

Yesu aingiapo miyoni mwetu na haki yake kamiliivu, atahakikisha kuishi maisha yake kuititia kwetu, huku akitufanya kuwa haki kila kuchao- Haki hii haitatuokoa ila inaonyesha ya kwamba tumeokolewa. Hatuhitaji kuwa wema ili tuokolewe bali tunaokolewa ili tuwe wema.

Meza ya Bwana yatufunza kuwa kusulubiwa kwa kristo hakukuwa makosa ila ilikuwa mbinu ya Mungu ya kouko ulimwengu.

Mkate ulomegwa uliashiria mwili wa Yesu uliovunjwa msalabani kwa ajili yetu. Na divai iliashiria damu ya Yesu iliyomwagika kwa ajili yetu. Kuukubali mkate na divai ni kuashiria kukubali kafara ya Yesu Kristo juu yetu.

10: Yesu Asema Msifadhaike

Yohana sura 14-16 hurekodi mafundisho ya mwisho ya Kristo kabla ya kusulubiwa. Wakristo wengi hujiisi kuwa Yohana 14 ndio sura ya kutia moyo zaidi katika bibilia. Hotuba hii ya kuyeyusha miyo ni kama utukufu huwakao wa juu linalozama, likiwa limezungukwa na mawingu tayari kuzama ndani ya mawingu meusi angani- mawingu yanayotikizwa na miezo, radi na ngurumo.

Lakini ajabu ya maajabu, badala ya kuzidiwa na uoga, Kristo anaanza kuwaandaa wanafunzi wake kwa majaribu yajayo. Mara mbili katika sura hii anasema ‘msifadhaike miyoni mwenu’.

Haijalishi vile mtu alivyo mtanashati, tajiri na mwenye nguvu, maisha hayanyooki kwa muda mrefu. C.S Lewis alisema, ‘nusu ya ubora wa maisha imejengwa kwenye vivuli ikiwa tutaamini kuwa vivuli vinaruhusiwa kwa upendo na hekima ya Mungu, na kuwa mikasa haidumu milele, basi tunaweza kustahimiri matatizo ya maisha.

Mikasa mingi huja bila taarifa. Hakuna yeote wetu ajuaye kile ambacho siku imebeba, kwa hiyo basi, twapaswa kusikiza ushauri wa Yesu ‘msifadhaike miyoni mwenu’ hakuna chochote cha kuogopa kwa sababu yu pamoja nasi katika mawimbi na vile mwangani.

Yesu anatoa sababu saba za kutofadhalika.

1. Mungu anayo mahili kwa ajili yetu pamoja naye, na Yesu alienda kutengeneza mahali kwa ajili yetu.
2. Yesu angerejea ili kutupeleka kwa baba (14:3)
3. Njia inayokwenda kwa baba ni Yesu. Hakuna ajaye kwa Baba ila kupitia kwangu (14:6)
4. Wale walio na imani katika Yesu watafanya hata kazi kubwa kuliko zilizofanywa hata na Petero, kwa mfano

alitumiwa kuongoa watu elifu tatu katika siku ya Pentekote (14:12)

5. Yesu angemwomba Baba yake kumtuma mwagine, mfariji ambaye angechukua nafasi yake.
6. Huyu msaidizi mpya angewaongoza wote kwenye kweli-kweli ambayo ingetoka kutoka katika maisha ya Yesu, kifo na ufuo (14-25).
7. Kristo angeaachia kumbukumbu ya amani “amani niwapayo haifanani na amani ulimwengu huwapayo. Kwa hivyo msifadhaike wala kuogopa (14,27 cev)

Kristo ndiye njia kweli na uzima (14:6). Japo wengi wataokolewa pasipo kusikia jina lake. Majina ya wengi katika Waibrenia II ambao hawakujua lolote kuhusu Yesu lakini watakuwa katika ufalme wa Mungu kwa sababu ya kile Kristo aliwatendea msalabani. Ni kwa sababu ya Kalvari tu, kila mmoja anaokolewa kama ambavyo watu hunufaika na umeme bila kujua jinsi na mahali ilikotengenezewa. Kuna wengi wanaopata manufaa ya kafara ya Yesu pasina kujua wapi na vipi ilitolewa. Siku moja watajifunza kuhusu kafara ya Yesu kwao.

Katika Yohana 14:15-18, Yesu anadhidi kutuma msaidizi kuwa na wafuasi wake milele Yesu ndiye msaidizi wa kwanza kuja kwa roho mtakatifu kungekuwa msaidizi mwagine kupitia kwa roho mtakatifu, Yesu angekuja kwa watu wake(14:14). Huyu Roho angefahamika kuwa Roho wa Mungu na Roho wa Kristo (War 8:9). Hili lingekuwaje? Ni kwa sababu Mungu ni mmoja. Yesu angelisalia mbinguni na Baba kuja ulimwengu afe kwa ajili yetu, hatungegundua tofauti. Ikiwa tumemwona Yesu, tumemwona Baba (14:8-11). Na kwa njia hiyo, ikiwa tuna Roho mtakatifu basi tunaye Yesu.

Yesu na Roho mtakatifu ni kama sura mbili za sarafu moja ziko tafauti kabisa kutoka kwa nyingine lakini ni moja kwa sababu haiwezekani kuwa na moja pasipo nyingine.

Wakati kumbukumbu 6:4 inazungumzia juu ya Mungu mmoja, neno la kiibrenia (Echad) (moja) ni sawa na lile lililotumika mwanzo 2:24 lisemalo Adamu na Hawa wakawa mwili mmoja. Yesu aliomba kuwa wafiasi wake wamoja ye ye na Baba walivyo wamoja (Yohana 17:21-22). Umoja huu si wa idadi ila ni umoja uletwao na umoja wa Roho (Yohana 17:23).

Fananisha Mat 7:11 na Luka 11:13. Fungu moja li sambamba ya yingine. Matayo anasema, ikiwa ninyi japo waovu mlivyo mwajua namna ya kuwapa watoto wenu zawadi njema, sembuse baba yenu huko mbinguni awezavyo kuwapa zawadi nzuri kwa wale wanamwomba. Luka yasema ikiwa ninyi waovu mlivyo mwawenza kuwapa watoto wenu zawadi nzuri sembuze baba yenu wa mbinguni aweza kuwapa zawadi nzuri ya Roho mtakatifu kwa wote wanaomwomba. Ufupisho wa mafungu haya mawili ni kwamba, kupata Roho mtakatifu ni sawa na kupokea zawadi nzuri kutoka kwa Mungu. Wakristo ni matajiri kiasi gani!

Yesu aliwaambia wanafunzi wake katika pasaka ya mwisho kwamba yu aenda kuwaandalia mahali kwa Baba kama Yusufu aliyekwenda Misiri kuandaa kujaza magala ili kuokoa familia yake iliyokuwa imetishiwa, ndivyo Yesu alivyotoweka kwa kitambo kidogo ili atoe wokovu kwa familia yake.

11: Yesu Mzabibu Wa Kweli

Sura ya kumi na nne ya Yohana yafunga na usemi “Njoo sasa tuondoke” Hivyo tuliyonayo katika sura tatu zifuatazo yalizingumzwa njiani kwenda Gethsemane. walivyotembea sako kwa bako chini ya mwanga wa mbalamwezi wangeweza kuona mianga midogo kwenye bustani ya mizabibu, ambapo matawi ya mizabibu yaliokatwa yanakuwa yanachomeka.

Ni katika hatua hii, ambapo Yesu aliwageukia wanafunzi wake na kusema, mimi ndimi mzabibu wa kweli na baba ndiye mkulima. Hakata kila tawi lisilozaa ili liweze kuzaa zaidi – kaa ndani yangu na mimi ndani yenu. Hakuna tawi linaloweza kuzaa bila ya kuwa ndani ya mzabibu kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu (Yohana 15:1-4)

Matawi mengine hayazai kamwe matawi haya yafanyayo mzabibu kuonekana na afya na kushamiri huchukua nguvu za mzabibu ambazo zinatafaa kuzalisha mizabibu, kwa hivyo mkulima wa mizabibu huzikata maana hazizai zabibu.

Hata matawi yayozaa zabibu yanahitaji kusafishwa ili nguvu zao zitumike kuzalisha zabibu badala ya kuni na matawi yasiyofaa.

Kusafisha ni kuchungu lakini matokeo ni ya ajabu. Wakati Mungu anataka kusafisha vitu kutoka maisha yako ambavyo havizai matunda kwa ufalme wake usimzuie. Wakristo borawale waliojazwa amani na furaha- ni wale waliomruhusu Mungu kusafisha upambavu na vita visivyofaa katika maisha yao.

Mwishoni mwa sura ya mwisho tunasoma kuhusu mwaliko wa Yesu kunyanya mezaani na mkristo aliyefufuliwa. Wale ambao wameonyesha kwamba wamempokea Kristo aliyesulubishwa kwa njia ya kula mkate na kunywa divai, sasa wanatembea chini ya mamlaka ya roho wa Yesu huzaa

matunda mengi. Hakuna mkristo halisi asiyezaa matunda na mkristo hatazaa zaidi ya tunda la upendo.

Mara nyingi katika safari hii, Yesu anatumia neno ‘kaa’. Maisha ya mkristo yanategemea kukaa ndani ya Yesu. Lazima tukae ndani ya Yesu kama vile tawi. Tukikatwa kutoka kwa mzabibu ‘Yesu’ tunakufa kiroho na mahali pekee pa matawi yaliyokufa ni motoni. Matawi yasiyozaa hayafai kitu chochote.

Kwa kadri tunavyoolewa hitaji letu, tunakaa ndani ya Mwokozi lakini wakati tunapofikiria kuwa sisi ni wazuri, werevu na wenye nguvu, wakati huo tuna hatari ya kutengwa kutoka kwenye tawi.

Mti wa mpera haujitätahidi sana kutengeneza mapera. Na mzabibu haujitätahidi sana kutengeneza zabibu. Hutokea tu. Tukiunganishwa na Kristo kiasi kwamba maisha yake yako ndani yetu tutazaa matunda mengi.

Kwa nini Mungu anasema kwamba tutatupwa motoni kama hatutazaa matunda. Ni kwa sababu madhumuni ya mzabibu ni kuzaa matunda. Kwa hivyo kama hatuzai tunda zuri la upendo, hatuna sehemu katika ufalme wa Kristo. Ikiwa mioyo yetu na i sawa maisha yetu yako sawa.

Mara nane katika fungu la 9-13, tunasoma kuhusu upendo hatujaitwa kuzaa kisichozaalika. Msalaba wa Yesu si chuma ila mtu. Chemichemi ya upendo ni kujua kwamba tunapendwa. Hakuna atakayempenda Kristo mpaka atakapogundua kwamba Kristo anampenda- kama alivyo. Na kama twaishi tukiunganishwa na Kristo, tunakuwa kama yeze. Sisi, vilevile tutawavuta watu kwa upendo. Tuna chaguzi mbili tu kuwa wapenzi wa wengine au kuwachukua.

Katika fungu la 7, Bwana anasema “mkikaa ndani yangu na maneno yangu ndani yenu, ombeni chochote mtakacho, na mtapewa” Fungu hili lapaswa kueleweka katika tunda la upendo na unaendelea kuomba kwalo, utapewa. Ikiwa wahitaji

tunda la kuongoa roho kwa ajili ya Yesu na unaomba Bwana kwa ajili yalo utapewa. Ni mapenzi yake kwamba uzae tunda kwa ajili yake.

Sura ya kumi na tano ya injili ya Yohana inaangazia amri tano za Kristo ‘njoo’ jifunze ‘aminii’ ‘fuata’ na ‘kaa’. Mkristo ambaye hutii haya ndiye mkristo wa kuzaa tunda.

12: Ujumbe Wa Maagano Wa Yesu

Ujumbe wa maisha kwa wanafunzi wake ulikuwa ni kuwatia moyo kwa kile kilichoonekana kama kazi ngumu- kupeleka habari njema kuhusu masihi aliyesulubishwa na kufufuka kwa ulimwengu usiomani. Hiyo shughuli ingewezezanaje kama Yesu alikuwa anawaacha?

Yesu anaanza kwa kuwaambia wanafunzi wake kwamba ni muhimu yeye awache ndiposa Roho mtakatifu aje achukue nafasi yake kwa kuwa Yesu aliubeba mwili, ilikuwa vigumu kwake kuwa na waumini kote duniani kwa wakati mmoja. Lakini hili lingewezezanaje kwa Roho mtakatifu kwa kuwa yeye hakubeba mwili.

Wakati Yesu alikuwa na wanafunzi wake hawakuogopa maadui wao uwepo wake ungekuwa ngao yao. Lakini sasa walipaswa kuweka imani yao katika uwepo wa roho asiyeonekana. Yesu aliwaambia kwamba Roho mtakatifu ajapo atawaonyesha watu dhambi yao hasa ni kukataa kumwamini, kwamba haki ya kweli ni zawadi kutoka kwa Mungu na kuomba kuna hukumu ijayo.

Dhambi, haki na hukumu ndizo kweli kuu za maisha. Dhambi na kinyume chake haki mara kwa mara hugongana na kusababisha hukumu. Leo ndiyo hukumu ya jana. Hakika kama vile kufuja kidogo tu laweza kuzamisha meli hivyo dhambi moja iliyopaliliwa yaweza kuangamzia mdhambi.

Wakati Bwana wetu aliwazia dhambi moja hasa ambayo ni mbaya zaidi ya nyingine zote. Kule kuamua kukataa upendo wa Mungu uliodhihirishwa katika kafara ambayo Yesu ameweka kwa ajili ya kila mmoja wetu.

Ikiwa tutapuuza kile chema ambacho mbingu yaweza kutupatia tumezama chini zana kuliko asili ya mwanadamu yaweza kwenda. likukataa yesu lazima tuachane na mikono

yake ambayo imejaa zawadi, mikono ambayo inatupatia mibaraka tunayohitaji ili kuishi maisha yaliyojawa na usalama, amani na furaha.

Fungu la kumi na nane linatuambia kwanza kuhusu ugonjwa wa mwanadamu, dhambi na pia kuhusu suluhu pekee, na haki. Suluhisho hili ambalo Yesu anatupatia ni bure. Lakini laweza kupokelewa kutoka katika mikono iliyo na makovu ya misumari ya Kristo aliyefufuka.

Sisi, ambao tulifanywa wenyе dhambi kupidia kutotii kwa Adamu, tumefanywa wenyе haki kupidia kutii kwa Yesu. Warumi 5:19). Anaweka utiifu wake mkamilifu kwenye akaunti za wale wote waloweka imani yao kwake. Japo hatukuchangia kwa kile Adamu alitufanya, vilivile hatukuchangia kwa kile alichotufanya Kristo. Ila tunawaijibikia uchaguzi wetu kuhusu nani tutakayemfuata. Tunaweza kumfuata Adamu na kubaki wenyе dhambi, au tunaweza kumfuata Yesu na kupokea zawadi yake ya bure ya haki.

Baada ya dhambi na haki huja hukumu (Yohana 16:8-11) ikiwa tutangangania dhambi tutahukumiwa kifo, kwa kuwa mshahara wa dhambi ni mauti (Warumi 6:23a). Lakini kama tutapokea uzima wa milele (Warumi 6:23b). Kwa kuwa Yesu alihukumiwa kwa dhambi zetu, hatutahukumiwa. Hakuna hukumu kwa wale wako ndani ya Kristo Yesu (Warumi 8:1).

Siku ya hukumu hukujia unapokutana na Kristo na kukabiliwa na uamuzi wa kukubali au kukataa Yesu kwa kuwa ye yote asiyе na Yesu yu kinyume chake. Bali amchaguaye Yesu anao uzima na hatahukumiwa; amevuka kutoka mauti kuenda uzimani.(Yohana 5:24).

Waweza kuamua safari ya hukumu na hatima yako sasa hivi. Bibilia inasema, amwaminiye mwana anao uzima wa milele, bali amkataaye mwana hataona uzima, maana ghadhabu ya Mungu juu yake (Yohana 3:36).

13: Ombi La Mwisho La Yesu

Katika Yohana 17, tunalo ombi ambalo Yesu aliomba huku kivuli cha ajabu kuhusu ombi hili ni kwamba Yesu anatazama mbele kwenye msalaba kama mahali ambapo kwapo atainuliwa, ambapo Baba atatukuzwa na wokovu kupatikana kwa ulimwengu.

Katika ombi hili, Yesu anajiweka wakifu tayari kuwa kafara, na kwa wakati huo ndiye kuhanini mkuu na mwana kondoo wa kafara, anawaombea pia wafuasi wake sio kwamba wawe wakwasi wa mali au waheshimiwa bali wawe na umoja. "Wametii neno lako" Yesu alimwambia Baba (mst 6). Watu hawa wadhambi na wadhaifu walipongezwa na ukamilifu wa Yesu. Ndivyo ilivyo kwetu, Mungu atuangaliapo anaona tumefanikiwa na joho la haki ambalo Kristo ametuvika.

Kristo anaomba kwamba Baba awangalie na kuwatunza wote wawekao imani kwake. Hatutajikimu bali mkono wa Mungu mabegani mwetu ni ule wa ndugu atupendaye. Hatatuachilia. Hatutapotea, tungali twashikilia Yesu huku tukitazamia kuwa kama alivyo.

Mara kadha kwa ombi hili, Yesu anaomba umoja kati ya wafuasi wake (mst 11,22-23). Walakini umoja si kufanana umoja huumaanishi kwamba tuafikiane na wafuasi wengine wa Yesu, bali in maana kwamba tunaweza kutofautiana pasipo kukosana. Huenda kukawa na tofuti kubwa kwa mafunzo na itakadi za dini mionganoni mwa wakristo, kwa vile tumeokolewa sote kwa kafara ya Yesu, tu ndugu na dada wa Baba mmoja wa mbinguni.

Makanisa mengi yamesababisha madhara makubwa kwa kuhitaji washiriki wao kuamini jinsi viongozi hufunza haswa! Makanisa hayo ni kama viwanda ambavyo huunda viatu vya namna moja. Maoni yanaweza kuwa yasiyo sawa. Lakini katu

upendo haukosei, kwa hivyo sharti tufahamu tofauti baina ya umoja wa maoni na umoja ya moyo. Ni umoja wa mioyo ambao kristo anaomba.

Kadri Bwana anavyohitimisha ombi lake anasema, Baba mwenye haki..... nimekujulisha kwao, na nitazidi kukujulisha kwao ili kwamba upendo wako kwangu uwe ndani yao nami niwe ndani yao. Ni madhumuni ya Yesu kuwa na mbingu ulimwenguni yakidhihirishwa katika maneno na matendo ya wafuasi wake.

14: Yesu Akiwa Gethsemane

Mfalme mkuu kwa huzuni mwingi anaondoka Yerusalem, anavuka kijito cha Kedron na kundi dogo la marafiki, huku akilengwalengwa na machozi anapanda mlima wa mizaituni. Nyuma yake anaiacha nchi yake iliyomgeuka. Mmoja wa waliowake aliyemsaliti amesalia kule jijini.

Kisa hiki kinapatikana katika II Samweli 15-18. ni kuhusu mfalme aliyesalitiwa na Absolumu miaka elfu moja baadaye mwana wa Daudi mfalme Yesu aliyesalitiwa na Yudas Iskariota, anaondoka Yerusalem na mitume wake na kupanda mlima wa mizeituni.

Alipofika bustani ya Gethsemane, Yesu aliandamana na Petro, Yakobo na Yohana na akaanza kusononeka na kuhuzunika, "Roho yangu imezidiwa na huzuni kiasi cha kufa. Aliwaambia (Mariko 14:33-34)

Kwa nini huyu mtu amesononeka? Ni kwa sababu amejitolea kubeba dhambi za ulimwengu wote na kilipa gharama yake ambayo ni kutengwa kutoka kwa Mungu baba. Bibilia yasema 'Mungu almtia dhambi yeye asiye na dhambi kwa sababu yetu (II Wakorintho 5:21)

Hakuna uamuzi mkuu uliowahi kufanywa au utakaowahi kufanywa kuliko uamuzi alioufanya Yesu kule Gethsemane. Gethsemani Yesu alithibitisha uamuzi wake wa kuchukua mahali petu na kufa kwetu ili tuishi milele. Angeenda msalabani alikokufa kifo cha pili kwa ajili yetu. Kifo ambacho kingekuwa cha mwisho na kikamilivu bila tumaini la kuishi baadaye. Ndio maana ulikuwa uamuzi mgumu kufanya ndipoza akasononeka.

Mungu alichukia dhambi kwa sababu ya madhara isababishayo kwa watu, familia, na taifa, ndiposa akafanya mpango wa kuiangamiza. Lakini dhambi haishi nje ya watu. Ni

uasi dhidi ya sheria za Mungu inavyosonekana katika mauaji, uzinzi wizi na udanganyifu n.k

Kwa sababu dhambi huishi ndani ya watu tu, Mungu ataiangamiza tu kwa watu. Kuna njia mbili ambazo kwazo ataiangamiza. Anaweza kuamisha dhambi kutoka kwetu kwenda kwake n kuijangamiza, kwanihaba yetu au kuiangamiza kwa kutwangamiza. Kwa sababu yeye ni Mungu wa upendo alichagua kuangamizwa kwaniahaba yetu. Alilipa deni lote la dhambi zetu msalabani kwanihaba yetu. Mungu anadhihirisha upendo wake kwetu katika hili. 'Tulipokuwa wenye dhnambi Yesu alitufilia (Warumi 5:8)

Watu wengine hata hivyo wanazipenda dhambi zao, hawazisalimishi kwa Yesu ili alipe gharama kwa ajili yao katika hukumu ya mwisho. Watalipa gharama ya dhambi zao. Ni kwamba Yesu afe ka dhambi zetu au tufe kwanzo. Hakuna uchaguzi mwingine.

Ikiwa tutaangamizwa kwa hukumu ya mwisho, ni kwa sababu tulikataa gharama ya Mungu ya bure ya Uzima kuititia kwa Yesu Kristo. Itakuwa kwa sababu tulipenda dhambi zetu kuliko tulivyompenda Yesu. Dhambi kuu kuliko zote ni kumkataa Yesu aliyekabiliana na kifo cha pili cha utengano wa milele na Mungu kwa ajili yetu.

Ni katika bustani ya Gethsemane ambako Yesu alipaswa kuchagua kama atakufa mauti ya pili kwanihaba yetu au tufe wenyewe.

Muumba wa dunia alikuwa kwenye njia panda juu ya hilo kiasi kwamba alitokwa na jasho la damu. Na ilimbidi Mungu kumtuma malaika ili amtie nguvu (Luka 22:41-44)

Tunapokuwa kwenye maumivu, Mungu anakusudia tumwendee kwa maombi alivyofanya Yesu. Pale bustanini, Yesu alimtaja baba kwa neno ambalo wayahudi hawajawahi kulitumia kwa mtawala wa dunia- Abba, limanishalo 'baba'

(Mariko 14:36). Mungu wetu ni baba wa upendo anahisi maumivu yetu. Anakumbuka kwamba tumeundwa kwa mavumbi kama baba ahurumiavyo wanawe, ndivyo Bwana ahurumiavyo wanaomheshimu hatutagundua amani katikati ya matatizo hadi tutakapomjua Mungu kwa Baba.

Katika Matayo 26:39, tunasoma, aliposogea mbele alianguka kifudi fudi na kuomba. Hata tukazama ndani ya shida, kumbuka Yesu alisonga mbele kidogo. Hata machungu yazidi kumbuka kwamba Yesu alipitia zaidi. Miguu yake imekanyaga kila miiba inayotutisha. Bibilia inaposema, Yesu alizidiwa na huzuni zetu kiasi cha kufa (Matayo 26:38), hebu tukumbuke kwamba alijua anapitia uchungu wa wapotevu na kutenganishwa na Mungu milele. Hii ndio ajabu isuluhihayo maajabu yote. Punde tu tutakapogundua machungu ya Mungu mtu, tuna funguo za wokovu wetu. Mara tu tutaelewa sababu ya giza lake, giza letu linatoweka.

Huku Gethsamane na kalwari inaunda kitu kibaya ambacho dunia imewahi kuona(mtu kumuua muumbaji wake), vile vile ni kitu bora zaidi ulimwengu kuwahi kushuhudia (muumbaji akitoa maisha yake bure kwa mwanadamu ili aishi milele katika ulimwengu usio na dhambi).

Gethsemane na kalwari zatwambia kwamba kuwa katika maumivu hakumaanishi tuko peke yetu. Kilio cha Yesu msalabani Mungu wangu, Munga wangu mbona umeniacha? Kinatuhakikishia kwamba, tunaweza kujihisi upweke wakati hatujaachwa. Yesu alipokufa alichukuwa kule kuachwa na Mungu kwa ajili yetu. Lilosalia ni Mungu kutupenda.

Je, umewahi gundua kwamba laana zilizotolewa kwa Adamu kwa dhambi zake Edeni zilimwangukia Yesu? Alipokosa Adamu, aliambiwa, ‘kwa jasho lako utafanya kazi na ardhi itakuota miiba na michongoma. Katika Gethsemane,

Yesu atokwa jasho la damu na kabla ya kusulubiwa anavishwa taji ya miiba kichwani mwake.

Adamu alipfanya dhambi alikuwa uchi machoni pa Mungu na Roho wa Mungu maishani mwake Yesu alipoangikwa alitundikwa msalabani uchi wa mnyama. Adamu alipofanya dhambi, alifukuzwa machoni pa Mungu. Yesu alipochukua dhambi zetu mabegani mwake, alikataliwa na Mungu.

Hebu, na turejee Gethsemane Yesu aomba, baba yangu, ikiwa ni mapenzi yako, kikombe hiki kiniondokee. Sio kwa mapenzi yangu bali kama upendavyo wewe (Matayo 26:39). Kikombe kibebacho dhambi za ulimwengu kilishapitishwa kwa Yesu ili akinywee na ni lazima achague kukinywea au la. Ikiwa angekataa, basi kila mmoja wetu angekinywea kikombe chake mwenyewe. Hatimaye anaomba “kama haiwezekani kikombe hiki kinipite hadi nitakapokinywe mapenzi yako yatimie” (Matayo 26:42). Yesu alichagua kukinywea kwa ajili yetu.

Uchungu wa Yesu bustanini ulimwandaa kwa uchungu wa msalaba Gethsemane palikuwa ni mahili.

Pa uamuzi, kalwari ni mahali pa kitendo. Yudasi pamoja na Yesu wote walifanya maamuzi ya mwisho bustanini. Yesu aliamua kuwa upande wetu huku Yudasi akiwa dhidi ya Yesu. Binadamu aliangamizwa kule bustanini vile vile wamuzi wa kumkomboa ulifanyika bustanini.

Kristo akiwa anaomba bustanini, askari wa kirumi na maafisa wa hekalu wanafika na kumtia nguvuni (Yohana 18:2-3). Wanaongozwa pale na Yudasi, ‘mwana wa upotevu’ (Yohana 17:12). Wanapokaribia, Yesu anasogea karibu na kuuliza, ‘ni nani mnayemtafuta?’

‘Yesu mnazareti, walijibu’ wakati Yesu alijibu, ‘mimi ndiye’ askari walindi nyuma wakaanguka chini.

Yesu alidhihirisha mamlaka yake juu ya adui zake ili kuwaonyesha kwamba alishikilia ushukani na chochote

wangefaulu kufanya ni kwa idhini yake. Wale waliokuja Gethsemane kumshika Yesu waliongozwa na Yudasi, mmoja wa wanafunzi wa Yesu. Yudasi mwanafunzi aliyebarikiwa na talanta alikuwa mweka hazina. Kwa bahati mbaya alikuwa akiiba pesa kutoka kwenye hazina kwa ajili yake. Yudasi hakujisalimisha kikamilivu kwa Yesu. Na Yesu alipomkemea kwa tama yake, aliamua kulipiza kisasi kwa kumsaliti kwa mamlaka ya wayahudi (Yohana 12:3-7); Mariko 14:7-10)

Hii inaashiria mateso makuu. Jamii ya pekee ya wakristo, itagawanyiza kama Israeli ya siku za Yesu, kwa mpangilio wa kidini, na wafuasi wao na waumini wachache ambao wamejitolea kikamilivu kwa Yesu. Aliyechaguliwa kama Yudasi mwana wa uasi. (Yohana 17:12; II Wathesalonike 2:3), watawasaliti waumini kama wayahudi na watu wa mataifa walivyounagna kumwagamiza Kristo, ndivyo kanisa na serikali zitaungana kuwaangamiza wafuasi waaminifu wa Yesu. (Ufunuo 13:15).

Kusalitiwa na rafiki ni jambo lisilofikirika lakini kusalitiwa na busu la rafiki! Busu ni ishara ya uaminifu na upendo. Na ndivyo itapokuwa mwisho wa wakati. Mpanga Kristo ataahidi uaminifu kwa wafuasi wa Yesu ili kuwaangamiza. Wasifu hupendwa kwa sababu nyingi, mojawapo ni huzuni, majoribu, ushindi, na kukatishwa tamaa. Zinaonyesha huzuni zetu, majoribu yote na kukatishwa tama kwetu. Kwanguka kwa Yudasi kwapaswa kutukumbusha tulivyomsaliti Yesu kwa mara nyingi na pengine kwa vipande vichache kuliko vipande thelathini nya fedha.

Pengine kama tungetaja dhambi zetu kwa jina tungeliziacha.

‘Unafanya ni Yudasi?’

‘Nimekuja kukusaliti Bwana?’

‘Unafanya nini Julia?’

‘Ninadanganya Bwana?’

‘Jack, Unafanya nini?’

‘Ninaiba Bwana!’

‘Mariko, unafanya nini?’

‘Ninazini Bwana.’

Kama tungenesema ukweli kuhusu dhambi zetu, tungeliona ndani ya Yudasi sio tu ubaya wetu bali pia uwezo wetu wa kukataa Mungu mwenyewe. Uwezo huu unaitwa uhuru. Mungu alitufanya kuwa huru lakini uhuru una uwajibikaji. Watu walio huru wanaweza kufanya mazuri au mabaya sana.

Mungu ni muungwana awezi kutulazimisha kumfuata. Kumbuka yale kijana kiongozi tajiri (Mariko 10:17-23). Aliondoka kwa Kristo akiwa na huzuni na Kristo alimwacha akaenda. Hakumkimbilia amshike mkono amwambie, tazama, hebu nikweleze vizuri. Hiyo inatisha. Ina maana kuwa inabidi niwe chonjo kila wakati ikiwa ninaupuza uhuru huo.

Tazama wale askari walioangushwa chini baada ya Kristo kutangaza uhuru wake. Je, walikimbia? La hasa. Wala hawakujifunza kutoka kwa kuponywa kwa sikio la malika (Luka 22:49-51) waliendelea katika uovu wao. Na ndivyo ilivyo kwako na kwangu- mara nydingi.

Tunasoma kwamba hawa watu walifunga mikono ya Yesu. Nasi pia tuna hatia ya kufanya hivyo. Kama maisha yanatufanya kuhangaika mpaka tukose muda na Kristo, tunafunga mikono yake. Kama sisi wenyewe hatuna muda wa watoto wetu na tunategemea kuwaokoa, tunafunga mikono yake. Kama hatutaishi upendo, tutakuwa tunafanya vivyo hivyo. Tunafanana wale askari waliomfunga mikono yake.

Baada ya Yesu kushikwa, alipelekwa kwa nyumba ya kuhani mkuu ili ajaribiwe. Wanafunzi wote wakapa kuwa wangeshikwa, walikimbia. Baadaye kidogo, Yohana na Petro walimfuata kwa umbali. Nyumbani kwa kuhani mkuu waliruhusiwa kuingia katika kisimba cha ndani.

Petro aliingia mle, ambapo palikuwa mahali wazi palikojengwa na mawe pakizungukwa na pembe nne za nyumba ya ghorofa. Ilikuwa ni usiku wa baridi na moto ulikuwa umewashwa katikati. Petro alisogea karibu na moto ili apate joto. Yule msichana aliyejkuwa kwenye zamu langoni alimwona Petro na akapita kando yake. Alimchunguza kwa ukaribu na kusema, 'Ulikuwa pamoja na yule mnazareti Yesu.'

Shetani ni mganga hawesi kukuvamia kwa namna tunayotegemea. Petro angeliletwa kwa kayafa kwa sababu ya imani yake kwa Yesu, angelikufa badala ya kumkataa Bwana wake. Katika wakati huu hata hivyo, muuliza swali alikuwa ni mwanamke wa umri wa makamu. Alikuwa msumbu kama nzi na Petro alijaribu kumnyamazisha kwa kukana. Lakini kukataa huko kulikuwa ni kudogo tu na shetani angeendelea kusukuma Petro mpaka amtenge na Yesu.

Petro, ili kujiepusha na maswali, aliondoka akakaa karibu na mlango wa kuingilia ndani, yule msichana mtumishi alipomwona, aliwaambia waliosimama pale, huyu jamaa alikuwa pamoja nao kwa kuwa alikuwa amemkataa Yesu kwa mara ya kwanza, ingekuwa aibu kwake sasa kukubali kwamba alikuwa mwanafunzi wa Yesu kwa hivyo alikataa tena mara ya pili. Walawi pale wakishangilia kushikwa kwa Yesu, walimwangalia Petro, tunaweza kujua kupitia lafudhi yako yakwamba wewe ni mgalilaya, kwa hiyo lazima uwe mmoja wao. Mara hii Petro anahaba kwa kula kiapo ya kwamba hamjiu Yesu.

Papo hapo jogoo linawika mara mbili. Ndipo Petro akakumbuka neno la Yesu alilomwambia! Kabla jogoo haijawika mara mbil, utakuwa umenikana mara tatu. Kwa wakati huo, Yesu anageuka kutoka katika chumba cha juu na kumwangalia Petro. Ni mwonekano wa kufa moyo, mtazamo wa upendo na mtazamo wa msamaha. Kule kuangalia

kunamvunja moyo wake. Akilia kwa uchungu, anaondoka kwa haraka kama kipofu kutoka kwa ile nyumba (Mariko 14:66-72). Pale nje, akiwa pekee na Mungu, Petro anazaliwa tena. Mapema Yesu alikuwa amemwambia, Petro utakapoongoka uwatie wenzako nguvu. Kwa hiyo Mungu alikuwa ameona yote kwa umbali na alikuwa amemsamehe na humrejesha mapema. Ni upendo ulioje!

Hivi sasa aina ya visa ambavyo wakristo wangebuni kisa hiki kina pete ya ukweli. Ni matukio machache tu yaliyorekodiwa katika injili zote nne na hili ni mojawapo kukataa kwa Petro kuhusu uhusiano wake na Yesu, kulikuwa muhimu sana kiasi cha Yohana kutaja, akijua kwamba waandishi wa kwanza watatu wa injili walikuwa wamelizungumzia hili.

Kila andiko la maelezo haya ni la usanii. Maandiko machache yanaweza kuwa na umaana wa kushangaza kwa nini Petro ageuka na kumfuata Yesu mpaka kwa nyumba ya kuhani mkuu? Alifanya hivyo kwa maringo.

Mapema alikuwa amejivuna kuwa hata wanafunzi wengine wamwacha Yesu, ye ye asingethubutu (Mariko 14:29-31). Angewambiaje wenzake kama naye angetoroka?

Kisa hicho ndicho kisa chetu majaribuni sasa kama ilivyokuwa kule nyumbani mwa kuhani mkuu. Hiki si kitu kilichopita. Iko mpaka leo! Kazi Yesu majaribuni leo na tunaweza kumkana Yesu kama aivyofanya Petro twaweza kujifanya kuwa sisi si wafuasi wa Yesu, lakini lazima tukumbuke siku zote yakwamba kila neno bayu au kitendo kinazidishika na kuwa mlima mkuu.

Kama vile shimo moja laweza kuzamisha meli, ndivyo dhambi yaweza kumpeleka chini mdhambi. Mahali salama pekee ni kuishi karibu na Yesu. Historia inatwambia kwamba popote Petro alipokuwa akihubiri katika miaka ya baadaye, na punde jogoo likawika, angeacha kuhubiri alipoanza tena,

kulikuwa na uungwana, upole uliomzunguka kiasi kila mtu kwenye mkuutano alisisimuka naye.

Yesu alimrejesha Petro aliyeanguka na kumtumia kutangaza habari njema kuhusu kifo na ufufuo kwa watu wa mataifa kule pentekote. Petro alikuwa muhubiri matata wa Bwana mpaka yeche, sawa na Bwana wake alisulubishwa kwa imani yake.

Kuna aina mbili ya udanganyifu dhidi ya mfalme wa Mungu, moja ni kujifanya kwamba wewe si mfuasi wa Yesu huku ukiwa mmoja wao. Yudasi alikuwa msaliti wa kwanza wa aina hiyo, na Petro akawa wa pili. Yudasi alipanga kumsaliti Yesu, ila Petro alijikwaa. Yudasi hakujitoa kwa Yesu ila petro alijitoa.

Petro aliamini kuwa angempigania Yesu kupitia upanga wake, lakini adui wake, alikwepa na badala ya kumkata kichwa chake, alikata sikio lake. Pindi kanisa lianzalo kupigania au kupeleka ufalme wa Mungu kwa upanga huwa limepoteza mlengo.

Bila kumkosea Petro, sababu iliyofanya upanga wake usichukue maisha ya mtu mwingine ni kwamba hakuna mtu aliyewahi kufa mbele ya Yesu anayeishi. Alivunja kila mazishi aliyohudhuria na ndiye wa kwanza kufa katika watatu waliosulubishwa.

Lakini Kristo ana uwezo wa kuondoa makosa yetu. Ana uwezo wa kurejesha uzima kutoka kwa mauti, ushindi kutoka kwa kushindwa na mafanikio kutoka kwa kutokufanikiwa. Unipokuwa shindani usikimbie kukatakata masikio ya watu. Ukiyanya hivyo utakuwa unauzuia mpango wa Mungu. Yesu alimwamuru Petro, ‘weka upanga wako mbali! Kwani siwezi kukinywea kikombe nilichopewa na baba yangu? (Yohana 18:11). Yesu anahitaji kuingilia kwetu, anahitajik kutii kwetu kwa na kwa mipango yake.

Tunamwona Bwana akijitoa kafara kule Gethsamane anajisalimisha kushikwa anatoa mikono yake afungwe na tumsikia akinongona msalabani ‘sikujokoa, ili nikuokoe wewe. Sikutoa uso kutoka kwenye aibu na kutemewa mate, ili uso wako ungae kama jua. Niliubeba msalaba ili siku moja, wewe uibebe fimbo ya utawala. Nilivaa taji ya miiba ili wewe uweze kuvaataji ya utukufu. Nilininginia kwa uchungu ili wewe ukae kwa ushindi. Nilikwenda chini ya vina wewe upae kwenye angaza mbingu.

Kama upendo wa Yesu hautatubadilisha kwa wema, mioyo yetu basi imepitwa na wokovu.

Hatupaswi kukisia kwamba Kristo alishikwa na kusulubiwa na askari wa kirumi, walinzi wa hekalu, Yudasi kuyafa na anasi. Au na pontio Pilato. Hapana ni sheria iliyomchukua Kristo na ni hukumu na haki ya Mungu iliyokuja kumtafuta, kuwa alikuwa mmoja aliyyeteuliwa kuchukua nafasi ya wadhambi kila kitu kilichomtendekea Kristo ndicho kinapaswa kumtendekea mwenye dhambi.

Tunastahili kufungwa, kutemewa mate, kufutwa na kusulubishwa. Lakini kwa sababu Yesu aliyechukua mauti yangu, mnao uzima wa milele ikiwa nitaweka imani yangu kwake. Kwa sababu alichukua aibu yangu ninao utukufu. Kwa sababu alichukua hatia yangu ninayo haki yake.

15: Yesu Ajaribiwa

Wakati ANASI alimuliza Yesu kuhusu mafunzo yake Yesu alimjibu kwamba aliwahi kuyazungumzia waziwazi katika sinagogi na hekaluni, ambapo Wayahudi wote walikuwa wakijumuika, hakuwahi kusema lolote kwa siri. Mashahindi wake walikuwawatu wa pale, hivyo anasi akawwafulize.

Kila neon lisemwalo kwa siri lina shaka na dhambi kinaya Bwana weyu alikuwa kama mwanga wa jua. Na kila mfuasi wa Yesu yafaa awe wazi kama mwangaza wa jua.

Askari alipomzaba Yesu kofi kwa namna alivyomjibu Anasi. Yesu alijibu akisema iwapo nilikosea kusema vile niambie ni lipi. Lakini kama nilisema ukweli mbona uknipiga? Yesu hakutishwa. Kuwa mkristo si kuwa zulia la mlangoni. Ni kusimama wima kama mwamba kwa kilicho haki.

Insaikitisha tunapoona jinsi hii mahakama ilivyoweka mfano zingine zilizifuata baadaye. Miaka elfu mbili baadaye mashirika ya kidini yaliyokataa ukweli injili waliwatesa walioikubali. Kwa sababu, ukweli huo wa injili ilihitilafiana na tamaduniza binadamu zilizozozana na injili. Injili ikadhalihishwa ili tamaduni za wanadamu zisalie.

Kasha yesu akapelekwa kw akayafa, kuhani mkuu alyekuwa msimamizi wa maswala yote ya dini. Bwana huyu mwenye mamalaka makuu alisheheni kiburi. Takribani kuhani elfu ishiriniwalimtumikia na Isreali yote ilimheshimu kama sauti ya Mungu. Je kwa nini alishikilia kazi yake? Lilikuwa jukumu lake kuhifadhi tamaduni za dini kwa gharama yoyote. Lakini wakati bamaduni za watu huhutifafana na Amri za mungu watu wema hukwazwa.

Kastika matayo 23, Yesu alimramia kayafa na uongozi wake fisadi kwa wadau yasiyo haki tamaduni zao, fedha mtizamo wao wa kimshauri na udini wao ulikuwa mvutano wa

ana kwa ana. Sasa lazima taasisis zilizazohasi zile au Kristo aje kayafaalikuwa na jibu tayari. Akasema nyie ni wapumbaovu iwapo hamtagundua kwamba heri kutoa kafara ya mtu mmoja kuliko uyahudi (Yohana 11:40-50).

Lakini Yesu awageuza vibao anawambia kwamba saa itakuja wakti hapatakuwa hukumu,. Yaani chochote wnachofanya yafaa wapeze jicho moja lowa kwa litakulokuja.

Yesu alijaribiwa mbele ya nleao saba mwanzo na Anasi iliyofuata; kasha mbele ya Pilato, Herode na kasha tena kwa Pilato. Wayahudi walimshtaki Yesu kwa makosa saba. Kwamba alitishia kubomoa hekalu alikuwa mahalifi, alikuwa anapindua itikadi za taifa, kwamba alisema ni makosa warumi kutoza kadi aliwachanganya watu, na kudai ni mfalme, na kwamba alisema ni makosa warumi kutoza kodi, aliwachanganya watu, na kujidai ni mfalme na kwamba aldai kuwa mwana wa Mungu.

Kadhalika watu saba walitoa ushaahidi wa ukamilifu wa Yesu. Na jaribio lake kuu mbele ya Pilato lilikuwa na sehemu saba ambapo Yesu alingia na kutoka kwenye kikao cha Pilato. Injili ya Yohana inadhirisha kuwa Pilato alimuuliza Yesu maswali saba na injili zote nne zinaonyesha Pilato akisema mara saba kwamba haoni kosa kwa KRISTO Yesu aliteswa kwa adhabu saba zisizo haki walicharaza usoni, kumpiga ngumi, walinzi walimpa kipigo kama ada, wakamcharaza, kumtemea mate, kumpiga mara kadha kichwani kwa kifaa na wakasulubisha. Yesu aliyesulubiwa alikuwa na majerajh a saba na aliangikwa kwa muda wa masaa saba; sita msalabani nay a saba ikiwa muda wake wamapumziko aliposhushwa chini. Msalabani, Yesu alinena mara saba, na kuna matamshi saba yaliyosemwa kwa Yesu aliponninginia msalabani.

Si sadfa kwa saba kujirudiarudia . neon la Kihiberania sheba laweza kutafsiriwa kama 'saba' au ago'(tazama Mwanzo 21:27-

31) Mungu alifanya agano kwamba angetukoa kutoka dhambini na kuwa iwapo tungeukabali wokovu tungekuwa watu wake. Juu msalabani Yesu alimwaga damu yake kwa ajili ya wokovu wetu. Alikuwa damu ya agano ambayo ingemwagwa juu ya wengi kwa msamaha wa dhambi (matayo 26:28). Tunapoinywa damu tunaonyesha kuwa tunamkubali Yesu kama Mwokozi.

Saba zote fiche zilizoangaziwa hapa juu ni muhuri wa Mungu kwa agno hili la ahadi- kwamba Yesu ndiye tu atkayetimiza sehemu ya Mungu ya agano ili kutuokoa.

16: Yesu Mbele Ya Kayafa

Kikao kati ya Yesu na Kayafa ndicho kilikuwa kikao cha wakati wa kiroho zaidi ambacho ulimwengu haujawahi kuona. Kristo, mwana wa Mungu, mbele ya kayafa, mkuu wa dini. Dini ya Mungu ilikuwa imedumu duniani kwa zaidi ya millennia moja, lakini sasa ilikuwa inarudi kuwa mbegu. Ilikuwa imefanywa rasmi na ilikuwa imechangamana na chachu ya utamaduni. Yesu alaitaji kuwa kaburi lililo wazi, mahame ya hekalu ambalo alikuwa ameliacha. (mat 23:38). Makuhani badala ya kuwachunga watu walikuwa wakiwadhulumu. Kayafa akiwa na hasira za mashtaka ya Yesu, aliamua kijiondolea mwiba huu, lazima Yesu afe.

Kulikuwa na shida moja hata hivyo wayahudi hawakuwa na mamlaka ya kumua mtu. Hiyo ilikuwa ni haki ya warumi waliokuwa mamlakani. Shida ni kwamba wayahudi hawakuwa na mashitaka ya kutosha kupeleka mbele ya pontio Pilato. Hawakumpata shahidi yeyote aliyekubali. Ilionekana kwamba mashtaka ya Yesu yangesambaratika. Na hapa Kristo alikuwa amesimama mbele zao kana kwamba anawahukumu. Hapo ndipo kuhani mkuu alipandwa na hasira na kuuliza, ‘twambie, ni kweli kuwa wewe ni mwana wa Mungu?’ kwa kujibu, yesu aliwaambia kwamba atakuja kwao baadaye kama hakimu wao; atakuja kulainisha maovu yote.

Usihofu kisimama na wachache wampendao na kumtumikia Yesu. Usiogope umati unaodai kwamba wewe umekosea. Ukitimama na Yesu naye asimame nawe, utasema saa inakuja ambapo vibao vitageuzwa wakati wa kwanza watakuwa wa mwisho na wa mwisho watakuwa wa kwanza.

Ni mda mfupi baadaye ulimwengu ulitetemeka chini ya miguu ya Kayafa na wafuasi wake, na kufungu makaburi na wafu kufufuka (mat 27:50-63). Jua halikutoa mwanga na

kitambaa cha hekalu kupasuka kuwili kikifungua njia ya kwenda kwenye uwepo wa Mungu. Yote haya yaliashiria wakati Yesu atakaporudi kwetu kama hakimu. Siku hiyo makaburi yatafunguka tena (Yohana 5:28-29).siku hiyo juu litageuka giza (Ufunuo 6:12) kisha Mungu atajifunua kwa wote (Ufunuo 6:16-17)

Yesu anakuja kwa kuhukumu, atawahuku watu binafsi ya kidini, mashirika, makundi mataifa na miungano ulimwengu wote. Kunayo njia moja ya kuponyoka hukumu, nayo ni kusalimisha dhambi zetu kwake aliyekufa kwazo msalabani. Watakaofanya hivyo, watatazamia kuja kwake kwa furaha kubwa (II Tim 2:8, Yohana 2:28) Wasiofanya hivyo watajawa na hofu ajapo 9Uf 1:7,6:12-17) wataangamizwa kwa dhambi zao.

Kayafa aliamua kwamba ikiwa angeokoa kanisa, basi Yesu angekufa. Ila Yesu alikuja kuokoa kanisa. Tungesimama upanda gani tungelikuwepo siku hiyo? Je tungelisimama na kayafa ili kutetea kanisa na michafuko ya tamaduni zao? Au tungesimama na Yesu na neno la Mungu? Lazima twendelee kuchagua baina ya Kristo na kanisa. Kati ya kilicho maarufu au kilicho kweli. Baina ya kilicho kibaya au kilicho kizuri.

Daktari Arthur Beltz alisema, hamna haja kumsulubisha Kristo ili kuokoa taasisi. Isipokuwa Yesu aishi taasisi imekufa tayari.

Hatma yetu inategemea yale tunayotenda na Yesu. Tunachagua Jehanamu au Mbingu. Kristo anapotukabili kwa kweli na madai yake, tunachagua hatma yetu halisi.

Yudasi alichagua kusimama na Kayafa lakini baadaye aligundua kwamba uamuzi wa kumkana Yesu ulikuwa mbaya. Alirudisha fedha alizopokea kutoka kwa makuhani wakuu na wazee na kukili kwamba amesaliti damu isiyo na hatia (Mat 27:3-5).

Kuna Yudasi wengi kanisani leo. Watu wapokea mapato kutoka kwa makundi ya kidini huku wakimsaliti Yesu na injili yake. badala ya kusimama kwa imani na Yesu ambaye amehahidi kukidhi mahitaji yao (matayo 6:25-34), wanasimama na wale wanaowapatia usalama wa kiuchumi duniani. Uamuzi ni wetu. Imani kwa Yesu au pesa mkononi.

Wale wachaguao fedha mkononi badala ya imani kwa ulinzi wa Yesu kwao, watajuta siku moja kwa kutokuwa na imani na maono mafupi, na nia, kama Yudasi, wakiri kosa lao lakini watakuwa wamechelewa si dhambi zao zitakaowangamiza ila kukosa kwao kusimama na Yesu.

Dhambi huonekana nzuri na ya kuvutia kabla ya kuinamia lakini tufanyapo dhambi, utukufu unatoweke. Kabla ya kufanya dhambi tendo la dhambi linaonekana dogo, na hiyo dhambi inakuwa kama mlima.

Shetani hututongoza na ahadi zilizo tupu na baadaye uzito wa hatia yetu unatosha kutufanya tujisalimishe. Dhambi haiwezi kutoa kile inachoahidi mtego wake huwa na ndoano mbaya juu yake.

Tazama makuhani walivyomuitikia Yudasi alipokuwa akitubu. Hiyo ni nini kwetu? Walimaka. Huo ni wajibu wako (Mat 27:4) kama kaini aliyemuua kakaye, hawakukubali kuwajibika kuwa mlinzi wa kaka yao. Ni rahisi kujua kama tu wa Yesu au shetani kwa kutazama jinsi tumtendeavyo kaka yetu. Kama tutabeba mizigo ya kaka zetu na dada zetu, tu wa Yesu. Kama tujijali sisi wenyewe na wala si kaka zetu na dada zetu wahitaji, tu wa shetani.

Kunaye mmoja ambaye kwa kweli anatujali anatwalika njooni kwangu nyinyi msumbukao na mizigo, nami nitawapa pumziko (Mat 11:28)

17: Yesu Mbele Ya Pilato

Tumemwona Yesu akihukumiwa mbele ya mamlaka ya kidini. Sasa tutamwona akihukumiwa mbele ya mamlaka ya Kisiasa.

Viongozi wakuu wa Israeli walimharakisha Yesu. Kwenda mbele za pontio Pilato, Gavana wa Kirumi wa Palestina. Pilato alikuwa amekuja kutoka katika makazi yake yaliyoko katika mji wa pembedi mwa bahari ya kaisaria maritima mara nyingi hakupenda kupanda Yesasalemu maana hapakumvuta. Yeye alipenda jamii ya mwonekano na msisimuko. Pindi alipokuja alikaa ikuluni mwa Herode. Huko ndiko alikopelekwa Yesu.

Lakini wayahudi hawataingia katika nyumba ya mtu ambaye si myahudi kabla ya tambiko kwa hofu ya kuliwa najisi kwa maana najisi hiyo ingewazuia kutiunza pasaka. Wakiwa na Yesu aliyefungwa, walifika katika mtaa mkuu wenyewe bustani nyingi, njia bana ya kutoka, na viziwa vidogo viliozungukwa na mitu ya yakupendeza. Baada ya kavu kisimba cha inje, walimshauri mmoja wa askari wa mlangoni, kuwa walikuwa wamekuja kumwona pilato ili waweze kupeana mafungwa Yesu kwao. Lakini wao wasingeweza kuingia wenywewe.

Hawa viongozi wa kiyaudi hawakuelewa kuwa kwa kumtua Yesu kwa wasioamini, wao kama taifa walikuwa wanamkataa masihi wao na kuwaachia watu wa mataifa.

Kwa hivyo Pilato anaamshwa saa kumi na mbili ya asubuhu, kitu ambacho hakuifurahia kwake Pilato, kukutana na wayahudi ndio mojawapo ya vitu ambavyo vilimkera katika kazi yake. Aliwachukia wayahudi na wayahudi walimchukia.

Pilato alitoka nje kukutana na msafara wa waliomleta Yesu na akauliza, ni mashitaka yapi mliyo nayo dhidi ya huyu mtu?

Walilikwepa swalii kwa kujibu, asingalikuwa jambazi, tusingalimleta kwako.

Akiomba kujua kile wanachotaka, pilato aliwajibu, mchukueni nyinyi wenyewe mkamhukumu nyinyi wenyewe sawa sawa na sheria yenu. Lakini hatuna haki ya kuua yejote wakajibu wayahudi.

Adhabu ya wayahudi ilikuwa ni kumpiga mtu mawe mpaka afe. Yesu, hata hivyo, alikuwa ametabiri kuwa angekufa kwa kusulubiwa (Luka 24:6-8) adhabu ambayo ingemchukua kuvumilia kule kupondwa kwa roho, ambayo ni gharama alikuwa alipe kwa ajili ya dhambi zetu.

Pilato aliwaagiza askari wake wamletee Yule mfungwa Yesu akisimama mbele yake alimuuliza wewe ndiye mfalme wa wayahudi? (Yohana 18:33).

Pilato alijua vyema hitaji la wayahudi la kuwa huru kutoka Rumi wakiwa na mfalme wao anayewatawala na hilo lilimtia hofu.

Yesu akiri ya kuwa yuna hatia ya shtaka hilo ila kwa namna ambayo anakaa kama asiyé na hatia. Hiyo inawezekanaje? Kwa maana ufalme wake si wa dunia hii. Kwa kuwa ungekuwa wa dunia hii, watumishi wake wangemptetea kwa vita. Ufalme wa Kristo ni wa Kiroho katika mioyo ya watu, ufalme ambao siku moja utakua na wenyeji wake kutoka katika kila taifa la sayari hii.

Naam, Yesu alikuwa mfalme wa wafalme na Bwana wa Mbwana.

Pilato alikuja kuelewa baadaye kuwa wayahudi walisalimisha Yesu kwake, si kwa sababu Yesu alitenda lolote baya, lakini ni kwa sababu walimchukia (Mar 15:10). Mara kwa mara Pilato alitaka kumwachia Yesu huru (Luka 23: 20) inasema kuwa alitaka sana kufanya hivyo. (Yohana 19:12) yasema alitaka kumweka huru. (Matendo 3:13) inarekodi kwamba alikuwa ameamua kumwachia.

Pilato alikuwa na mamlaka ya kumwachia Yesu lakini gharama ya kufanya hivyo ilikuwa mbaya zaidi kuliko alivyokuwa tayari kulipa. Wayahudi walisha mwambia tena kwa uwazi ya kwamba asingemuua Yesu, watamshitaki huko Rumi. Pilato ambaye tayari hakuwa na rekodi nzuri, alijua kuwa wakifanya hivyo, angeipoteza nafasi ya cheo cha ugavana. Basi ilidhihirika wazi kwamba ni yeye au Yesu. Mmoja wao ilikuwa aondolewe, lakini alihakikisha kuwa batakuwa yeye. Hivyo alitoa amri Yesu asulubishwe.

18: Yesu Au Baranaba

Mashtaka yote dhidi ya Yesu yalikuwa si ya haki. Kila hakimu alikuwa ndiye kiongozi wa mashtaka, na hakuna shahidi aliyeruhusiwa kumtetea Yesu. Mashtaka ambayo kwayo uamuzi ulifikiwa kwamba Yesu asulubiwe yalifanywa usiku, ambayo ilikuwa kinyume cha sheria kawaida kwenye mashtaka ambayo pilato alikuwa hakimu, mushtakiwa aliruhusiwa kukubiliana na mashtaka yake, lakini kwa Yesu hilli halikufanyika.

Baada ya Pilato kupanda kitandani mwake ili ajue ni kwa nini makuhani wa kiyahudi wamekuja kwenye makazi yake masaa ya mapema kama hayo, mke wake aliota ndoto iliyomsumbu. Aliandika kijikaratasi na kumtumia Pilato kwa njia ya mtumishi. Pilato alikuwa ameketi kwenye kitu cha hakimu alipopatiwa hicho kijikaratasi. Alikifungua na kukisoma, 'Usifanye chocho dhidi ya huyu mtu asiyе na hatia maana nimeteseka moyoni leo katika ndoto kwa ajili yake.'

Ilikuwa ni nadra sana mwanake kutuma nakala ya ndoto yake kazini kwa mume wake, sana sana kama huyo mwanamume ni gavana au hakimu. Kawaida ndoto ilikuwa ya kipekee kutoka katika ndoto zingine. Alitazimishwa akizingatia uzito uzito wa ndoto yenyewe, kujaribu kumsimamisha mume wake asimhukumu mtu asiyе na hatia. Mungu alikuwa anatumia mbinu zote zipatikanazo kumwongoa Pilato kutohana na kufanya makosa makubwa katika fani yake.

Wakati Pilato alimuuliza Yesu ' kwani hutambui kuwa nina mamlaka ya kukuachia au kukusulubisha? 'Yesu alijibu Usingalikuwa na mamlaka juu yangu pasipo kupewa hayo mamlaka kutoka mbinguni' (Yohana 19:11).

Jibu la Yesu ni mkufu wa thamani unaoweza kutuletea amani katika kila shida. Mungu anatulinda vile ambavyo

alimlinda Yesu. Anaijua kila unywele uangukao kutoka kichwani mwetu (Mat 10:29-31) Hakuna litakalo tendeka pasipo yeye kuruhusu. Lazima tujifunze kusema juu ya kila shida, kila jaribu, kila kukatishwa tama.' Huna mamlaka juu yangu pasipo kupewa kutoka mbinguni.'

Basi Pilato bila kupenda alitoa kadi ya hukumu. Wezi watatu walioshtakiwa kufa, walikuwa wameshikwa wanasubiri kusulubishwa wafe (Mariko 15:7; Luka 23:19). Kiongozi wao ni mtu aliyeitwa Baraba, jina liliolomaanisha 'motto wa babaye.' Ilikuwa ni desturi ya sikukuu ya wayahudi kwamba Warumi wamwachie mfungwa aliyependekezwa na watu. Pilato alikuwa achague kutoka kwenye wafungwa wane wa kumwachia. Aliuja viongozi walihitaji Yesu asulubiwe, ila alikusudia kutumia msaada maarufu wa watu ili kuamua kumchagua Yesu.

"Je, mwataka niwafungulie kwenu mfalme wa wayahudi" Pilato aliuliza akijua kwamba ni kwa sababu ya chuki makuhani wakuu walimsalimishia Yesu kwake. Lakini makuhani wakuu walihamakisha watu ili kusukuma pilato awafungulie Baranaba badala ya Yesu.

"Nimfenyeje basi huyu mnayemwita mfalme wa wayahudi?"
Pilato akauliza

"Msulubishe" wakapaza sauti

"Kwa nini? Ni kosa gani amefanya?" aliuliza Pilato

"Lakini wakapaza sauti zaidi, msulubishe!"

Akitaka kuridhisha Umati Pilato alimwachia Baraba kwao. Alimwachia Yesu achapwe na kumtoa kwao asulubishwe. (Mariko 15:9-15).

Maamuzi yaliyofanywa pale yalifanywa kwa sababu watu walitekwa na msisimuko wa kibinadamu badala ya ukweli na haki. Umati uliwasikiza makuhani wakuu, huku Pilato akiusikiza umati. Hakuna aliyemsikiza Mungu.

Sisi pia tuna hatia ya kusikiza mamlaka ya kibinadamu badala ya Yesu, tusukumwapo mpaka mwisho. Asili ya tabia inafanuliwa tunapolazimishwa kufanya kitu Fulani Kibaya ili kujioskao.uamuzi tunaofanya wakati huo unaonyesha sisi ni akina nani.

Si kwa kitu chochote tunapoona kwa uwazi udhaifu wa asili ya mwanadamu na upotovu wake. Kuliko kwenye sauti kilio kinachopanda kikisema, 'si huyu mtu ila Barabba!' fikiria inachomaanisha. Fikiria kinachotwambia kuhusu miyo yetu. Katika kila Uamuzi, tunafanya uamuzi huu. Katika maneno tunayochagua kuyazungumza, huwa tunasimama kwa ajili ya shetani au kwa ajili ya Kristo. Katika mambo tunayofanya na matazamio tuyakumbatiayo, tunamchagua Barabba au Kristo. Hatuna wasiochagua kabisa au wafugufugu. 'Asiyekuwa nami; yesu alisema , yu kinyume changu'.

Mtazame Barabba akilala kule jelani akisubiri auwawe, anasikia bolti ikosogezwa na mlango wa chuma wa jela lake ukiachwa wazi. Lakini badala ya kuona atakayemuua, anaona mtu aliye na uso wa tabasamu akimwambia uko huru. Barabba akajibu 'usifanye mzaha na mimi unaongea matope. Basi anaambiwa, Yesu wa Nazareti anakwenda kufa msalabani kwa nihaba yako. Kwa hiyo toka hapa! Huko huru.

Hapa ndiko kuna kiini cha injili wewe na mimi ni barabba-wanawa baba wa ulimwengu tumehukumiwa kufa kwa sababu tumekataa Baba wa mbinguni. Lakini asiye na hatia amechagua kuchukua mahali petu na kufa kwa ajili yetu. Atateswa, ataumia, atavumilia ili tuwekwe huru. Kristo anakwenda msalabani uchi ili tuweze kuvishwa na vazi lake la haki lisilo na doa. Kristo anavishwa taji ya miiiba ili tuwe na taji ya utukufu. Mwili wake ulivunjwa ili wetu utukume .

Tuseme Barabba alikataa kuamini ujumbe kwamba sasa alikuwa huru. Tuseme alikazia kuendelea mpaka kwenye kifo

chake hata hivyo. Unaweza kufikiria kitu cha upumbavu kama hicho? Lakini upumbavu kama huu waonekana kila mahali. Mamillioni duniani wanakataa ya kwamba Yesu hakufa kwa ajili yao. Mamillioni wakataa uhuru wao na kukazia kuendelea mpaka kwenye kusulubishwa kwao, kitu ambacho kitakuwa na madhara ya milele. Hawataamini habari njema. Hawatamwamini Mungu ambaye angewapenda namna hiyo.

Au tuseme Barabba alisema ‘nitakapobadiliika niwe mtu mzuri wa chi yangu, ndipo nitakubali msamaha huu? Wenzake wafungua wangemjibu “Wacha ufara lazima uwe huru kwanza kabla ya kuwa mtu wa manufaa katika jamii.

Kwamba uwe mtu mzuri ndiposa upate kupatanishwa na krisito ni injili ya uongo. Injili hasa ni kumwalika krisito kwenye maisha kwa njia ya imani ndipo upate hamazisho na nguvu ya kuwa mtu mwema.

Kama vile askari walikuwa wakimuongoza yesu kuelekea mahali ambako angeuliwa, walimshika Simioni mkurene—na kumtwika msalaba na kumfanya aubebe nyuma ya Yesu (Luka 23:26). Mkono wa mungu ulikuwa katika jambo hili pia; simioni alikuwa mtu wa mataifa kutoka Afrika kasikazini wa kwanza kuchukua msalaba na kumfuata yesu, watoto wake Alexandra na Rufusi walikuwa wafuasi wa yesu na walijulikana vizuri katika kanisa la kwanza (Mariko 15:21), Warumi 16:13). Yesu hakufa kwa ajili ya wayahudi tu, bali kwa ajili ya dhambi za ulimwengu mzima (1 Yohana 2:2).

19: Yesu Msalabani

Magaidi wawili waliokuwa wameshikwa pamoja na barabba waliongozwa kalvari pamoja na Yesu. Walipofika fufu la kichwa hapo walimsulubisha Yesu msabala na magaidi- mmoja kwenye kulia wake na mwingine kushoto wake. Yesu aliwaombea waliomsulubisha. Baba wasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo (Luka 23:32-34)

Kupitia kwa Yesu, tumeingia patakatifu pa patakatifu (Waibrenia 4:16). Msalaba wa Kalvari ndio ufunuo mkubwa wa ukweli. Unatufunulia asili kamili ya Mungu tunayemwabudu – Mungu ambaye si tu mwenye haki na mtakatifu bali pia aliye radhi kujitua mhanga kwa ajili yetu.hakuna mungu mwingine aliyewahi jitoa kafara kwa watu wake. Badala yake miungu wengine hudai kafara kutoka kwa watu wengine. Mungu wetu alijitua kafara ili tuwe huru kutokana na hukumu.

Msalaba ulikuwa matabahu ambayo kwayo mwana kondoo wa Mungu alichinjwa kwa dhambi za ulimwengu. Damu yake ilimwagwa kwa dhambi zako ili uwe huru kutokana na hukumu ya sheria (Yohana 3:18), Warumi 8:1)

Msalaba pia ulikuwa mahali ambapo hukumu ya Mungu ilitekelezwa dhidi ya dhambi, kama ilivyoashiriwa na giza, radi, tetemeko la ardhi na kufunguliwa kwa makaburi ya watakatifu (Matayo 27:50-53). Kama vile msalaba wa Yesu uliwagawanya watu wawili walioangikwa naye kuwa, wapotevu na waokolewao, ndivyo unagawanya ulimwengu kuwili, wapotevu, na waokolewao. Siku moja tutapangwa nyuma ya hawa watu wawili kulingana na vile tutakavyo mwitikia Yesu.

Sawa na hawa watu wawili, sote twastahili kifo. Tofauti pekee yake ni kuwa wengine tumetubu.

Kalvari, upendo na chuki vilikutana muumbaji amejitolea kuwa kafara kwa vyumbe vyake huku vyumbe vikiisisitaki

kumuua muumbaji. Lakini wakati damu ya Yesu inachuruzika, misumari ikigongelewa mikononi na miguuni pake, Yesu anaomba 'Baba wasamehe.....

Tulikuwepo siku hiyo, tulinyanya nyundo na kugongelea misumari. Ni dhambi zetu zilizomsulubisha Yesu. Ni kwa dhambi zetu aliangikwa pale ili tusamehewe.

Kalvari ilikuwa jehanamu- Jehanamu ya kimwili na kiroho. Kilikuwa ndicho kitu tu mwanadamu alichowahi kutengeneza. Na Kristo alikuwa amejitoa kwa kina chake ili akiangamize kutoka ndani ya wote watakaoweka imani yao kwake. Ni kwamba achukue nafasi Yesu jehanamu au tuijendee wenyewe. Hakuna uchaguzi mwingine.

Kristo msalabani ndiyo sababu ya Mungu kutusamehe dhambi. Ni katika kalvari tunajifunza dini ya kweli ilivyo. Ni kuhusu upendo usioaminika, ni kuhusu msamaha, haki, tumaini kwenye lindi la giza, na ni kuhusu furaha ukitawala huzuni.

Mtu Fulani aliandika kwamba msalaba ni kuishi hubiri la mlimani, kufunuliwa kwa amri kumi, na I Wakorintho 13 kutimishwa. Huko tunalionia tunda la roho katika ubora wake.

Msalabani Yesu alitwaa uchungu wa kifo. Nyuka amngatapo mtu hujiua kwa sababu amepoteza sehemu ya mwili wake na huwezi kungata tena. kifo kilipomngata yesu kilijiangamiza. Ndio maana Paulo anandika akiuliza kifo, wapi nguvu zako, ewe kaburi wapi ushidi wako? (I Wakorintho 15:55). Yesu alichukua mngato wa kifo tuishi milele.

Nakala za injili zatwambia kwamba misalaba mitatu ilinuliwa kando ya barabara. Watu walipita huko walitikiza vichwa vyao kwa Yesu. Walimkejeli mfalme alyekataliwa na ndivyo ilivyo hata leo. Wengi katika safari zao wanabahatika kupitia alikosulubiwa Kristo, wanashangilia na kumdhihaki.....

Kuna wachache waliotua na kuona utukufu kupitia kwa damu, jasho na nzi. Walikiri pamoja na akida kwamba, hakika huyu ni mwana wa mungu. Na ndivyo ilivyo hata leo. Huku wengi wakidhahiki na huku Ukristo na wafuasi wake wakikosa umaarufu, kuna wale watakaona utukufu kwa mwanga wake.

Ilikuwa ni wakati wa pasaka mwokozi wetu alikuwa. Kwa karne 15, taifa la wayahudi lilitabiri tarehe ya kufa kwa masihi ambaye ingekuwa siku ya 14 mwezi wa kwanza wakati kafara za kila familia zilikuwa zinatolewa saa tisa mchana. Mwezi huo huo, tarehe ile ile na saa ile ile Kristo mwanakondoo wa pasaka yetu alitolewa kafara msalabani. (I Wakorintho 5:7). Namna kondoo aliyechinjwa aliviyowaweka wana wa Israeli huru kutoka kwa utumwa wao kule Misri, na kuanzisha safari yao kwenda kanani, ndivyo kifo cha Yesu katika pasaka ya mwisho kiliviyotuweka huru kutoka hutumwa wa shetani na kutuanzishia safari kwenda mbinguni.

Kule kukubali msalaba kwa Yesu, kunatufunza kwamba, pale tusipoweza kubadilisha mambo kuwa bora, lazima tumwamini Mungu ambaye anaweza na huweza kwa wakati wake kugeuza taji yetu ya miiba kuwa taji ya utukufu.

Bwana wetu alivuliwa nguo. Kabla atundikwe msalabani. Hakuwa na chupi, akinninginia hewani kama aliyekatiliwa na Mbingu na dunia ni dhahiri Kwamba hamiliki chochote wala hana haki ya chochote. Fikiria kwamba mmiliki wa dunia na mbingu uachwa uchi aliaachilia kila kitu ili tumiliki kila kitu.

Kusulubisha haikuwa kifo- ilikuwa ni mbinu ya kuvuta kwa uchungu mwingine mpaka kifo. Maisha ni usulubisho uendeleo mpaka tutakapokufa. Lazima tujifunze namna ya kukabiliana nao kwa kumwangalia yule aliyekuwa pale kwa nihaba yetu.

Ile sura ya msalaba imeuchora urefu, ufupi, ubana, na kina cha upendo wa Mungu. Unaelekea mbinguni ambako Mungu alitokea lakini umezimikwa kwa dunia ambayo alikuja

kuikomboa. Mikono yake iliyonyoshwa ni mwaliko kwa watu wote, hata kwa wachomi wake waje kwake. Watu wanaweza kumkataa

Mungu mwenye hasira lakini watamkataaje atesekaye, aliyejiondoa kufa kwa ajili yao?

20: Maneno Saba Yesu Msalabani

Huku Yesu akininginia msalabani, alitamka maneno saba. Haya maneno saba hueleza majuukumu saba muhimu ya wafusi wa Kristo.

Maneno yatamkwayo katika kitanda cha mauti ni ya thamani mno. Ni muhimu zaidi kiasi gani kwa maneno ya Yesu Kristo mwana wa Mungu anayekufa ndio haya yafuatayo:

Kwanza neno la msamaha kwa maadui wake, “Baba, wasamehe kwa kuwa hawajui walitendalo” (Luka 23:34)

Pili neno la wokovu kwa mwizi aliyetubu na waliyelebiwa naye(hakika nina kahidi leo, utakuwa pamoja nami paradiso (Luka 23:43)

Tatu neno la msalaba kwa mama yake ‘Huyu mtu sasa ni mwanaao, ‘Ndipo akamwambia Yohana, ‘huyu sasa ni mama yako (Yohana 19:26-27)

Nne neno la uchungu kwa Mungu, ‘Mungu wangu, Mungu wangu mbona umeniacha? (Mat 27:46)

Tano, neno la mateso kwa watazamaji ‘Nina Kiu’ (Yohana 19: 28)

Sita, neno la ushidi kwa watu wake ‘Imeisha’ (Yohana 19:30)

Saba, neno la uhakikisho kwa Baba yake ‘Baba nimejisalimisha mikononi mwako! (Luka 23:46)

Neno la kwanza kutoka msalabani ni la muhimu sana. Ni ‘Baba tunaweza kukabiliana na vitu vigumu vya maisha ikiwa tunajua Baba mpenzi anayetujali tunaweza kuvumilia karibu kila kitu kama kuna sababu nzuri ya kufanya hivyo. Mtoto anaweza kuimudu hata dawa kali zaidi madam anapewa kutoka kwa mikono ya wazazi wake. Lakini kuwa mpweke, kutokupendwa, na kuteseka bila sababu inadhoushifa na kuangamiza.

Maneno saba ya Yesu yalielekezwa kwa marafiki na maadui waliosimama karibu na msalaba. Kama kawaida, pamoja na saba ya maandiko, yamegawanywa katika makundi ya tatu na nne, ambapo kundi la kwanza likiwekwa wakfu kwa ajili ya mahitaji ya wengine. Kuandamana na maneno haya , giza la siri ya ajabu lililogubika mahali pale kwa masaa matatu, huku Yesu akiwa amenyamaza kimya. Ulipowadia mwisho wa mola huu, alilia kwa sauti, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona Umeniacha? (Matayo 27:46). Ndipo, maneno matatu ya mwisho ya Yesu yaliandamana mfululizo kwa haraka, moja baada ya lingine.

Askari wa Kirumi na wapitaji wa shingo upande walitegemea kusikia chemi chemi za matusi kutoka kwa hawa watatu waliosulubiwa kulingana na Seneca, mzalendo wa Kirumi na mwanafalsafa wale waliosulubiwa waliikana siku walliyozaliwa, mama zao, wasulubishaji wao na saa zingine waliwatemea mate waliokuwa chini yao wakati Fulani ndimi za waliosulubiwa zilikatwa ili kunyamazisha matusi na laana. Badala yake, yesu aliwaombea waliomsulubisha akiomba Mungu awasamehe.

Hatuanzi kuishi mpaka tukapofunga milango ya zamani kupitia msamaha. Na hakuna atakayekuwa salama mpaka awe na uzoevu wa msamaha wenyewe. Kwa bahati nzuri, si vigumu kujua wakati tunapopokea msamaha sisi wenyewe. Kama vile huwezi kumpatia mtu pesa mpaka umezipokea wewe mwenyewe, hivyo huwezi kutoa msamaha kwa mtu mpaka uupokee wewe mwenyewe. Kama huwezi kumsamehe mtu aliyekukosea, ni kwa sababu hujapokea msamaha wewe mwenyewe. Na kama hujasamehewa, basi hujaokolewa (Matayo 6: 14-15) msamaha ndio daraja ambayo sisi sote tutavukia kuingia katika ufalme wa mungu.

Kila uhusiano katika maisha wahitaji msamaha. Hakuna wake wakamilivu, waume wakamilivu, au watoto wakamilivu. Hakuna waajirl wakamilivu au waajiri wakamilivu. Na hakuna marafiki wakamilivu au majirani. Kwa sababu hii, msamaha lazima uwe msingi wa uhusiano wetu na wengine. Lazima uwe wa kawaida kama kulivyo kupumua.

Hebu tulingalie neno la wokovu. Kama iliwezekana Yesu kutoa uzima wa milele kwa mwizi aliyetubu msalabani mtu ambaye hakuwa na chochote kizuri cha kumpendekezea kwa Mungu- kuna yejote wetu anayeogopa kwamba huenda Mungu asimsamehe? Lakini usiache kutubu mpaka saa ya kumi na moja maana waweza kufa saa nne na nusu.

Kitu cha kutia moyo zaidi kilichomtendekea Yesu, kule msalabani ni kwamba mmoja wa wezi aliyekuwa akitukana amenyamaza kwa utulivu na kuichunguza tabia ya Yesu. Njia ambayo Yesu alikabiliana na watesi wake ilikuwa tofauti kabisa na ile ya wenzake. Ndiposa akakumbuka visa vyote alivyosikikia kuhusu Yesu na kutambua kwamba vilikuwa vya kweli. Hapo ndipo alijichukia na maisha aliyoishi. Vipi alitamani lati angelifanana na Yesu ambaye aliwaponya watu badala ya kuwaua. Akimgeukia mwenzake aliyekuwa akimtukana Yesu, aliuliza ‘Humwogopi Mungu? Si unapokea adhabu moja na mtu huyu? Sisi tunapokea tulichostahili, ila yeye hakutenda chochote kibaya (Luka 23:40-41)

Kwa maneno haya, yule mwizi alionyesha kwa wakati ule kuwa alikuwa mwerevu kuliko Anasi Kayafa, Kikao cha wazee na Herode. Kutoka katika mahakama yake ya juu alirudisha nyuma hukumu kuhusu Yesu. Basi akigeuza kichwa chake kwa Bwana, aliomba, Yesu unikumbuke utakapokuja katika ufalme wako!

Tazama tofauti baina ya mwizi aliyetubu na yule mwenzake. Hakuomba maisha katika ulimwengu. Hakuomba ashushwe

chini kutoka msalabani. Kwa mara ya kwanza katika maisha yake, aliweka sawa vipaumbele vyake.

Kwa nini wayahudi wakamua Yesu? Kwa sababu walimtaka masihi atakayewaletea ufalme wa kiulimwengu. Yesu, badala yake aliwapa Mungu! Je, sisi si wapumbavu kwa matakwa yetu? Tunahitaji vitu vya dunia mpaka tunazama ndani yavyo, na Mungu anafinyiliwa nje.

Huyu mwizi aliyetubu ni mchoro wa wokovu kwetu sote. Aliokolewa kwa imani katika Yesu na si matendo (tazama Waefeso 2:8-9).

Angalia vile Bwana ahitiakiavyo kwa haraka ‘Nakuahidi, kwamba utakuwa pamoja nami paradiso leo.’ Siku ileile yule mwizi aliweka imani yake kwa Yesu, alisajiliwa kama raia wa ufalme wa Kristo mwenyewe alitangaza hatma yake.

Ni mtu wa ajabu kiasi gani huyu mwizi alikuwa. Lakini kuliwa na mtu mwingine wa ajabu zaidi kutoka ndani mwake. Kristo aliahidi uzima wa milele kwa mtu, ambaye dakika chache zilizopita, alikuwa akimtukana. Kuna neema katika ubora wake, katika ukuu wake, na katika ukina wake katika uhakika wake. Ina maana kwamba, yejote wetu asikate tama, bila kujali maisha ya nyuma, haijalishi ndhaifu au ubaya wetu. Tunaye mwokozi kama u mdhambi mkuu, tunaye mwokozi mkuu.

Zingatia vile vile kwamba haijalishi majaribu unayoyipitia, Bwana Yesu amepitia mabaya zaidi. Huyu aliyetubu alikuwa kifo cha kwanza tu; Yesu aliyeangikwa kando, yake angekufa kifo cha pili- kifo ambacho kisingempa nafasi ya maisha zaidi ya kaburi.

Neno la tatu la Bwana wetu msalabani ni tamko la upendo kwa mama yake. Anamwona amesimama akionekana kana kwamba ndiye anayepitia machungu ya kuangikwa. Anakumbuka kwamba siku ya kwamza Yesu, alitahadhalishwa kwa upanga ungechoma moyo wake. Ni kweli kiasi gani!

Haikuwa anaelewa kuwa mwanaye alikuwa katika shughuli ya babaye. Hata hivyo, Yesu hakosi kuwajibika kwa familia yake-Anamwomba Yohana amtunze mama yake, Jambo ambalo kila mwana angefanya.

Katika neno la nne kutoka msalabani, ‘Mungu wangu, mungu wangu mbona umeniacha? tunapata sababu ya kifo cha Yesu. Rekodi za wakati na umilele hazina msemo uliofaa na uchungu. Si kifo kilicho mshahara kweli wa dhambi, ila kutenganishwa na Mungu. Wakati Mungu aliye chanzo cha uzima wote, tumaini, furaha na amani hutoweza pia. Na hiyo ni jehanamu mbali na Mungu, hakuna umilele kamwe. Ni shimo lenye giza la maangamizo.

limbidi Kristo aliyebeba dhambi za ulimwengu kuonja utengano huu. Mungu alijitenga na Yesu ili aungane nasi. Yesu aliachwa mpweke ili tuwe washirika wa familia ya Mungu. Alikufa ili tuishi milele. Hiyo ndiyo kafara aliyoitao Bwana wetu. Aliacha vyote ili turithi vyote.

Lilofuata ni neno la mateso ‘Nimeona Kiu’ Hakuna malalamiko ya uchungu yaliyotoka kinywani mwa Kristo. Hakutamka neno lolote la kujuhurumia. alitoa tu tamko la kweli nimeona Kiu. Askari alichukua kitambaa na kukikosa ndani ya siki na kumunywesha kwenye vinywa vyake.

Divai hii iliashiria divai ya dhambi zetu (Matayo 26: 20) Yesu aliiemeza yote, akijua kwamba kwa kufanya hivyo, hakungekuwa na njia nyingine ya kurudi nyuma.

Neno la sita la Yesu lililofuata katika saa ya sita msalabani, katika siku ya sita ya Juma, alipaza sauti ya ushindi imekwisha! Katika ya asili ni neno hilo. Hilo hilo neno kwa mdeni lilimaanisha kuwa deni lake limelipwa kwa ukamilivu. Hilo neno kwa mfungwa lilimanisha, hukumu imemalizwa, na ndivyo ilivyo kwetu. Deni letu kwa Mungu limelipwa kwa ukamilivu na

kifungo chetu cha kifo kimekamilika sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu kwa walio ndani ya Kristo Yesu (Warumi 8:1).

Huku Yesu akizungumza haya, pasia la hekalu lilipasuka kuwili kutoka juu hadi chini kuonyesha kwamba, Yesu kwa kifo chake ameondoa kizuizi kilichomzuia mwanadamu kutoka kwa Mungu, ili sasa tuweze kwenda mbele za Bwana kwa ujasiri (Matayo 27:51, Waibrenia 10:19-22). Alitengwa na Mungu ili tuingie ndani.

Neno la mwisho la Kristo kwa Baba yake ‘Baba mikononi mwako naiweka roho yako (Luka 23:46). kama Ayubu aliyeishirikilia imani yake kwa Mungu licha ya mateso yaliyomkumba, Yesu alijisalimisha kwa Baba yake hata kama hapakuonekana namna nyingine ya kujinusuru kutokwa maangamizo.

Kama Bwana wetu alivoyoyasema maneno yake ya mwisho, sauti ilichangamana na vilio vya wanakondo wa pasaka nje ya kisimba cha nje ya hekalu kwenye uliopakawa na Kalvari. Lakini imani haipo kwa damu ya wanakondoo bali kwa damu ya Kristo mwanakondoo wa pasaka yetu (I Wakorintho 5:7) aliyetolewa kafara kwetu.

Tunajua vyema misemo saba kutoka msalabani, lakini pia kuna misemo saba kwenda msalabani. Misemo hii ilisemwa kwelekea msalabani na wapita njia (matayo 27: 39-40)

Mwizi aliyekuwa upande wa kushoto na mwenzake wa upande wa kilia (Luka 23:39; 23:40-42). Kuhani mkuu, walimu wa sheria na wazee (Matayo 27:41-43), watu Fulani waliosimama karibu na msalaba (Mariko 15:35); Askari (Luka 23:36-37); na akida (Mariko 15:39).

Tayari tunagundua kutoka katika mbili ya misemo hii kwamba mti mpya wa uzima ulikuwa tunda. Mwizi aliyetubu alikuwa muuaji na akida, watu wawili ambao waliwakilisha milengo ya miwili ya waliokolewa. Lakini kwa

watazamaji wengi, msalaba ulikuwa hasa. Na imesalia hivyo hata leo.

Mwandishi asiyejulikana alisema, Yesu alianza huduma yake akiwa na njaa licha yake kuwa mkate wa uzima. Alikamilisha huduma yake akiona kiu licha yake kuwa maji yaliyo hai. Yesu alichoka na yeye ndiye pumziko letu. Yesu alitoa heshima licha yake kuwa mfalme. Yesu alishtumiwa kuwa na mapepo, wakati ndiye aliyetoa mapepo. Yesu alilia, lakini anayafuta machozi yetu. Yesu aliuzwa kwa vipande thelathini vya fedha, lakini alikomboa ulimwengu. Yesu aliletwa kama mwaanakondoo kichinjoni, lakini ndiye mchungachi mwema. Yesu alikufa lakini kwa kifo chake akashinda kifo.

21: Nyuso Zilizozunguka Msalaba.

Hebu na tuanze na watu wawili waliosulubiwa na Yesu. Wote walikuwa magaidi. Yesu aliyesulubiwa nao, alikuwa na dhambi juu yake bali si ndani yake. Yule mtu wa kulia ni mtu aliyekuwa na dhambi ndani yake ila si juu yake maana alikuwa amesamehewa. Yule mtu wa kushoto alikuwa na dhambi ndani yake na juu yake kwa sababu alikuwa hajaomba msahamaha, hatia yake ilibakipamoja naye.

Hii ina maana gani kwetu leo? Fikiri kuhusu yule mtu aliyeokolewa alikuwa rafiki wa karibu wa mwisho wa Bwana. Alikuwa na ujasiri wa kukiri kwamba ye ye ni mkosaji. Hata alirudisha nyuma hukumu ya makuhani wakuu na warabbi aliposema kuhusu Yesu, huyu mtu hajafanya chochote kibaya. Huyu mdhambi aliyetubu anawakilisha wenyе dhambi wote watakaotubu.

Bado tunayo dhambi ndani yetu ingawa twaichukia lakini sasa haiko juu yetu kwa sababu tumeikabidhi Yesu aliyekuwa dhambi kwa ajili yetu. (Il Wakorintho 5:2) tumesamehewa na hatia yetu imeondolewa.

Tazama sasa gaidi mwingine ambaye hakutoa dhambi zake kwa Yesu. Alikuwa karibu kwa Yesu kama yule gaidi mwenzake, lakini hakutambua uovu uliokuwa majoni mwake. Hakukubali kuwa alikuwa mgonjwa wa kiroho.

Ni wale tu wanaokubali kuwa ni wagonjwa huenda kwa daktari. Ni wale wanaotambua kuwa ni wenyе dhambi wataftafuta mwokozi.

Je, wokovu u rahisi au mgumu? Si mgumu tu bali hauwezekani isipokuwa unahitaji kuwa mwema kuliko ilivyo. Kuna umati wakristo na kikafiri wanaojiamini zaidi ya wanavyo-mwamini Yesu. Sasa, sawa na yule gaidi watakufa katika dhambi zao.

Tazama sasa askari kule msalabani matayo 27:35 inasema, walipokwisha kumushulubisha, waliyagawa mavazi kwa kuyapigia kura. Na wakiwa mameketi walimchunga akiwa kule juu. Hapa kuna watu waliokaa na kutazama alikuwanatazama lakini hawakumwona mfalme. Na ndivyo askari walivyomwona Yesu kama muasi yeyote apeokeaye adhabu kamili dhidi ya matendo yake.

Askari waliomsulubisha Yesu wanawakilisha taifa lote la wanadamu. Yesu hakufa kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe maana hakuwa na dhambi, alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Lakini dunia isiyojali, sawa na wale askari, haimwoni mwana wa Mungu akifa kwa dhambi zake. Kwa maana ni vipofu wa kiroho, wao wanamwona mtu tu mwingine aliyedharauliwa akininginia huko. Ni hasara ya namna gani! Yesu alikufa kuwatia huru kutoka kwa dhambi zao, lakini wanazipenda dhambi zao kuliko Yesu.

Moja kati ya nyuso zilizokuwa karibu na msalaba ni uso wa akida. Alikuwa pale kwa sababu alikuwa kiongozi wa kikosi cha wasulubishaji.

Alitambua Yesu ni mtu wa aina gani na akasikiza kila neon alilotamka. Yale masaa matatu ya giza lisilo la kawaida, na mtetemeko wa ardhi uliotokea alipokufa Yesu, uliashiria kwa akida kuwa Yesu hakuwa mtu wa kawaida. Akida akiona yaliyotendeka alikiri kuwa hakika huyu alikuwa mtu wa haki (Luka 23:47). Huyu mtu aliyejukumishwa kumwangika Yesu msalabuni alikiri imani yake kwa Yesu. Ni injili ya ajabu kiasi gani, inayoweza kubadilisha hata miyo ya wale wamsulubishao Bwana. Inayobadilisha maadui kuwa marafiki.

Makuhani wakuu, walimu wa sheria, wazee walikuwa huko msalabani pia. Walimdhihaki na kuwaambia! (Matayo 27:41-42). Walichokisema kilikuwa kweli. Kama Yesu angejiokoa

mwenyewe, basi hangeokoa wengine. Ilimbidi afe kwa dhambi za ulimwengu.

Hawa viongozi wa kidini sawa na viongozi wengi wa kidini wa leo, wanaoweka imani yao kwa tamaduni na taasisi zao kuliko kwa Yesu, walimpinga Yesu. Walipaza sauti kwa kila mmoja kusikia. "Yeye ndiye mfalme wa waisraeli! Hebu na ashuke sasa kutoka msalabani, nasi tutamwamini. Anamwamini Mungu, hebu na amwokoe (Matayo 27:42-43). Ahadi zao hata hivyo zilikuwa za uongo kwa sababu Yesu alipotoka alipojirasua kutoka kwa kifo, na mungu akamwokoa kutoka kaburini, hawakumwamini bado. Nani atawatetea wanafiki hao wakati wa huruma?

Wengine msalabani, ni wale wote waliomjua pamoja na wale wanawake waliomfuata kutoka Galilaya. Walisimama kwa mbali wakiyatazama matukio hayo. (Luka 23:49)

Mwisho wa Yesu ulivyokaribia, baadhi yao walikaribia kumfariji (Yohana 19:25-26). Hawakuelewa ni kwa nini Yesu aliruhusu mambo haya mabaya kumtendekea. Alikuwa ameshinda kila changamoto maishani kwa nini ashindwe na hii? Mbona hakuonyesha mamlaka yake au kushuka msalabani?

Mara nyigi maishani tunauliza swalii kama hili. Kwa nini hafanyi kitu? Mbona aruhusu uovu mkubwa namna hii? Kuna sababu. Twahitaji kuamini kwamba Mungu atafanya jambo kwa wakati wake. Na atakapofanya, itaonekana kwamba wakati wake ndio bora. Kwa hivyo kuwa na imani kwamba hasa unapopita chini ya bonde la kivili cha mauti.

22: Mafundisho Yatokayo Msalabani.

Maandiko

Juu ya kichwa cha Yesu kuliwa na nakala ya andiko la kejeli dhidi yake. MFALME WA WAYAHUDI (MARIKO 15:26). Lilikuwa limeandikwa kwa lugha ya kiaramaika kilatini na kiyunani (Yohana 19:20) ili kila mmoja aliyepita aweze kusoma. Andiko hilo ambalo lilikuwa Biblia kwa ulimwengu wote, lilitoa ukweli kumhusu Yesu.

Kama Yesu asingalikuwa msalabani asingalikuwa na ufalme wowote duniani. Ni mauti yake yaliyolipa gharma ya dhambi zetu ili tuachane na ufalme wa mda wa shetani, tuingie katika ufalme wa milele (Wakolasai 1:13-14). Kupitia mauti yake alifungua mlango kwetu ili turejee kwenye nchi ya uzima na kutoka kwa nchi ya mauti (Matayo 27: 50-51) Waibrenia 10:19-22). Ni waliokombolewa kwa damu, ya mwanakondoo watakaongia pale (Ufunuo 7:14-15); ni waliosamehewa tu, watakaokuwa raia wa mbinguni (Ufunuo 5:9-10).

Mmoja tu atakayekalia kiti cha utukufu cha uzima wa milele ni yale ambaye angevumilia kiti cha mauti ya milele- msalaba. Kwa sababu Yesu alivumilia msalaba kwa ajili yetu, alitunukiwa kuwa mfalme. Baada ya kufufuka kutoka kwa wafu, aliwaambia wanafunzi wake, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani (Matayo 28:18) tazama Wafilip 2: 9-10). Hakuna anayeweza kuwa na mamlaka ya juu kama hayo. Ndio Yesu ndiye mfalme wa kila muumini.

Taji Ya Miiba

Askari walimvisha Yesu vazi la sambarau ndipo wakaikunja taji ya miiba na kumvisha Yesu kichwani. Walimwita, hewala mfalme wa wayahudi! Mara kwa mara walimchapa kichwani

kwa fimbo na kumtemea mate. Wakiiga magoti yao walimpa heshima ya kejeli (Mariko 15:16-19)

Yesu alivumilia aibu, na kejeli yetu ili tuweze kupokea heshima na taadhima iliyokuwa yake.

Miiba inayotusumbua, haitatusumbua milile kwa sababu Yesu aliondoa umilele huo kutoka kwa shida zetu. Lakini kadri tunavyokaa hapa duniani, tutakuwa na miiba ya kukabiliana nayo. Hakuna taji isiyo na miiba hakuna familia isiyo na shida na hakuna moyo wa binadamu usio na huzuni. Hata mtume Paulo alikuwa na mwiba uliomsumbua. Mara tatu aliomba kwamba Mungu Mungu angemwondolea mwiba wake, lakini kila wakati Bwana alisema, neema yangu yakutosha kwa kuwa nguvu yangu inakamilika katika udhaifu. (IIWakorintho 12: 7-10)

Bila kujali mwiba ulio nao, vumilia katika neema kwa ajili ya Yesu, ukikumbuka kwamba silku yaja upesi wakati miliba iliyokuja duniani kwetu na dhambi (Mwanzo 3:18) itaangamizwa milele pamoja na dhambi ilioizalisha.

Giza Totoro

Kwanzia saa sita mchana hadi saa tisa giza liligubika nchi yote. Yapata saa tisa Yesu akalia kwa sauti “Eloi, Eloi lama sabachthani?” maana yake, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” (Mathayo 27:45-46).

Mchana, jua likiwa angani, giza nene liligubika nchi Mungu anayeishi kwenye mwanga unaopofusha (Timotheo 6:6) ulikuwa anaondoka polepole kutoka kwa Yesu. Ule uhusiano wa milele kati ya mwana na baba ulikuua unakandamizwa. Jua lilipisha giza, amani- uoga, tumaini likapisha kukata tama, usalama ukapisha utovu wa usalama na uzima – mauti. Pindi tu hili pigo la giza lilikamilika, malaika wa pasaka alitokea kuchukua

maisha ya mwana mzaliwa wa kwanza wa Mungu. Alitoa maisha yake kwetu ili tuishi.

Kulitanda giza nene katika nchi ya Misri kabla ya kifo cha wazaliwa wa kwanza (Kutoka 10-11), lakini kulikuwepo mwanga kwenye makazi ya waisraeli ambao walikua wamelindwa na damu ya mwana kondoo wa pasaka. Popote hivi leo ambapo kuna imani ndani ya mwana kondoo wa Mungu, kuna mwanga.

Yesu alipopaza sauti “Mungu wangu , Mungu wangu mbona umeniacha? Maneno yake yalikuwa mwanga uliomulika tukio zima. Yeye mwenye haki, aliachwa, ili sisi tusio na haki, tuweze kukubaliwa. Kifo chake ni mwanga wa injili unaongamiza giza ikiwa hatutashiriki mwanga wa injili, bali tuufiche chini ya meza, hakutakuwepo kitu ila kukata tama, utupu na mauti (Mathayo 5:14-16).

Vazi Lake

Wakati askari walimsulubisha yesu walichukua mavazi yake wakayagawa mafungu manne moja kwa kila mmoja huku wakimwachia ya ndani tu. Vazi hili halikuwa limeshonwa fumwa lote kutoka juu mpaka chini

“Tusilirarue wakasemezana wao kwa wao”. Hebu tupigekura nani talichukua.

Hili lilitendeka ili maandiko yapate kutimizwa yaliposena waligawanya mavazi yangu na kuyapigia kura “waligawanya mavazi yangu na kuyapigia kura “kwa hivyo hiki ndicho askari walifanya (yohana 19:23-24)yesu alivuliwa nguo alishafanya hivyo miaka 33kabla alipojivua utukufu wa mbingu na kuzaliwa humu duniani uchi kama mtoto wa kibinadamu masaa24 kabla hajasulubishwa yesu aliigiza hilo alipovua vazi lake la nje na kujifunga taulo kiunoni ili kuwatawadha wanafunzi wake .vazi la yesu ndani ambalo halikuwa na pindo,lilikuwa la kikuhanii

vazi hili liliwaendea askari waliomsulubisha yesu .na hilo ndilo linalotendeka hata leo sisi ni wasulubishaji na vazi la haki la yesu kristo limewekwa tayari kwa ajili yetu tunapoweka imani yetu kwa yesu dhambi zetu zinafunikwa na haki yake .isaya aliandika “nitafurahi sana amenivika na mavazi ya wokovu na kunipamba na vazi la haki” (isaya61:10)

Pazia Liliopasuka

Tetemeko liloloadhimisha kifo cha yesu lilipasua kutoka juu mpaka chini liliogawa mahala patakatifu mno pa hekalu ambapo uwepo wa mungu ulishamiri (mathayo 27:51) tetemeko lilo hilo lilitfungua makaburi ya watakatifu wengi. Watu hawa walifufuliwa na baada ya yesu kufufuliwa kutoka kwa wafu ,walienda kwenye mji mtakatifu na walijitokeza kwa watu wengi (mathayo27:52-53) Ni kifo cha yesu kilicho funga njia ya kurudi kwa mungu –njia ambayo ilishafungwa tangu adamu aondolewe edeni (mwanzo 3:22-24)biblia yasema,basi ndugu kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya yesu ,njia ile aliyotuanzia iliyo mpya iliyo hai ,’ipitayo katika pazia yaani mwili wake ...na tukaribie karibu na mungu (waibrania10:19-20).

Pazia baina yetu na mungu liliashiria dhambi zetu zilizotuzuia kutoka kwa mungu lakini yesu alipochukua dhambi zetu kwake, basi pazia liliashiria mwili wake. Wakati mwili wa Yesu ulipasuliwa msalabani, hilo pazia nalo lilipasuliwa. Kifo chake kilipoondoa dhambi zetu, kizuizi baina ya Mungu nasi kiliondolewa. Mauti yake yalifungua njia kwenda kwa Mungu.

Kiroho, sisi tulikufa kwa dhambi tuliletwa uzimani kupitia kifo cha Yesu. Na katika ufufuo wake kutoka kwa wafu, tuliiingia kwenye mji mtakatifu ili kuishi kwenye uwepo wa Mungu, Yesu na malaika wa mbinguni (Waebrania 12:22-24)

Damu Na Maji

Ikiwa mfungwa yeote alitoroka kutoka kwa askari wa Kirumi huyo askari angeuawa (tazama Matendo 12: 18-19) Hiyo ndiyo ilikuwa sheria. Ikiwa kungeonekana hatari ya wafungwa waliosulubiwa kutoroka, wakati wanashushwa kutoka kwa msalaba, waliuawa (matendo 27:42). Ili kuhakikisha ya kwamba Yesu alikuwa amekufa kweli, askari wa kirumi walimchoma Yesu mkuki kwenye moyo kusababisha mtiririko Fulani wa damu na maji (Yohana 19:34) Askari walikuwa wauji wataalamu walielewa ni vidonda gani vilivyonona na vile visingalipona. Kidonda cha Yesu hakingepona.

Damu ya Yesu iliwakilisha kuhesabiwa haki kwetu. Ni damu ya Yesu inayotufanya kuwa wenye haki kwa Mungu (I Yohana 1:7). Maji kadhalika, yaliwakilisha kuhesabiwa utakaso wetu kwa njia ya roho wa Yesu anayeishi ndani yetu; anatusafi kwa kutuosha kwa maji ya neno lake(Waefeso 5:25)

Kuhesabiwa haki ni kazi ya mda mfupi. Pindi tunapoweka imani yetu kwa Yesu tunawekwa sawa na Mungu (Warumi 3:21-24,28). Mara hiyo tunapokea uzima wa milele (Yohana 5:24). Pia, kwa wakati uo huo, haki ya Mungu inaingizwa katika akundi zetu (II Wakorintho 5:21). Kama mwana mpotevu aliyeishi maisha ya dhambi lakini akatubu na kurudi nyumbani, ndivyo Bwana anavyotukubali wadhambi tuliotubu katika familia yake na kuweka roho yake safi mabegani mwetu (Luka 15:11-24). Haifai kwetu kutafuta nafasi katika familia ya Mungu; tumepewa haki kwa 100% (II Wakorintho 5:21). Ila, haki hiyo haiko ndani yetu; ndani ya Yesu kama tunaye Yesu tunayo zawadi ya bure ya haki kamilifu ya Mungu. Utakaso – anachofanya roho mtakatifu kwetu si 100% na haitakuwa 100% mpaka tutakopewa miili mipya ya kiroho katika ufufuo (IWakorintho 15:42-44). Kwa kuwa utakaso maisha haya bila

shaka utapungua kinachohitajika kwa uzima wa milele, hatutaweka imani yetu kwa kile tunachofanya. Imani inayotupatia uzima wa milele ni imani iliyo ndani ya Yesu na zawadi yake ya bure 100% ya haki.

Injili inafundisha kwamba Yesu alichukuliwa kama mdhambi, wala sivyo, huku tukichukuliwa kama wenye haki tusivyo. Aliadhibwa kwa dhambi ambazo hakufanya, na tunawekwa sawa na Mungu kwa haki ambayo haituistahili.

Hakuna kitu kinachotia moyo kama kuhesabiwa haki, kumaanisha kwamba nimewekwa sawa na Mungu. Inaniambia kwamba damu ya Yesu imefunika dhambi zangu zote- zamani, sasa na baadaye. Kadri nitakavyoshikilia Yesu kwa imani ninao uzima wa milele hata ninapojikwaa na kuanguka , ikiwa nitainuka niushike mkono wa mtu wa Galilaya, nimesamehewa na kuwekwa sawa na Mungu.

Ninapomkubali Yesu kwa imani, anakuja kwa maisha yangu na zawadi yake ya wokovu kama ninaye Yesu ninao uzima (1 Yohana 5:11-12). Na maisha ambayo anayaishi ndani yangu baada yangu kuokolewa inaitwa utakaso (Wafilipi 2:13). Hata hivyo, ninaokolewa tu kwa kile alichonifanya msalabani karibu miaka 2000 iliyopita na sio kwa anachokifanya ndani ni 100%, anachofanya ndani yangu katika maisha haya si 100% kwa sababu ya madhara ambayo dhambi imefanya kwa mawazo yetu.

23: Yesu Apumzika Kaburini

Moja ya siku kuu za posaka iliyotunzwa na kanisa la kikristo kwa miaka ya kwanza mia tano ilikuwa sabato kuu siku ambayo alipumzika kaburini siku hii ilishelekea punziko ambalo Yesu alitushudia kwa mauti yake msalabani mwandishi wa Waiberania aliandika sisi tulioamini twaingia pumzikoni waiberania 4:3

Waiberania walitololewa kwenye utumwa kule misri waliaminini kwamba wangeingia kwenye pumziko wakati wangefika kwenye nchi ya ahadi lakini kanani haikuwa pumziko lisilovunjika kama walivyokusudia pumziko hilo la ahadi lilikwa la siku usoni kama joshua angewapatia pumziko Joshua 23:1

Mungu asingalizungumzia baadaye kuhusu siku nyingine basi kumesalia pumziko kwa ajili ya watu wa mungu kwa kuwa yeoyote aingiaye kwenye pumziko la mung u apumzike kutoka katika kazi yake (waiberania 4:8 -10)

Pumziko la kweli kutoka katika shida zetu linapatikana ndani ya yesu mwenyewe pekee ikiwa tutakubali kwamba yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu mzigo mzito wa hatia unaanguka kutoka kwa mabega na kuviririka chini ya mlima mpaka kwenye kaburi ambako unazikwa milele .Hapo ndipo tutapata uzoevu wa pumziko la kweli

Mungu alipokamilisha kazi yake ya uumbaji, alisema ni vizuri imekwisha na akapumzika siku ya sabato (mwanzo 2:1-3) Na Adamu na Hawa walipumzika pamoja naye. Hakuna chochote wangefanya ili kuuboresha uumbaji wa mungu hakuna chocho wangefanya juu yake. Ambacho wangefanya tu, ni kumtukuza kwao kupumzika na kuufurahia.

Wakati bwana wetu alikamilisha kazi yake ya ukombozi, alisema ni vizuri, imekwisha, akapumzika siku ya sabato (Luka 23:50-56). Na wote waliokombolewa kuingia katika pumziko

pamoja naye. Tunaloweza kufanya tu, ni kumtukuzza Bwana kwa ajili ya ukombozi, na kupumzika, na kuufurahia.

Kama ambavyo sabato ilikuwa siku ya pumziko na si ya kazi hivyo sisi tunaoweka tumaini letu ndani ya yesu twapumzika katika kaza yake iliyokamilika. Hakuna chochote tutakachofanya ili tupate wokovu maana yesu amefanya kila kitu kwa ajili yetu .tutakalofa ni kupumzika ndani ya kazi yake iliyomalizika. Hilo ndilo pumziko la kweli, na tunasherehekea pumziko hilo tunapokuja pamoja kila juma kando ya kazi zetu ilikuwa na muda pamoja na bwana wetu.

24: Kaburi La Yesu Li Wazi

Dunia yote ni kaburi limezalo mabillioni ya watu ulimwenguni mahali pa makaburi ambapo tunafanyia biashara kidogo tunajilingiza kwenye raha kidogo na baadaye tunashuka chini kulala kando kando ya wafu maisha ni safari tu ya kuelekea kwenye mazishi yetu. Mwanadamu amevishida vitu vingi sana ila kifo si mojawapo.

Kumekuwepo na viongozi wa kidini wengi duniani lakini wote wamesalimu amri dhidi ya kifo. Ni mmoja tu aliyefufuka kutoka kwa wafu, na huyo ni yesu kristo wakati bwana wetu alifufuka kutoka kwa wafu aligeuza vibao kwa dhambi na kifo wimbo kwa wingi waliokombolewa sasa ni u wapi ewe mauti kushinda kwako?

Mtume Paulo aliandika kwa maana niliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe kwa kuwa kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo maandiko na kwa kuwa alizikwa ‘na kwa kuwa alifufuka siku ya tatu kama yanenavyo mandiko na yakuwa alitokea kufa na wale thenashara baaadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja katika hao wingi wanaishi hata sasa ila baadhi yao wamelala .baadaye akamtokea yakobo tena mitume wote na mwisho wa watu wote alinitokea mimi kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake (1wakorinto 5:3-8)

Wakwati Paulo aliandika waraka huu kwa kanisa la Koritho yapata miaka ishirini na tano baada ya kufa na kufufuka kwa yesu, kulikuwa na mamia yawatu hai waliomwona yesu aliyefufuka, anayeweza kuzungumsiwa. Hata kama mlevi anasoma habari hizi huku amelewa bado sitamsisimua.

Mauti yameshindwa na Yesu aliyefufuka kutoka kwa wafu baada ya siku tatu anasema, kwa wote wanaomfuata, kwa sababu ninaishi (Yohana 14:19). Alisema pia ndimi ninayeishi

nilikufa na tazama niko hai milele, na nimebeba funguo za kifo na kuzimu (ufunuo 1:18). Yesu ajapo kwa mawingu ya mbingu atafungua makaburi ya wote wanaomwamini na kuwatia huru (1 Wathesolonika 4:16-18).

Kwa maandiko yote tunapewa taswira ya ufuluo wa yesu. Mwazo 22 ni hadithi ya Isaka ambaye kwa siku tatu alikuwa chini ya kifungo cha kifo ila alinusuriwa kama ilivyo katika ufuluo (Waiberenia 11:19).

Pi katika mwazo ni kisa cha Yusufu aliyeshitakiwa na kuhukumiwa na wengine, mmoja wao aliokolewa na mwingine kupotea. Ndipo Yusufu akainuliwa kutoka shimoni na kupewa kiti karibu na mfalme. Kutoka mahali hapo alotoa wokovu kwa watu wake. Yona pia alionja ufuluo. Kafara yake ilizua gadhabu ya mungu, na alirejeshwa uzimani katika siku ya tatu.

Daniel pia alionja ufuluo. Kupitia chuki alitupwa tunduni mwa samba wenye njaa na mlango wa juu ukafungwa (Danieli 6) lakini mlango ulifunguliwa akatoka nje akiwa hai.

Kaburi alilowekwa yesu lilifunika na kulindwa kama liliyokuwa lango la Eden liloongoza kutoka kifo hadi uzima (Matayo 27:62-66). Lakini katika siku ya tatu kulikuwa na tetemeko kuu kwa maana malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni na kwenda kaburini, alitoa lile jiwe na kulikalia. Kuonekana kwake kulikuwa kama umeme na mavazi yake yalikuwa mwupe kama theluji. Walinzi walimuogopa sana kiasi kwamba walikuwa kama wafu. (Matayo 28:2-4). Yesu kwa kufa na kufufuka kwake alirejesha njia kwenda mungu na uzima kwetu. Ndio maana alipofufuka kutoka kwa wafu, wote waliofufuliwa kwa kifo chake waliingia naye kwenye mji mtakatifu (Matayo 27:53). Ni kufa na kufufuka kwa yesu kunaotupa makao ya milele na mungu.

Ardhini mwa Rumi kuna takribani kilomita 1000 za mapito ya ardhi zilizokuwa karibu karibu kilomita 15 chini ya ardhi.

Zilikuwa zimechimbwa ili kupata mawe ya kujengea mji. Ni katika mahandaki haya ambapo wakristo walisika wafu wao. Warumi walichoma wafu wao lakini wakristo walichagua maziko kama ishara ya imani yao katika ufufuo unaokuja katika siku ya mwisho. Katika kila moja ya makaburi arobaini yalokuwa ardhini mwa Rumi kulikuwepo na kanisa kuu mwisho mita isitini mwa mapango haya, hapo ndipo wakristo walioteswa walikutana faraghani na kuimba sifa kwa mungu. Baada ya kila mkutano, wale waliokusanyika walipaza sauti Amefufuka!

25: Yesu Akiwa Galilaya

Punde baada ya ufuluo wake, Yesu alikutana na wanafunzi wake katika chumba cha juu cha Yerusalem na akawatuma wapeleke injili kwa ulimwengu wote. Lakini kabla watoe wokovu kwa wengine walipaswa kuelewa wao wenyewe. Hivyo Yesu akawaambia amani iwe nanyi. Baada ya kusema haya aliwaonyesha mikono yake na upavu wake (Yohana 20:20)

Amani yetu ya kwanza huja tunapoona vidonda vya Yesu na kuelewa kwamba alisulubishwa na kuchinjwa kwa ajili ya dhambi zetu ‘Tulipokuwa wenyе dhambi. Kristo alikufa kwa ajili yetu’ (Warumi 5:8). Amani inakuja kwa wale wanaojua yakwamba Yesu alilipa gharama yote ya dhambi zao. Wana amani miyoni mwao maana hawako tena chini ya hukumu ya Mungu.

Tena Yesu alisema, ‘Amani iwe nanyi’ kama alivyonituma baba, nami nimewatumeni’ (Yohana 20:21).

Amani ya pili ambayo Yesu anatoa ni amani ya kina. Hii amani ya pili inakupeleka ndani zaidi kwa maana ni vuguma kufurahia amani ya kwanza ya wokovu huku marafiki zako na jamaa yako wakiikosa. Amani ya kwanza ni wokovu kwako, amani hii ya pili inakuja unapotoa wokovu kwa wengine. Yesu yuko hapa akikutuma ushiriki wokovu wake na hao.

Lakini, unakataa, ‘sina uwezo wa kushiriki injili na wengine. Nisingelijua la kusema. Yesu anajua hilo, kwa hiyo anakupatia nguvu za mbingu kwa huduma yako. Anakupulizia pumzi na kusema, pokea Roho mtakatifu (Yohana 20:22).

omba kwamba Roho mtakatifu mwenyewe atakujaza na kukusaidia kuleta wokovu kwa wengine. Unapoongoa Roho kwa Yesu, amani kubwa na furaha vitakujaza mpaka kufurika. Yesu hapa anasema, kama utashiriki habari njema kuhusu kufa kwake msalabani kwa ajili ya dhambi za watu, pamoja

unaweza kuwafikia na kuwakubali, watasamehewa. Wajibu ni wako enenda. Kwa nguvu unazopewa na Mungu na uwalete watu katika zizi lake.

Yesu alibaki duniani pamoja na wanafunzi wake kwa majuma sita baada ya ufufuo wake. Sehemu kubwa ya mda huo, alikaa Galilaya ambapo alichukuwa muda wake mwingi kuwahudumia wengine. Yesu alikaa duniani kwa muda wa kutosha mpaka kweli kuhusu ufufuo wake ikahakikishwa.

Lakini kwanza Yesu alihitaji kukutana na wanafunzi kumi na moja ili kujenga uhusiano Fulani ulioharibika. Petro mwanafunzi ambaye Yesu alimchagua awe mwinjilisti Mkuu wa kundi alishamwangusha vibaya. Mara tatu alikataa kwamba alimjua Yesu na hata kuhaba kwa kula kiapo kuhusu hilo mara moja baadaye. Petro alitubu makosa yake na kulia kwa uchungu. Wakiwa wanamsubiri Yesu kule Galilaya petro, pamoja na Yohana, Yakobo, Tomaso, Nathanieli na wanafunzi wengine wawili walienda kuvua usiku ziwani lakini huwakupata kitu (Yohana 21)

Mapema asubuhi iliyofuata, mtu mmoja ufuoni aliita akitata kujua kama walipata samaki yoyote. Hapa wakajibu la yule mtu aliyekuwa ufuoni aliita tupa neti pemberi kulia mwa mashua na mtapata samaki. Wavuvi walikaziana macho na kugusana mabega, na kutupa neti pemberi mwa mashua. Hawakuwa na kitu cha kupoteza. Kwa mshangao, hawakuweza kuibeba neti kwa sababu ya wingi wa samaki walokuwa ndani.

Yohana akidokeza kwa mtu aliyekuwa ufuoni alimwambia petro ni Bwana! Punde aliposikia hilo, Petro alianguka bahali na kuogelea mpaka ufuoni.

Hata kama alikuwa amemwangusha mwokozi vibaya alikuwa amejua Yesu kwa mda mrefu na kujua kwamba hangekasirikia. Wakati Petro alijikwaa ufuoni Yesu alimwalika aje wale sitafutahi pamoja naya.

Baada ya kula na jazba ya Petro kupunguzwa, Yesu alimuuliza mara tatu kama bado alikuwa anampenda. Petro alikuwa amemkataa Yesu mara tatu, sasa ilikuwa ni fursa kwake kurejeshwa katika uhusiano na Bwana kwa kukuri mara tatu upendo wake kwa Yesu. Baada ya kukiri mara ya kwanza, Yesu alimwambia Petro, kalishe wanakondoo wangu; baada ya kukiri mara mbili, alisema, chunga kondoo wangu.

Baada ya mara tatu, alisema, "Lisha kondoo wangu. Petro alijukumishwa kwa mara nyingine na hivyo kuwa mmoja wa wale thenashara.

Baada ya wanafunzi kuvuta wavu ufuoni, walihesabu samaki. Walikuwa 153. katika huo kulikuwa na aina 153 ya samaki waliojulikana duniani kwa hiyo mavuno hayo kutoka ziwani yaliwakilisha aina zote za watu ambao kanisa litawanasa kwenye wavu wa ufalme wake (Matayo 13:47).

Kuna nyakati katika maisha ambapo utakuja ufuoni bila kitu cha kuonyesha baada ya kazi, ngumu. Lakini kuna mgeni anayekusubiri. Anakwambia unachofaa kufanya, na utakapofuata maagizo yake, utakutana na mafanikio ya kustaajabisha. Na hapo ndipo utakopogundua kuwa yule mgeni alikuwa Yesu. Atakwalika ule pamoja naye. Baada ya kupumzika na kula anajua kuwa umekuwa ukifanya kazi ngumu, na umechoka na u baridi atakufunulia kwamba anataka umfuate. Usijisugulishe na mipango ya watu wengine. Kazi yako ni kumfuata yeye. Siri ya maisha yaliyokamilika na yenye mafanikio ni kumfuata Yesu. Inaweza kukugharimu sana-kama ilivyotendeka kwa Petro (Yohana 21:18-19, II Petro 1:13-15)- Lakini gharama unayolipa ni ndogo sana ukilinganisha na zawadi yako ya umilele.

